# Nipashe

Jumatatu Januari 27, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580138

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Lipumba atiwa mbaroni polisi mkutano wa ndani

UKURASA 2




UKURASA 13

# Bunge laagiza Takukuru iwakate vigogo wizara

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 5

**VYAKULA VYA NJE SASA MARUFUKU MIGODINI**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameviagiza vyombo hivyo kuhakikisha kuanzia sasa vyakula kwenye migodi...

UKURASA WA 3

**MKAPA AWAPA NENO WANUFAIKA WAHISANI**

RAIS mstaafu Benjamini Mkapa amewataka Watanzania wanaonufaika na wahisani, kutumia fursa hiyo kujifunza...

## AHADI SAMIA UJENZI CHUO VETA IGUNGA BADO GIZA

UKURASA 3



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza wakati wa kufunga semina ya viongozi wa dola katika usimamizi na udhibiti wa rasilimali madini jijini Dodoma jana. **PICHA: OWM**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


## Upinzani waikosoa serikali 'zimamoto' ujenzi madarasa

UKURASA 2

**MICHEZO** KIWANGO SIMBA CHAMKERA SVEN UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

# Bunge laiagiza Takukuru kukamata vigogo wizara

Na Mwandishi Wetu, DODOMA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, imeagiza kukamatwa na kushtakiwa watendaji wa Kampuni ya Ranchi za Taifa (Narco), watendaji wakuu wa Wizara ya Mifugo na viongozi wa Kampuni ya Taifa ya Uwekezaji (Nicol) kutokana na kashfa ya uchotwaji wa Sh. bilioni 15.

Imeelezwa na chombo hicho cha kutunga sheria kuwa fedha hizo zilichotwa katika biashara ya uendeshaji wa machinjio ya Dodoma katika kipindi cha miaka 11 iliyopita.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mahmoud Mgimwa, amesema wamebaini watendaji wa Narco na Wizara ya Mifugo na Uvuvi waliohudumu katika kipindi cha kuanzia mwaka 2008 hadi mwaka 2015, walishirikiana kwa pamoja na Kampuni ya Nicol kuwaibia Watanzania fedha hizo, akisisitiza kuwa Bunge la 11 kamwe haliwezi kubariki wizi huo.

Alitoa agizo hilo alipozungumza kwenye ziara ya kamati hiyo kutembelea machinjio ya Dodoma ambayo kwa sasa yanaendeshwa na serikali baada ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, kuvunja mkataba huo baina ya Narco na Nicol ulioingiizia hasara serikali kwa kipindi cha miaka 11, huku wahusika waliohusika na kashfa hiyo wakiwa bado hawajachukuliwa hatua yoyote.

Mgimwa alieleza kushangazwa na usimamizi mbovu, ubadhirifu na ukiukwaji mkubwa wa mkataba wa uendeshaji wa machinjio hayo, akihoji uadilifu wa watendaji waliopewa dhamana kusimamia mali hiyo kwa niaba ya Watanzania.

Alihoji iweje tangu mwaka

INAENDELEA UK.8

## Polisi wamtia mbaroni Lipumba kikao cha ndani

Na Boniface Gideon, TANGA

WAKATI Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Wananchi (CUF), Prof. Ibrahim Lupumba, akianza kuonja shubiri ya kukamatwa na polisi kwa kufanya siasa nje ya wakati, Mkuu wa Wilaya ya Handeni mkoani Tanga, Godwin Gondwe, amesema uamuzi wa kumkamata ulilenga kumkumbusha kuwa yeye sio mbunge wala diwani.

Prof. Lipumba alikamatwa jana katika Kijiji cha Mbogoni, Kata ya Mgwe, Wilaya ya Handeni akiwa kwenye kikao cha ndani katika moja ya nyumba ya mwanachama wa chama hicho.

Baada ya kukamatwa kwa kiongozi huyo wa upinzani, Mkuu wa Wilaya hiyo, Godwin Gondwe, aliiambia Nipashe kuwa Prof. Lipumba alikamatwa ili kukumbushwa kuwa mikutano ya hadhara hairuhusiwi mpaka muda wa kampeni kwa wanasiasa walio nje ya maeneo yao.

"Tulikuwa tunakumbusha tu kuwa mikutano ya hadhara hairuhusiwi, isipokuwa madiwani na wabunge," alisema Godwe.

Aliongeza akisema: "Prof. Lipumba ni kiongozi mkubwa nchini, hivyo ni lazima serikali ifahamu ili ikiwezekana awekewe ulinzi. Yule ni kiongozi mkubwa lazima awe na ulinzi wa polisi hivyo tumemzuia ili kumkumbusha," alisema Gondwe.

Alipotafutwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Edward Bukombe, kutoa ufafanuzi kuhusu taarifa za kukamatwa kwa mwanasiasa huyo, hakupatikana kutokana na simu

INAENDELEA UK. 8



Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angeline Mabula, akizungumza na vibarua wa mradi wa ujenzi wa Ofisi ya Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Obadia Kita na Yusufu Kijalo alipokwenda kukagua maendeleo ya mradi huo unaojengwa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kwenye shamba la misitu la Iyondo Msimwa Ileje mkoani Songwe mwishoni mwa wiki. **PICHA: WANMM**


**THE COMPANIES ACT NO. 12 OF 2002**
**WINDING UP BY VOLUNTARILY**
**MAGRETH SCHOOLS (T) LIMITED**

**TANGAZO LA KUFUNGWA KAMPUNI**

Katika kikao cha wakurugenzi wa kampuni ya Magreth Schools (T) Limited kilichofanyika tarehe 8 January 2020 iliamuliwa kampuni ya Magreth Schools (T) Limited zifungwe shughuli zake kisheria.

Na kwamba shughuli zote zilizokuwa zikiendeshwa na kampuni hiyo tajwa hapo juu zitahamishiwa kwenye kampuni ya The Amazon Colleges Tanzania Limited.

Aidha bodi ya wakurugenzi wa kampuni ya Magreth Schools (T) Limited imemteua msimamizi atakayehusika na yeyote mwenye madai dhidi ya kampuni ambaye anuani yake ni.

**UBAIDI G. HAMIDU ( ADVOCATE)**
**LJ ADVOCATES,**
**LUMUMBA/AMANI STREE, KARIAKOO,**
**P.O.BOX 72382, DAR ES SALAAM,**
**MOB; 0755317060,068526844**

Kwa yeyote mwenye madai dhidi ya kampuni inayofungwa anaweza kuwasiliana naye siku za kazi kwanzia saa 2:30 asubuhi hadi saa 10:00.

Limetolewa leo tarehe 24 Januari 2020.

**Emmanuel Kayombo**
**Mkurufenzi mtendaji,**

115599902


## Upinzani wakosoa mpango ujenzi wa vyumba madarasa

Na Paul Mabeja, DODOMA

WAZIRI kivuli wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Suzan Lyimo, ameitaka serikali kuhakikisha inaweka mikakati endelevu ya kuondoa tatizo la uhaba wa vyumba vya madarasa kila mwaka.

Lyimo, aliyasema hayo jana jijini hapa wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu tatizo lililopo hivi sasa na ukosefu wa vyumba vya madarasa kwa wanafunzi waliochaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika mwaka wa masomo 2020.

Alisema kuwa kila mwaka serikali imekuwa na matamko ya kushtukiza kwa watendaji wake juu ya ujenzi wa vyumba vya madarasa kwa ajili ya wanafunzi wanaokuwa wanachaguliwa kujiunga kidato cha kwanza.

Waziri kivuli alisema matamko hayo yamekuwa hayana msaada wowote kwa wanafunzi hao ambao wamekuwa wakichaguliwa kujiunga kidato cha kwanza kutokana na wengi wao kukosa masomo kwa muda mwafaka.

"Hivi sasa kwa mkoa wa Dar es Saalam pekee yake tu kuna watoto 19,000 bado hawajaanza masomo na nilisikia hivi karibu wanadai kuwa wataanza Machi, hivyo wanakosa miezi miwili kabisa ukilinganisha na wengine walioanza Januari 6, mwaka huu," alisema Lyimo.

Lyimo alisema ipo haja kwa serikali kuweka mikakati hususani kwenye kutenga bajeti ambayo itasaidia kuondoa kabisa tatizo la uhaba wa vyumba vya madarasa kila mwaka.

"Ni lazima sasa serikali kuona ni jinsi gani bajeti inayopangwa inakwenda yote ili kuondoa tatizo hili la vyumba vya madarasa kwani hivi sasa unakuta bunge linatenga asilimia 100 ya bajeti, lakini inayokwenda ni asilimia 30, ambayo haitoshelezi mahitaji," alisema.

Alifafanua kuwa kutokana na uhaba wa madarasa hivi sasa watoto katika maeneo mengi ya nchi wanasomo katika stoo, na maturubai na wengine ofisi za walimu zimegeuka kuwa madarasa.

Vile vile, alisema kutokana hali hiyo ndio sababu kuu ya shule za serikali kufanya vibaya katika matokeo mbalimbali ya mitihani ya taifa ikilinganishwa na zile za binafsi.

"Sera ya elimu inadai kuwa darasa moja ni watoto 50, lakini hivi sasa baadhi ya shule kuna watoto 100, ndani ya darasa moja, hivyo mrundikano huo ni moja ya sababu ya watoto wetu kufanya vibaya, serikali inatakiwa kushirikiana na taasisi binafsi ili kujifunza wanachofanya kuondoa tatizo hili," alisema Lyimo.

Akizungumzi juu ya taasisi za elimu za serikali kutoa gawio, alisema suala hilo hakubaliani nalo kwa kuwa bado zinakabiliwa na matatizo mengi.

"Wanadai kuwa hili gawio pia ni kama mchango, lakini kwangu mimi naona kuwa hii siyo sahihi kwani sawa na mtu kwenda kumuona hospitali mgonjwa mahututi halafu bado ukala chakula chake," alisema.

HABARI KITAIFA

# Mkapa awapa neno wanufaika wahisani

**Na Asraji Mvungi,** MONDULI

RAIS mstaafu Benjamini Mkapa amewataka Watanzania wanaonufaika na wahisani, kutumia fursa hiyo kujifunza mbinu za kujitegemea na kujinyima kwa ajili ya wengine.

Mkapa aliyasema hayo jana wilayani Monduli mkoani Arusha, wakati akitoa salamu zake katika ibada maalum ya jubilee ya miaka 25 ya shule ya sekondari ya wasichana wa jamii ya wafugaji ya Maasai Girls, inayomilikiwa na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Kaskazini Kati na wahisani kutoka Marekani.

Alisema kuna haja Watanzania kujifunza kutofautisha na kuelewa kuwa wahisani wanavyotoa misaada, wanafanya hivyo kwa hiari yao na wakiamua kusitisha, hakuna mtu wa kuwauliza ama kuwalazimisha na ni tofauti na mkataba ambao mtu akisitisha unaweza ukamuuliza.

"Kwanza, nawashukuru wahisani wanaoendelea kutusaidia na ambao bado wanasaidia shule hii, lakini ninawauliza ninyi mnaosaidiwa sasa ni miaka 25 mmekuwa mkisaidiwa, mtasaidiwa hivi mpaka lini?" Alihoji.

"Mimi naona wakati umefika wa kujitathmini na kuchukua hatua ikiwamo ya kuanza kujiandaa kupata vyanzo vingine vya mapato ili hata wahisani wakichoka, miradi hii iwe endelevu ama siku wakisema basi hawatoi tena misaada, mtabadilisha lengo lenu la kuwasaidia hawa watoto wa wafuaji."

Katika hatua nyingine, Mkapa alizitaka jamii za wafugaji kubadilika na kuthamini elimu, vinginevyo dunia itazilazimisha kubadilika kwa kuwa kulingana na kasi ya mabadiliko, inayoendelea kujitokeza, hakuna njia ya mkato ya kukwepa kusomesha watoto wa jinsi zote.

"Inasikitisha sana kuona kwamba pamoja na umuhimu wa elimu ambao uko wazi, bado kuna watu wanapata msaada wa kusomeshewa watoto wao halafu wanakaa, na nimeambiwa wengine wanawatishia na kuwalaani watoto wanaotaka kusoma na pia kuwafanyia vitendo vya ushirikina, hili ni tatizo kubwa ndugu zangu wafugaji, badilikeni kwani inawezekana," alisema.

Awali, Mkuu wa KKKT nchini, DK. Fredrick Shoo na Askofu wa Dayosisi ya Kaskazini Kati, Dk. Solomon Masangwa, kwa nyakati tofauti walielezea umuhimu wa kuendelea kuimarishwa kwa ushirikiano kati sekta binafsi na serikali.

Mkuu wa KKKT, Dk. Shoo katika nasaha zake, aliwashukuru wahisani wa taasisi ya kidini ya OBA kutoka Marekani na Watanzania waliojitolea kwa hali na mali kuisaidia shule hiyo, akiwamo aliyekuwa Mwenyekiti wa Kampuni za IPP, marehemu Dk. Reginald Mengi. Wengine waliotajwa kuonyesha jitihada binafsi za kusaidia watoto wa wafugaji kupitia shule hiyo ni pamoja na Waziri Mkuu mstaafu, Edward Lowasa.

Shule hiyo ilianzishwa mwaka 1995 kwa ushirikiano wa Mchungaji Mmisionari David Simonson toka Marekani na aliyekuwa Askofu wa KKKT, Dayosisi ya Arusha ambayo sasa ni Dayosisi ya Kaskazini Kati kwa lengo la kuwasomesha wanafunzi wa kike wa jamii za wafugaji ambao hawapati fursa hiyo kutokana uelewa mdogo wa umuhimu wa elimu waliokuwa nao wazazi wao.

Kwa mujibu wa Askofu DK. Solomon Masangwa shule hiyo ilianzishwa ikiwa na wanafunzi wa kike 24 na kwa sasa ina wanafunzi 350 na wahitimu 1,007 wa kidato cha nne, 361 kidato cha sita na wengi wao sasa ni wataalamu wa fani mbalimbali wakiwamo madaktari, walimu, wahandisi, wanasheria na mmoja ni rubani.




Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria, Najma Giga (kushoto) na Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Augustine Mahiga, wakishuhudia mhudumu wa afya katika Hospitali ya Wilaya ya Frelimo katika Manispaa ya Iringa akitoa huduma ya usajili wa cheti cha kuzaliwa kwa mtoto wa umri chini ya miaka mitano jana, wakati ya ziara ya siku moja ya kamati hiyo mkoani Iringa. **PICHA FRIDAY SIMBAYA**

# Ujenzi chuo Veta bado kiza Igunga

**Na Mwandishi Wetu,** IGUNGA

IKIWA ni takriban miaka minne tangu Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, aahidi ujenzi wa Chuo cha Veta wilayani Igunga mkoani Tabora, ahadi hiyo bado haijatekelezwa.

Wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu mwaka 2015, Samia aliahidi kuwa serikali itahakikisha inakamilisha mradi wa ujenzi wa Chuo cha Veta Manonga kilichoko Choma wilayani hapa.

Hata hivyo, ujenzi huo umekwama kutokana na sababu mbalimbali, kubwa ikidaiwa kuwapo kwa mvutano wa viongozi kuhusu mahali pa kujengwa chuo hicho.

Mradi huo ulianzishwa mwaka 2005 na Shirika la World Vision, ambalo Agosti 28, mwaka jana, lilikabidhi kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Igunga eneo la Veta Manonga lenye ukubwa wa zaidi ya ekari 50.

Kwa mujibu wa Gasper Mgonja, mratibu wa mradi huo kutoka World Vision, wakati wanakabidhi eneo hilo, shirika lilikuwa limeweka nguvu ya kujenga madarasa manne na tayari kulikuwa na wanafunzi waliokuwa wanafundishwa kozi ya ushonaji na mwalimu aliyeajiriwa na serikali.

Shirika hilo pia liliahidi kukabidhi kwa serikali Septemba mwaka huu jengo la ofisi kuwa sehemu ya Veta Manonga. Eneo hilo lina ghala la mazao, mashine ya kukamua alizeti, mashine ya kukoboa mpunga, nyumba ya watumishi, kibanda cha mlinzi na kibanda cha jenereta.

Agosti 14, mwaka jana, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, William Ole Nasha, alizuru katika eneo hilo na kuwaagiza viongozi wa wilaya kuhakikisha mradi huo unatekelezwa.

Alisema serikali kupitia wizara yake inatarajia kutoa Sh. bilioni 1.5 kwa ajili ya uendelezaji wa chuo hicho cha Veta, lakini akaweka sharti kwamba fedha zitatolewa ikiwa tu uongozi wa halmashauri utakabidhi hati ya eneo la chuo hicho.

Kutokana na agizo hilo la Ole Nasha, viongozi wa halmashauri walipaswa kupeleka wataalamu ili kupima eneo hilo ili taratibu za ujenzi zifanywe na serikali.

Alipotafutwa na Nipashe mwishoni mwa wiki kuzungumzia suala hilo, Mkurugenzi wa Veta Kanda ya Magharibi, Wilhard Soko, alisema ujenzi wa mradi huo bado haujaanza kutokana na kutokamilika kwa taratibu ambazo hata hivyo hakuwa tayari kuziweka wazi.

Mkurugenzi huyo alimtaka mwandishi kumtafuta Mkurugenzi Mkuu wa Veta nchini, Dk. Pancras Bujuru, ili kupata ufafanuzi wa kina kuhusu mradi huo.

Alipotafutwa na gazeti hili, Dk. Bujuru alisema wanaendelea na ujenzi wa vyuo vya Veta nchi nzima na kwamba mradi wa Igunga bado haujaanza kutokana na halmashauri kutokamilisha taratibu zinazotakiwa.

"Kuna maelekezo ambayo tuliwapa, bado hawajatupa mrejesho. Wakishakamilisha, ujenzi utaanza mara moja. Tunaendelea kujenga vyuo nchi nzima kwa

INAENDELEA UK. 26

NHC
SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA
TUNAJENGA TAIFA LETU

## TAARIFA KWA UMMA

Shirika la Nyumba la Taifa linapenda kuwatangazia wapangaji wake wote wenye malimbikizo na waliohama na madeni wakiwamo watu binafsi, taasisi za umma, wakala za serikali na kampuni binafsi kulipa malimbikizo na madeni hayo katika kipindi cha siku 14 kuanzia tarehe ya tangazo hili na watakaoshindwa kufanya hivyo katika muda uliopangwa hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao. Shirika litawatangaza wadaiwa SUGU wote kwenye vyombo vya habari.

Kwa wale wanaofahamu kwamba upangaji wao ulipatikana kwa njia zisizo sahihi wanapaswa kutoa taarifa Makao Makuu ya Shirika ili kuweza kurasimishwa.

***Epuka usumbufu lipa kodi kwa wakati.***

**Imetolewa na:**

**OFISI YA MAWASILIANO KWA UMMA NA HUDUMA KWA JAMII**
**NHC- MAKAO MAKUU**

# UNITED BANK FOR AFRICA (TANZANIA) LIMITED

UBA

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA 31.12.2019

### Imetolewa chini ya kanuni ya 32 kifungu namba 3 ya kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2006

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31-DESEMBA 2019

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya 31-Dec-19 | Robo Mwaka ya 30-Sep-19 |
|---|---|---|---|
| | **A. MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 2 008 | 3 054 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 12 829 | 12 464 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 91 811 | 92 562 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 4 976 | 5 638 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 64 071 | 83 014 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 41 776 | 33 573 |
| 12 | Mali Nyingine | 4 842 | 5 483 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 1 538 | 1 318 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **223 851** | **237 106** |
| | **B. DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | - | - |
| 18 | Amana za Wateja | 111 095 | 118 784 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 15 265 | 16 582 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | 45 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 1 442 | 2 411 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 1 799 | 1 825 |
| 27 | Dhima Nyingine | 1 096 | 851 |
| 28 | Madeni | 72 788 | 76 826 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **203 484** | **217 325** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **20 367** | **19 781** |
| | **C. FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 31 420 | 31 420 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 29 104 | 29 104 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (42 166) | (42 166) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 2 009 | 1 423 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **20 367** | **19 781** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 841 483 | 847 525 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 234 | 232 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 891 | 592 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| | **D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 9% | 8% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 1% | 1% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 33% | 25% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 19% | 14% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 88% | 88% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -7% | -34% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -6% | -19% |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 DESEMBA 2019

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la ziada ya jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2019** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 31 420 | 29 104 | (42 568) | - | 402 | - | 18 358 |
| Faida/(Hasara) Halisi baada ya kodi ya mapato | - | - | 2 009 | - | - | - | 2 009 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| Share issued | | | - | | - | | |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **31 420** | **29 104** | **(40 559)** | **-** | **402** | **-** | **20 367** |
| **Mwaka uliopita 2018** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 31 420 | 29 104 | (39 454) | - | 351 | - | 21 421 |
| Faida/(Hasara) Halisi baada ya kodi ya mapato | - | - | - | - | - | - | - |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | (3 048) | - | - | - | (3 048) |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | (51) | - | - | - | (51) |
| Mengineyo | - | - | (16) | - | 51 | - | 35 |
| Share issued | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **31 420** | **29 104** | **(42 568)** | **-** | **402** | **-** | **18 358** |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 DESEMBA 2019

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo ya Mwaka ya sasa 31-Dec-19 | Robo ya Mwaka linganishi 30-Sep-19 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Dec-19 | Limbikizo la Mwaka linganishi 31-Dec-18 |
|---|---|---|---|---|
| **I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | **586** | **723** | **2 009** | **(2 168)** |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| - Hasara Katika Mali | 27 | 82 | 27 | (2 306) |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (8 204) | (885) | (8 204) | (7 039) |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | 429 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (9 007) | (70 401) | (9 007) | 12 526 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | 751 | (46 722) | 751 | 207 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 244 | (235) | 244 | 9 749 |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 642 | (583) | 642 | (6 644) |
| - Kodi Iliyolipwa | - | - | - | 1 397 |
| -Mengineyo (bainisha) | - | - | - | 568 |
| *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | **(14 962)** | **(118 022)** | **(13 538)** | **6 720** |
| **II. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (343) | (38) | (343) | (60) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | 1 |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | (445) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | **(343)** | **(38)** | **(343)** | **(504)** |
| ***III. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:*** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | (4 038) | 14 041 | (4 038) | (3 457) |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha*** | **(4 038)** | **14 041** | **(4 038)** | **(3 457)** |
| IV. Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu: | | | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | **(19 342)** | **(104 020)** | **(17 919)** | **2 759** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka | 135 644 | 239 664 | 135 644 | 81 294 |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka | **116 301** | **135 644** | **117 725** | **84 053** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 DESEMBA 2019

(Kiasi kwa shilingi millioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa 31-Dec-19 | Robo ya Mwaka linganishi 30-Sep-19 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Dec-19 | Limbikizo la Mwaka linganishi 31-Dec-18 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 4 423 | 4 063 | 12 515 | 8 567 |
| 2 | Gharama za Riba | (1 702) | (1 400) | (4 634) | (2 872) |
| **3** | **Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2)** | **2 722** | **2 664** | **7 881** | **5 696** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (298) | (181) | (480) | (37) |
| **6** | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **1 584** | **1 811** | **8 335** | **5 298** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 371 | 320 | 1 408 | 1 105 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 1 199 | 1 474 | 6 822 | 3 425 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 14 | 17 | 106 | 768 |
| **7** | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(3 421)** | **(3 571)** | **(13 728)** | **(13 125)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (1 658) | (1 669) | (6 367) | (6 068) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | (300) | (319) | (1 247) | (1 332) |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (1 464) | (1 584) | (6 115) | (5 724) |
| **8** | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **586** | **723** | **2 009** | **(2 168)** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | - | - | - | - |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **586** | **723** | **2 009** | **(2 168)** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - | - | - |
| **12** | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **586** | **723** | **2 009** | **(2 168)** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 114 | 117 | 114 | 105 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 93 | 115 | 320 | (345) |
| **15** | **Idadi ya Matawi** | 4 | 4 | 4 | 4 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| | (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.25% | 0.30% | 0.25% | -1.49% |
| | (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 2.92% | 3.65% | 2.92% | -11.18% |
| | (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 56.95% | 60.79% | 56.95% | 94.66% |
| | (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 1.34% | 1.27% | 1.34% | 4.87% |

| | *Jina na Cheo* | *Saini* | *Tarehe* |
|---|---|---|---|
| 1 | Usman Isiaka<br>**Mkurugenzi Mtendaji** | *Imesainiwa* | *27th January 2020* |
| 2 | Chomete Hussein<br>**Mkuu wa Fedha** | *Imesainiwa* | *27th January 2020* |
| 3 | Joseph Ringa<br>**Mkaguzi Mkuu wa Ndani** | *Imesainiwa* | *27th January 2020* |

Katika kuanda taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8).

| | *Jina na Cheo* | *Saini* | *Tarehe* |
|---|---|---|---|
| 1 | Amb.Tuvako Manongi<br>**Mwenyekiti wa Bodi** | *Imesainiwa* | *27th January 2020* |
| 2 | Oliver Alawuba<br>**Mkurugenzi** | *Imesainiwa* | *27th January 2020* |

215599602

United Bank for Africa (T) Ltd is a subsidiary of United Bank for Africa Plc, a leading Pan African bank offering universal banking to more than 13 million customers in over 1000 branches and outlets in Africa, USA and Europe.

**East & South Africa**
- Tanzania
- Kenya
- Congo DRC
- Mozambique
- Uganda
- Zambia

**Central Africa**
- Cameroon
- Gabon
- Tchad
- Congo Brazzaville

**West Africa**
- Ghana,
- Benin
- Burkina Faso,
- Cote D'Ivoire (CDI)
- Liberia
- Sierra Leone
- Senegal
- Mali
- Guinea

**Europe**
- UK
- France

**USA**
- New York

HABARI KITAIFA

# Majaliwa apiga marufuku vyakula vya nje migodini

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameviagiza vyombo hivyo kuhakikisha kuanzia sasa vyakula kwenye migodi havitoki nje ya nchi na badala yake watumie vinavyozalishwa nchini.

Pia amekemea ukamataji holela wa wawekezaji na wadau wa madini, akivitaka vyombo vya ulinzi na usalama kufuata sheria, kanuni na miongozo inayosimamia sekta hiyo.

Majaliwa alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akifunga semina maalum ya vyombo vya ulinzi na usalama kuhusu usimamizi wa rasilimali madini iliyofanyika jijini hapa.

Alisema katika kipindi cha hivi karibuni, kumejitokeza malalamiko mengi kutoka kwa wawekezaji na wadau wa madini kuhusu kukamatwa au kubughudhiwa bila sababu za msingi.

"Natumia nafasi hii kukemea suala la ukamataji holela wa wawekezaji au wadau wa madini pasipo kufuata taratibu. Hivyo basi, tumieni sheria, kanuni na miongozo mbalimbali iliyowekwa mahsusi kwa ajili ya kuimarisha usimamizi wa sekta ya madini," aliagiza.

Alisema uanzishaji wa masoko ya madini ni sehemu ya mkakati mahsusi wa serikali kupunguza utoroshwaji wa madini kwa kuwa awali ilionekana kuna utoroshaji mkubwa unaofanyika kwa kisingizio cha kutafuta soko.

"Hata hivyo, kuna tatizo lingine limeanza kujitokeza la kuwakamata wadau wakiwa na madini hata kama wanapeleka sokoni," alisema.

Aliagiza kuanzia sasa wadau wote wanaopatikana na madini, wapewe utaratibu wa kuelekea sokoni kuuza badala ya kuwakamata wakiwa wanaenda sokoni.

"Ni wajibu wetu kusimamia na kudhibiti utoroshwaji wa madini na pia ni jukumu letu sisi kama vyombo vya ulinzi na usalama kuhakikisha kuwa masoko haya pamoja na wafanyabiashara ya madini wanaofanya kazi zao kwa kufuata sheria wanalindwa na kuepuka kamata kamata zisizo na tija," aliagiza.

Alisema kuna wakati hawahitaji kutumia nguvu nyingi bali kutoa ushauri tu ili kutatua shida husika.

Kuhusu vyakula, Waziri Mkuu alisema vyombo hivyo vinapaswa kuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha huduma za vyakula migodini kuanzia sasa hazitoki nje ili bidhaa zilizopo nchini zitumike.

"Unakuta mchele wanaoutumia wafanyakazi wa migodini unatoka nje, jambo ambalo halikubaliki kwa sababu mchele tunalima sisi wenyewe, hivyo naagiza suala hilo likafanyiwe mabadiliko," alisema.

Waziri wa Madini, Dotto Biteko, alitangazia 'vita' dhidi ya watu wanaouza madini feki na kuwataka waache mara moja kwa kuwa tayari wamewabaini.

"Tunaomba wanaofanya hivyo waache mara moja, tunaanza msako wa kuwatafuta watu wa aina hii," alionya.

# Waziri atoa miezi mitano ujenzi soko

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo (pichani), amekerwa na kukithiri kwa uchafu katika Soko la Sabasaba jijini Dodoma, huku akiagiza ujenzi kuanza kabla ya Juni mwaka huu.



Agizo hilo alilitoa jana jijini hapa baada ya kutembelea soko hilo kujionea hali ya uchafu.

Katika ziara hiyo, Jafo alijionea mifereji ya maji ya mvua ikiwa imejaa uchafu, jambo ambalo linahatarisha afya za wafanyabiashara wa eneo hilo.

Akizungumza na wafanyabiashara wa soko hilo, waziri huyo alisema hakutarajia kushuhudia soko la aina hiyo linalohatarisha afya za watu kwenye jiji linalokusanya mapato zaidi ya Sh. bilioni 71.

"Nataka Soko la Sabasaba kabla ya mwaka wa fedha kuisha, ujenzi uanze kwenye soko hili, mrekebishe mazingira ya wafanyabiashara, haiwezekani mkusanye zaidi ya Sh. bilioni 71 halafu mkaliacha hili soko hivi," alionya.

Jafo pia aliutaka uongozi wa jiji hilo kuachana na ujenzi wa hoteli ya nyota tatu ili uboreshe kwanza mazingira ya wafanyabiashara wa soko hilo.

Aliutaka uongozi huo kuhakikisha unasimamia usafi ili kulinda afya na usalama wa wafanyabiashara na wananchi kwa ujumla.

Kaimu Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Mkufya Msekeni, alisema tayari wameshaandaa mchoro kwa ajili ya kujenga soko hilo.

Awali, mfanyabiashara aliyekutwa na waziri sokoni hapo, alisema kwa muda mrefu wamekuwa wakizungumzia suala la uchafu katika soko hilo, lakini hakuna hatua zozote zilizochukuliwa.

"Hili soko wafanyabiashara wa Majengo na Chang'ombe wanakuja kuchukua bidhaa, lakini limetelekezwa, halifanyiwi usafi, mifereji ya kupitishia maji hakuna, mazingira kwa ujumla ni machafu, kipindupindu hapa kipo nje nje, Waziri tunaomba utusaidie," alisema.


UNITED BANK FOR AFRICA (TANZANIA) LIMITED
MINIMUM DISCLOSURE OF CHARGES AND FEES

| S/N | ITEM/TRANSACTION | | |
|---|---|---|---|
| SECTION A | SAVINGS ACCOUNTS | RETAIL | CORPORATE |
| 1 | FREEDOM SAVINGS | | N/A |
| | Required minimum opening balance | TZS 5,000 | |
| | Minimum operating balance | TZS 2,000 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges | NIL | |
| 2 | GENERAL SAVINGS | | N/A |
| | Required minimum opening balance | TZS 20,000 | |
| | Minimum operating balance | TZS 5,000 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges | TZS 1,000 | |
| 3 | EMPLOYEE SAVINGS | | N/A |
| | Required minimum opening balance | TZS15,000 USD 15 | |
| | Minimum operating balance | TZS 2,000 USD 10 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Adhoc statement request | TZS 1,000/ PAGE | |
| | Withdrawal Charges @ Counter | TZS 1,000 | |
| 4 | SAVINGS ACCOUNT INDIVIDUALS | | N/A |
| | Required minimum opening balance | 15 000 | |
| | Minimum operating balance | 5 000 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges @ Counter | TZS 1,000 | |
| 5 | SAVINGS ACCOUNT SALARY | | N/A |
| | Required minimum opening balance | 15 000 | |
| | Minimum operating balance | 5 000 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges @ Counter | TZS 1,000 | |
| 6 | SAVINGS ACCOUNT DOMICILARY | | |
| | Required minimum opening balance | USD10 | |
| | Minimum operating balance | USD 5 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges | 1% per Transaction | |
| | Closing account | USD 5 | |
| 7 | U-CARE CHILDREN SAVINGS | | N/A |
| | Required minimum opening balance | TZS 20,000 USD 15 | |
| | Minimum operating balance | TZS 20,000 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges | TZS 1,000 | |
| SECTION B | CURRENT ACCOUNTS | | |
| 1 | INDIVIDUAL CURRENT ACCOUNT | | BUSINESS CURRENT ACCOUNT |
| | Required minimum opening balance | TZS 30,000 | TZS 100,000 |
| | Minimum operating balance | TZS 10,000 | TZS 100,000 |
| | Monthly maintenance fee | TZS 10,000 | TZS 12,000 |
| | Cash withdrawal at counter | 1 PER MILLE | TZS A/C 1 PER MILLE |
| | Closing account | TZS 10,000 | TZS 10,000 |
| | Penalty for overdrawn account | PLR + 10% | TZS A/C PLR + 10% |
| 2 | DIPLOMAT ACCOUNTS | | |
| | Required minimum opening balance | USD 200 | N/A |
| | Minimum operating balance | USD 100 | N/A |
| | Monthly maintenence fee | NIL | N/A |
| | Cash withdrawal at counter | NIL | N/A |
| | Closing account | NIL | N/A |
| | Penalty for overdrawn account | NIL | N/A |
| | Outward fund transfers(TTs) | MIN USD 50 in between 0.25% MAX USD 200 | N/A |
| | Inward fund transfers(TTs Incoming) | NIL | N/A |
| | FOREX exchange | Favourable rates will be applied | N/A |
| 3 | DOMICILIARY CURRENT ACCOUNT | | |
| | Required minimum opening balance | USD 100/ EUR 100/ GBP 100 | USD 100/ EUR 100/ GBP 100 |
| | Minimum operating balance | USD 100/ EUR 100/ GBP 100 | USD 100/ EUR 100/ GBP 100 |
| | Monthly maintenence fee | USD 12 or its equivalent | USD 15 or its equivalent |
| | Minimum search fees | USD 25/ EUR 25/ GBP 25 | USD 25/ EUR 25/ GBP 25 |
| | Cash withdrawal | 1% per Transaction | 1% per Transaction |
| | Cheque book - 25 LEAF | USD 10 or its equivalent | N/A |
| | Closing account | USD 10 | USD 10 |
| | Penalty for overdrawn account | PLR + 2% | PLR + 2% |
| | Transfer From TZS to DOMICILIARY/ DOMICILIARYto TZS | NIL | NIL |
| SECTION C | DEPOSIT ACCOUNTS | | |
| 1 | Call Accounts | | Call Accounts |
| | Minimum opening balance | TZS 1,000,000 | TZS 10,000,000 |
| | Minimum operating balance | TZS 1,000,000 | TZS 10,000,000 |
| | Monthly Average balance requirement | Negotiable | Negotiable |
| | Interest Rates | Negotiable | Negotiable |
| 2 | Term Deposits | | Term Deposits |
| | Minimum deposit - local currency | TZS 500,000 | TZS 10,000,000 |
| | Minimum deposit - USD | USD 1,000 | USD 10,000 or equivalent |
| | Interest Rates | Negotiable | Negotiable |
| SECTION D | ELECTRONIC BANKING | | |
| 1 | E-Banking | | E-Banking |
| | Internet banking monthly subscription | TZS 2,000 Per Month. | TZS 10,000 per Month |
| | Internet banking ( Re issue pin) | TZS 5000 | TZS 5000 |
| | U - Direct (Reversal of transaction) | TZS 4000 | TZS 4000 |
| | E-statement (self downloaded) | FREE | FREE |
| | POS purchase (Local) | FREE | N/A |
| | POS purchase (International) | TZS 6000 (up to 1000$) TZS 10,000 ($1001 - $2000) TZS 20,000 (Above $ 2000) | N/A |
| | ATM reversal | TZS 1,000 per transaction | N/A |
| | Fund transfer/ company load | TZS 1,000 per transaction | TZS 1,000 per transaction |
| | Card Load | TZS 1,000 per transaction | TZS 1,000 per transaction |
| | Manual pin change | TZS 1,500 per transaction | TZS 1,500 per transaction |
| | U-MOBILE(mobile banking-Bank to wallet) | TZS 1,000 (0 - 200,000/=) and TZS 2,000 (200,001 - 400,000/=) | N/A |
| | Card to card transfer | TZS 1,500 per transaction | TZS 1,500 per tr |
| | Africash | TZS 6000 + 1.5% of the amount sent/USD 4.45 + 1.5% | N/A |
| 2 | Visa Debit Card | | N/A |
| | Issuance fees | TZS 10,000 | |
| | Re-issuance fee | TZS 10,000 | |
| 3 | Visa Perapid Cards | | N/A |
| | Issuance fees for instant card | TZS 12,000 | |
| | Issuance fees for personalized card | TZS 16,000 | |
| | Re-issuance fees | TZS 12,000 | |
| | Online Passcode reset fee | TZS 1,500 | |
| | ATM Pin reset fee | TZS 1,500 | |
| | Loading fee | TZS 1,000 | |
| | Online shopping fee - Local transactions | FREE | N/A |
| | Online shopping fee/Web - Int. transactions | TZS 6000 (up to 1000$) TZS 10,000 ($1001 - $2000) TZS 20,000 (Above $ 2000) | N/A |
| 4 | ATM Withdrawals | | N/A |
| | At UBA ATMs (On us) | TZS 500 | |
| | ATM Balance inquiry(Local) | TZS 200 | |
| | ATM Balance inquiry(international) | TZS 1000 | |
| | To other banks ATM (On others/OFF US)Local | TZS 2,500 | |
| | international ATM withdraw | TZS 6000 | |
| SECTION E | ASSET BANKING | | |
| 1 | LOANS | | |
| | Processing fee | negotiable | 2% |
| | Insurance for personal loans | N/A | 1.50% |
| | Legal fees | 0.5% minimum of TZS 300,000 | 0.5% minimum of TZS 300,000 |
| 2 | TEMPORARY OVERDAFT (TODs) | | |
| | Processing fee | 2% | 2% |
| SECTION F | TRADE FINANCE | | |
| 1 | Guarantees | | Guarantees |
| | Facility Commission | 2% p.a (0.5% per qtr). Min USD 250 per qrt. | 2% p.a (0.5% per qtr). Min USD 250 per qtr. |
| | Arrangement fees | 2% | 2% |
| | Cash Covered | 0.5% per qtr Min 250 per qtr | 0.5% per qtr Min 250 per qtr |
| | Amendment | USD 100.00 flat | USD 100.00 flat |
| | Extension to next quarter | 0.5% per qtr ( Or % of the agreed rate) | 0.5% per qtr ( Or % of the agreed rate) |
| | Amount increase | 0.5% /qtr on the diff ( Or % of the agreed rate) | 0.5% /qtr on the diff ( Or % of the agreed rate) |
| 2 | Letters of Credit - Imports | | Letters of Credit - Imports |
| | Issuance commision | 0.5% per quarter. Min USD 150. | 0.5% per quarter. Min USD 150. |
| | Handling Fees | USD 100 flat | USD 100 flat |
| | Swift charge | USD 50 flat | USD 50 flat |
| | Amendment | USD 100.00 flat | USD 100.00 flat |
| 3 | Letters of Credit - Exports | | Letters of Credit - Exports |
| | LC Advising Commission | USD 200 flat | USD 200 flat |
| | Amendment advising commision | USD 100 Flat | USD 100 Flat |
| | Correspondences Swift charge | USD 50 flat | USD 50 flat |
| | Documents handling and examination fee | 1.5% of invoice amount ,min usd 200 | 1.5% of invoice amount ,min usd 200 |
| | Courier charge | USD 100 flat | USD 100 flat |
| | LC confirmation charges | 1.5% per quarter (only for confirmed usance lcs) | 1.5% per quarter (only for confirmed usance lcs) |
| 4 | Letters of Credit Refinancing | | Letters of Credit Refinancing |
| | Interest on refinance | LIBOR + 8% p.a of value. Min USD 100 | LIBOR + 8% p.a of value. Min USD 100 |
| | Commission on refinance | USD 50 flat | USD 50 flat |
| 5 | Discounting on LC/Invoice/Cheque | | |
| | Interest on discounting | LIBOR + 8% p.a of value. Min USD 100 | LIBOR + 8% p.a of value. Min USD 100 |
| | Commission on discounting | USD 50 flat | USD 50 flat |
| 6 | Bills Discounting (Bills of exchange including cheques) | | |
| | Interest on discounting | PLR +3%-local; International Lobor+8% | PLR +3%-local; International Lobor+8% |
| 7 | Documentary Collection - Export | | |
| | Handling charge | 0.25% of the invoice min USD 100 flat | 0.25% of the invoice min USD 100 flat |
| | Courier charge | USD 100 | USD 100 |
| | Corespondence commission | USD 50 Per tracer | USD 50 Per tracer |
| 8 | Documentary Collection - Import | | |
| | Handling Commission | 0.25%. Min USD 100 | 0.25%. Min USD 100 |
| | correspondence Swift charge | USD 50 | USD 50 |
| 9 | Outward Bills for Collection (clean collections & TCs) | | |
| | Handling Commision | 0.25% of value, min USD 75 or its equivalent | 0.25% of value, min USD 75 or its equivalent |
| | Dhl charges | usd 75 flat | usd 75 flat |
| | Returned foreign cheques | claimed charges + locally un re-covered charges | claimed charges + locally un re-covered charges |
| 10 | Inward Bills for Collection | | |
| | Handling Commission | USD 50 flat per collection | USD 50 flat per collection |
| | Swift charged | USD 40 flat per collection | USD 40 flat per collection |
| 11 | Local Currency Transactions | | Local Currency Transactions |
| | Outward remittances (TISS) | TZS10,000 PER TRANSACTION | TZS10,000 PER TRANSACTION |
| | Amendment fee for Outward remittances / Swift / Telegraphic Transfers by customer or by bank | TZS 10,000.00 OR ITS EQUIVALENT | TZS 10,000.00 OR ITS EQUIVALENT |
| | Inward Swift Transfers (TISS) | NIL | NIL |
| 12 | Foreign Currency Transactions | | Foreign Currency Transactions |
| | Outward remittances / Swift / Telegraphic Transfers | MIN USD 50 in between 0.25% MAX USD 500 | MIN USD 50 in between 0.25% MAX USD 500 |
| | Telegraphic Overseas Charges/ OURS | USD/EUR/GBP 35 FLAT (OURS) | USD/EUR/GBP 35 FLAT (OURS) |
| | Amendment fee for Outward remittances / Swift / Telegraphic Transfers by customer or by bank | USD 10 FLAT | USD 10 FLAT |
| | Inward Swift Transfers | USD 10 FLAT | USD 10 FLAT |
| | International Money Order (IMO) | USD 30 per IMO | USD 30 per IMO |
| | Foreign cheques for collection | 0.25% of value. USD 75 min; USD 250 max; | 0.25% of value. USD 75 min; USD 250 max; |
| SECTION G | OTHERS | | |
| 1 | Statements | | Statements |
| | Monthly | FREE | FREE |
| | Adhoc requests | TZS 1,000/ PAGE | TZS 1,000/ PAGE |
| 2 | Cheque Books Issuing | | Cheque Books Issuing |
| | - 25 Leaf | TZS 15,000; USD 10 | N/A |
| | - 50 Leaf | TZS 30,000; USD 20 | N/A |
| | - 100 Leaf | TZS 45,000; USD 30 | TZS 45,000; USD 30 |
| | Counter cheque request | TZS 20,000; USD 10 | TZS 20,000; USD 10 |
| | Cheque Stop payment instructions | leaf lost: TZS 20,000; Book lost: TZS 40,000; | Leaf lost: TZS 20,000; Book lost: TZS 40,000; |
| | Issuance of Manager's cheque | TZS 25,000; USD 20 per item | TZS 25,000; USD 20 per item |
| | Managers cheque cancellation charges | FREE | FREE |
| 3 | Standing order | | Standing order |
| | Standing order set-up | TZS 10,000; USD 10 or its equivalent | TZS 10,000; USD 10 or its equivalent |
| | Standing order maintanance | NIL | NIL |
| | Standing order/Foreign Bank (TT charge) | MIN USD 50; 0.25% MAX USD 500 | MIN USD 50; 0.25% MAX USD 500 |
| | Amend / Stop standing Order | TZS 10,000; USD 10 or its equivalent | TZS 10,000; USD 10 or its equivalent |
| | Unpaid standing order | TZS 40,000; USD 40 or its equivalent | TZS 40,000; USD 40 or its equivalent |
| 4 | Insufficient funds/effects not cleared | | Insufficient funds/effects not cleared |
| | Effects not cleared | ITEM REMOVED | ITEM REMOVED |
| | Insufficient Funds (Refer to drawer) | TZS 50,000; USD 50 | TZS 50,000; USD 50 |
| 5 | Other services/charges | | |
| | Retriving old documents (2-6 months) | TZS 10,000; USD 10 | TZS 10,000; USD 10 |
| | Retriving documents (6 months and above) | TZS 15,000; USD 15 | TZS 5,000; USD 15 |
| | Confirmation/Audit/ Certificate of balance | TZS 50,0,000; USD 25 or its equivalent | TZS 50,0,000; USD 25 or its equivalent |
| | Status enquiry / Reference Letters | TZS 25,000; USD 25 or its equivalent per customer request | TZS 25,000; USD 25 or its equivalent |
| | Manual processing of salaries | TZS 1,000; USD1 or its equivalent | TZS 1,000; USD1 or its equivalent |
| | Closure of Account | TZS10,000 | TZS10,000 |
| | Dormant Account Reactivation | FREE | FREE |
| | Cash handling fee-COINS ONLY | 9% of the Deposit | 9% of the Deposit |
| 6 | Soiled notes | 3% of principal amount | 3% of principal amount |
| 7 | Coins | 3% of principal amount | 3% of principal amount |
| | | | |
| | approved by: | | |
| | Signature: | | Signature: |
| | | | |
| | Flavia Kiyanga | | Chomete Hussein |
| | Chief Operating Officer | | Country Chief Finance Officer |
| | United Bank for Africa (Tanzania) Ltd | | United Bank for Africa (Tanzania) Ltd |
| | Disclaimer: All fees are VAT exclusive. | | |

215599602

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Maandalizi ya fainali za CHAN yasiwe zimamoto

**TIMU** ya soka ya Taifa (Taifa Stars), imefanikiwa kufuzu kwa mara ya pili kushiriki fainali za mwaka huu za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN).

Fainali hizo zimepangwa kufanyika kuanzia Aprili 4 hadi 25, mwaka huu katika miji mitatu ya Cameroon ambayo ni pamoja na Yaounde, Douala na Limbe huku droo kwa ajili ya kupanga ratiba ya fainali hizo itafanyika Februari 17, mwaka huu mjini Yaounde.

Taifa Stars ilipata tiketi ya kushiriki fainali hizo baada ya kuwaondoka majirani zetu Kenya (Harambee Stars) na Sudan ambayo pia iko kwenye ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

Mara ya kwanza Taifa Stars kufuzu michuano hiyo inayoandaliwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (Caf), ilikuwa mwaka 2008, ikiwa chini ya Kocha Mkuu raia wa Brazil, Marcio Maximo.

Ili Taifa Stars iweze kwenda kufanya vema katika fainali hizo, inatakiwa iwe na maandalizi sahihi na kuacha mazoea ya kujiandaa kwa zimamoto.

Nipashe imeamua kukumbusha kuhusu maandalizi ya timu hii, kwa sababu inaamini maandalizi bora ndiyo yanayotoa matokeo chanya katika mashindano yoyote au mchezo wowote hapa duniani.

Katika mafanikio hakuna njia ya mkato, ni lazima wachezaji wa Taifa Stars wapewe maandalizi yanayolingana na ukubwa wa michuano ambayo wanatarajia kwenda kuchuana huko Cameroon.

Ni wazi na kanuni zinajulikana kuwa mashindano hayo yanashirikisha wachezaji wanaocheza katika ligi za ndani. Kwa hapa Tanzania nyota wanaounda kikosi hicho asilimia 99 wanatarajiwa kutoka kwenye Ligi Kuu Bara.

Ni wakati huu Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), inatakiwa kukaa karibu na vilabu vyake na kuwaeleza umuhimu wa kuandaa vema timu zao na kuhakikisha wachezaji wote wanahudhuria kikamilifu programu za mazoezi kwa sababu mwisho wa siku, nyota ambao wameonekana imara ndiyo watakaoitwa katika kikosi cha CHAN.

Kwa faida ya nchi, sio vibaya kwa Kocha Mkuu wa Taifa Stars Mrundi Etienne Ndayiragije kukutana na makocha wa klabu za Ligi Kuu Bara kubadilishana mawazo, lakini kikiwa na msingi wa kuwapa fursa zaidi wachezaji wazawa kucheza ili kuwaimarisha na kuwaongezea uzoefu.

Tunaamini kuwa vikao hivyo vitakavyoandaliwa mbali na kulenga kuisaidia Stars, lakini pia vitasaidia kuboresha vikosi vyao na kuonyesha ushindani katika mechi za Ligi Kuu na mashindano ya Kombe la FA yanayoendelea hapa nchini.

Pia wachezaji wanatakiwa wasisubiri kuimarika kwa kutegemea mazoezi ya timu, kila mchezaji anayeamini ana nafasi ya kuitwa kwenye kikosi hicho cha Ndayiragije, anatakiwa kujipangia mazoezi binafsi ambayo yatamjenga na kumweka tayari kwenda kupambana na nyota wa timu za Magharibi au Afrika ya Kati.

Fainali hizo ni sehemu nyingine muhimu ya wachezaji kujiweka sokoni ili kununuliwa na timu za nje ya Tanzania au za mataifa ya Ulaya.


Tumeshuhudia wachezaji wa Afrika Magharibi wakipata timu Ulaya baada ya kumalizika kwa Fainali za CHAN au zile za AFCON ambazo zimezoeleka kwa mawakala kutoka klabu mbalimbali.

Lakini pia tunawakumbusha wachezaji kuwa na nidhamu bora ambayo ndiyo msingi wa kila jambo. Hakuna mwanamichezo yoyote ambaye amefanikiwa hali ya kuwa nidhamu yake ni mbovu.

Kama wachezaji wa mataifa mengine ya Afrika wamepata fursa ya kusajiliwa Ulaya kupitia fainali hizi, huu ni wakati mwingine wa wachezaji wa Tanzania kujipanga kutumia fainali hizi kujitangaza na baadaye watafaidi matunda ya kujituma na kujitunza, huku pia wakipeperusha vema bendera ya Tanzania.

Nipashe inaamini endapo maandalizi yatafanyika vizuri kupitia kwa TFF ambayo imepewa dhamana ya kusimamia soka nchini, Stars itakwenda Cameroon kushindana na si kusindikiza timu nyingine kama ilivyokwenda Cairo katika fainali za Afcon hapo mwaka jana.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Kwa Simba hii, kimataifa bado

**TUMEIONA** timu ya Simba kwenye mechi mbalimbali za Ligi Kuu, Kombe la Mapinduzi na Kombe la FA siku ya Jumamosi ilipoichapa Mwadui mabao 2-1 kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Kocha Mkuu wa klabu hiyo, Sven Vandenbroeck, ameonyesha kutoridhishwa na baadhi ya madhaifu yaliyopo kwenye kikosi chake, hasa kuruhusu magoli katika mechi kadhaa ambazo imecheza mpaka sasa, japo inashinda.

Lakini akasema kuwa kwenye mechi hiyo kipindi cha kwanza timu ilicheza taratibu sana, huku pia tatizo lingine ni kutotumiwa vema kwa nafasi ambazo zinatengenezwa.

Hii si mara ya kwanza kwa kocha huyo kulalamikia timu yake kutokuwa na kasi kwenye baadhi ya mechi zake.

Kwa jinsi Simba ilivyo haswa kwa mchezaji mmoja mmoja, ni hatari na tishio kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, na hata Kombe la FA japo kuna wakati inapata ushindi kwa tabu.

Kuna uwezekano mkubwa kwa jinsi kikosi kilivyo kwa soka la Tanzania, ikawa bingwa na kuiwakilisha nchi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, au Kombe la Shirikisho Afrika.

Kwa jinsi inavyocheza sasa zidhani kama Simba hii ina kikosi cha kufanya vema kwenye michuano hiyo mikubwa barani Afrika, labda baada ya hapo yafanyike mabadiliko katika baadhi ya idara zenye mapungufu.

Vinginevyo, haiwezi kucheza hata na timu za Ethiopia, Comoro, Djibouti, Botswana au Eswatini ikawa na uhakika wa moja kwa moja kuibuka na ushindi.

Simba ina mapungufu mengi ambayo yanashindwa tu kuadhibiwa na timu za Tanzania ambazo zina hofu zikicheza nayo, badala yake zinakuwa zinatafuta sare tu, badala yake wachezaji wa timu pinzani wanafanya kazi kubwa ya kupoteza muda kuliko kucheza mpira.

Kama ikikutana na timu ambayo inataka hasa ushindi kwa Simba, na ikashambulia mfululizo, inakuwa kwenye matatizo makubwa muda wote.

Shida ya Simba inaanzia kwa mabeki hasa wa kati ambao inaonekana ni kama wamechoka na hawana kasi tena. Mashambulizi ya kushtukiza ya wapinzani wanayofanya kwenye lango la Simba, yanaweka mabeki hao matatani na kushindwa la kufanya.

Pia mabeki hao hawamfuati adui ili kumsumbua na kutomruhusu kuliona goli na kupiga kwa uhuru, badala yake wote wamekuwa wakirudi nyuma na kumtazama adui nini atafanya, matokeo yake mashuti mengi yamekuwa yakipigwa langoni mwao kwa sababu ya kuwapa uhuru wapinzani wao kuchagua cha kufanya.

Hapa ukikutana na wachezaji au timu yenye uwezo mkubwa umekwisha.

Viungo wakabaji wa timu hiyo wamekuwa hawafanyi kazi yao barabara na kuwaweka kwenye heka heka kubwa mabeki na kipa wao.

Viungo washambuliaji wa Simba, pamoja na uwezo wao mkubwa wa kupiga chenga, kuchezea mpira, lakini wamekuwa na tatizo la kupiga pasi za mwisho.

Ni kwa sababu hawazipigi kwenye muda sahihi, wanapenda sana kukaa na mpira bila sababu yoyote na hawana kasi.


Hata Simba inaposhambuliwa na kupokonywa mpira, viungo wa Simba wanashindwa kupiga pasi ndefu kwa ajili ya kufanya mashambulizi la kushtukiza, badala yake wanaanza pasi fupi na kuwafanya wapinzani wao kurejea nyuma haraka na kujipanga vizuri.

Kwenye nafasi ya ushambuliaji kwa sasa inaonekana ni butu kwa sababu inachezesha straika mmoja, Meddie Kagere ambaye kiasili ni mfungaji tu, lakini si mpambanaji na mwenye uwezo wa kuweka mpira miguuni, huku akiminyana na mabeki kama John Bocco.

Kwa maana hiyo Simba kama itapata nafasi ya kucheza kimataifa inahitaji mabeki wawili wa kati wenye uwezo mkubwa, viungo mkabaji mmoja kwenye viwango vya kimataifa, lakini mastraika wawili wa kuwasaidia waliopo, na kutowachezesha kwa pamoja viungo washambuliaji ambao hawana kasi. Hapa inawezekana ikawa kwa asilimia kubwa imetibu tatizo linaloonekana wazi linaikumba kwa sasa.

MJADALA

# Yanga, hiki si kipindi cha kuuza wachezaji




**Na Adam Fungamwango**

KUNA taarifa kuwa wachezaji wa Yanga, Ditram Nchimbi na Feisal Salum maarufu kama 'Fei Toto' wanatakiwa na klabu moja nchini Misri.

Wachezaji hao wanatakiwa kwenda kufanya majaribio na endapo watafanya vema, watapata mikataba ya kuitumikia klabu hiyo inayowahitaji.

Baada ya taarifa hii kukawa na habari za kujikanganya kwa Maofisa Habari wa Yanga, Antonio Nugaz na mwenzake Hassan Bumbuli.

Wakati Nugaz akisema tetesi hizo zipo na klabu itatoa taarifa rasmi, Bumbuli akasema kuwa huo ni uzushi.

Uzoefu unaonyesha kuwa kwenye klabu hizi kubwa za Simba na Yanga ukisikia kuna kitu basi ujue kipo, ila tu hakijatamkwa rasmi.

Wanaotoa tetesi ni baadhi ya watu hao hao waliomo ndani ya klabu. Ni klabu zisizo na siri.

Kwenye makala hii sina maana kuwa nataka kueleza jinsi ya kutunza siri za klabu, au kujichanganya kwa maofisa habari wa klabu ya Yanga, la hasha.

Ni jinsi klabu ya Yanga inavyotaka kuwauza wachezaji hao kama jambo hilo litakuwa ni sahihi.

Kwenda kufanya majaribio ni sahihi kwa muda huu kwa sababu klabu inakuwa tayari imeshajua uwezo na mchezaji ambaye inataka kumnunua.

Ninachopinga hapa ni kuwauza wachezaji hao wakati dirisha dogo la usajili nchini Tanzania limeshafungwa. Hili hapa ndiyo tatizo.

Kama ni kweli viongozi wa Yanga watawauza wachezaji hao kipindi hiki basi watakuwa wanafanya makosa.

Huwezi kuwa na uhakika na afya za wachezaji ambao ni tegemeo kwa sasa, kwani soka ni mchezo wa kutumia nguvu na majeruhi kuwa wakati wowote, hivyo hata kama muda huu hawana umuhimu, lakini baadaye wanaweza kuja kuisaidia timu inapokuwa na wachezaji majeruhi.

Klabu nyingi za soka duniani, achilia mbali Afrika, huwa haziuzi mchezaji kipindi ambacho si cha usajili, iwe cha dirisha kubwa au dogo.

Husubiri vipindi hivyo ili kama ikiuza, basi inunue mbadala wake, hata kama mchezaji huyo si wa kikosi cha kwanza au tegemeo kwenye timu.

Ni soka la Tanzania tu ndilo huwa na maajabu yake. Tangu zamani tulikuwa tunaona na kusikia baadhi ya wachezaji nchini, wakiondoka kwenda kucheza soka la kulipwa katikati ya ligi, tena dirisha likiwa limefungwa, lakini mchezaji huyo ni muhimu kwa timu.

Jambo hili lilikuwa likidhoofisha klabu na kutofanya vema kwenye mechi za ndani na hata kimataifa.

Hakuna anayekataa mchezaji wa Kitanzania kwenda kucheza soka la kulipwa kwa sababu wanatakiwa wapatikane kina Mbwana Samatta wengi, lakini ukweli unabaki pale pale kuwa klabu za Bongo hapa nchini nazo zinahitaji mafanikio ndani na nje ya nchi, hivyo zinahitaji kuwa na wachezaji bora na kwa wakati sahihi.

Kinachotakiwa ni kwamba kama Nchimbi na Fei Toto wanaondoka kwenda kufanya majaribio, basi waende, lakini warejee na kuendelea kuitumikia klabu yao hadi mwisho wa msimu, ndipo waondoke rasmi kwa sababu fedha za mauzo zitakazopatikana zitanunua wachezaji wengine wazuri zaidi. Kwa sasa hata kama Yanga ikiwauza na kupata pesa, hawawezi kumnunua au kumsajili mchezaji yoyote yule.

Ni kwamba hiki si kipindi cha usajili. Na hata kama klabu ikiingia mkataba na mchezaji hawezi kucheza hadi msimu ujao, hivyo kupunguza idadi ya wachezaji kwenye timu.

Ikumbukwe pia kwa sasa wachezaji wazuri wote wapo kwenye klabu zao na hata kama wakiondoka, basi wataondoka mwishoni mwa msimu.

Kuuzwa ghafla kwa Nchimbi kutashangaza wengi kwa sababu hana hata mwezi tangu kusajiliwa na klabu hiyo akitokea Azam FC, lakini akiicheza Polisi Tanzania kwa mkopo.

Hata kama viongozi na benchi la ufundi likiona kama lilifanya makosa kumsajili, au kujikuta ina idadi kubwa ya mastraika kuliko ilivyotarajia, bado si wakati muafaka wa kumwachia straika huyo kwa sasa badala yake isubiri tu Ligi Kuu Tanzania Bara na michuano ya Kombe la FA imalizike.

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
TANZANIA COMMUNICATIONS REGULATORY AUTHORITY

ISO 9001:2015 CERTIFIED

TCRA
CREATING A LEVEL PLAYING FIELD

## TAHADHARI KWA UMMA

**NDUGU WATANZANIA;**

**KAMA MNAVYOFAHAMU, LAINI ZA SIMU AMBAZO HAZIJASAJILIWA KWA KUTUMIA NAMBA YA KITAMBUSHO CHA TAIFA (NIDA) NA KUTHIBITISHWA KWA ALAMA ZA VIDOLE ZILIANZA KUZIMWA TAREHE 20 JANUARI, 2020 USIKU NA ZOEZI LINAENDELEA.**

**HAKIKI TENA USAJILI WA LAINI ZAKO KWA KUPIGA NAMBA *106# NA UCHUKUE HATUA STAHIKI SASA.**

1.0 KWA WALIOSITISHIWA HUDUMA ZA LAINI ZAO ZA SIMU KUANZIA TAREHE 20.01.2020 WANAWEZA PIA KUENDELEA NA UTARATIBU WA USAJILI KWA LENGO LA AMA KURUDISHA LAINI ZAO ZILIZOFUNGWA KAMA ZITAKUWA BADO ZIPO AU KUPATA LAINI MPYA. ZOEZI HILI NI ENDELEVU.

2.0 KWA WATUMIAJI/WAOMBAJI (WATANZANIA) WAPYA WA LAINI ZA SIMU WATAENDELEA KUSAJILIWA MUDA WOTE KWA KUTUMIA KITAMBULISHO CHA TAIFA NA KUHAKIKIWA KWA ALAMA ZA VIDOLE. **HUDUMA HIYO NI ENDELEVU PIA.**

3.0 MATUMIZI SAHIHI YA VITAMBULISHO WAKATI WA USAJILI WA LAINI ZA SIMU (ZINAZOTUMIKA AMA KWA AJILI YA MAWASILIANO YA SIMU ZA SAUTI AU VIFAA VYA MAWASILIANO MENGINE) UKO KATIKA MAKUNDI YAFUATAYO:-

3.1 Sisi wa-**Tanzania** kitambulisho chetu ni kile cha Taifa kitolewacho na NIDA kwa vigezo vyao;

3.2 Kwa wageni wanaokaa hapa nchini **chini ya miezi sita** wanasajili laini za simu kwa kutumia namba za Hati zao za kusafiria na kuhakiki kwa alama za vidole;

3.3 Kwa wageni wanaokaa zaidi miezi sita wanatumia vitambulisho *(Legal Resident ID)* ambavyo hupewa na NIDA (Hii ni kwa mujibu wa utaratibu wa Uhamiaji na NIDA);

3.4 Kwa wanadiplomasia wanatumia Hati zao za kusafiria pamoja na vitambulisho vyao vinavyotolewa na Wizara ya Mambo ya nje; na

3.5 Kwa wakimbizi wanatumia vitambulisho vyao ambavyo hupewa na NIDA (Hii ni kwa mujibu wa utaratibu wa Uhamiaji na NIDA),

4.0 KATIKA KUJIRIDHISHA KUWA WALIOSAJILI LAINI ZAO ZA SIMU WAMETUMIA VITAMBULISHO SAHIHI, TCRA KWA KUSHIRIKIANA NA WATOA HUDUMA ITAFANYA ZOEZI LA KUHAKIKI LAINI ZOTE ZITAKAZOKUWA ZIMESAJILIWA ILI KUWAONDOA WALE WALIOSAJILI LAINI ZAO AMA KWA KUTUMIA VITAMBULISHO VYA WATU WENGINE AU KWA KUTUMIA KITAMBULISHO TOFAUTI SAMBAMBA NA KUWACHUKULIA HATUA ZA KISHERIA.

5.0 IKUMBUKWE PIA KWAMBA KUSAJILI LAINI YA SIMU KWA KUTUMIA KITAMBULISHO CHA MTU MWINGINE NI KOSA SANJARI NA KUPEWA LAINI ILIYOSAJILIWA NA MTU MWINGINE.

6.0 ONYO NA TAHADHARI ZINAENDELEA KUTOLEWA KWA MAKUNDI YOTE YALIYOORODHESHWA KWENYE KIPENGELE CHA 3.0 HAPO JUU, KUTOTUMIA KITAMBULISHO KISICHOKUHUSU WAKATI UNASAJILI LAINI ZAKO ZA SIMU (ZINAZOTUMIKA AMA KWA AJILI YA MAWASILIANO YA SIMU ZA SAUTI AU VIFAA VYA MAWASILIANO MENGINE).

**Imetolewa na Mkurugenzi Mkuu**
**Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)**
**24 Januari, 2020**

215600102

# Bunge laiagiza Takukuru kukamata vigogo wizara

INATOKA UK. 2

2008 ufisadi huo umefanyika bila wahusika kuchukulia hatua wakiwamo waliokuwa watendaji wa Narco, Nicol na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, hivyo akaitaka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) kuwatafuta na kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria.

Kamati hiyo ilipongeza uamuzi wa serikali kuvunja mkataba wa mauzo ya mali za machinjio hayo baina ya serikali na Kampuni ya Nicol na kuyarejesha machinjio chini ya umiliki wa serikali na kuitaka kufanya haraka kurejesha masoko ya nyama katika nchi za Falme za Kiarabu yaliyopotea kutokana na usimamizi mbovu wa waendeshaji hao wa zamani.

Pia iliitaka serikali kuhakikisha fedha zote kiasi cha Sh. 9,712,127,660 (Sh. bilioni 9.7) zilizoibwa katika biashara ya machinjio, zinalipwa haraka pamoja mbia Nicol kulipa madeni yote inayodaiwa Kampuni ya Ubia TMCL kiasi cha Sh. bilioni 5.248.

Licha ya kupongeza uamuzi wa Narco, ambaye ni mbia katika Kampuni ya Ubia TMCL kujiondoa kwenye ubia huo, kamati hiyo ilisema bado kuna haja viongozi waliohusika na ufisadi huo kuwajibishwa kwa mujibu wa sheria. Mbunge wa Moshi Vijijini, Antony Komu, alisema uamuzi uliofanywa na Waziri Mpina katika kubaini kasoro hizo na kuchukua hatua, unapaswa kuendelezwa kwa serikali kutengeneza mfumo endelevu wa kubaini udhaifu na kuchukua hatua, akisikitika kuona ufisadi mkubwa kiasi hicho umefanyika pasi na wahusika kuchukuliwa hatua.

Komu alitaka hatua kama hizo ziwe endelevu ili kunusuru mali za nchi badala ya kumwachia kiongozi mmoja tu ambaye ni Waziri Mpina kusimamia mambo kama hayo.

Mpina aliihakikishia kamati hiyo kuwa serikali iko kwenye hatua ya mwisho za kufanya ukarabati mkubwa wa machinjio hayo na kurejesha upya masoko ya nyama nje ya nchi, ikiwamo nchi za Famle za Kiarabu na Comoro.

Pia, aliihakikishia kamati hiyo kuwa wote waliohusika na wizi na ubadhirifu, hawatapona kwa kuwa serikali inajua kwa mbali na fedha hizo zilizoibwa, hata mishahara ya wafanyakazi wa kampuni hiyo nayo ilifanyiwa ufisadi na kuleta usumbufu mkubwa kwa watumishi.

Waziri Mpina alisema kwa muda mrefu Wizara ya Mifugo na Uvuvi imekuwa ikichukua hatua mbalimbali katika kurekebisha kasoro za uendeshaji wa Machinjio ya Dodoma kama sharti muhimu katika mkataba wa mauzo ya mali kwenye Ibara ya 4.1.3.1 na kwa kuwa jitihada za kuinusuru Machinjio hiyo zimefanyika kwa muda mrefu bila ya mafanikio yoyote.

Alisema serikali ilijiridhisha kwamba mbia (Nicol) amekiuka vipengele muhimu vya mkataba katika ibara ya 7, 13, 6, 9 na 102; Pia Nicol imekuwa ikifanya biashara na mali za kampuni bila ya kuwekeza na bila ya kutoa gawio kwa serikali kwa kipindi chote cha miaka 11 iliyokabidhiwa kiwanda hicho.

Waziri Mpina amesema tangu machinjio hiyo ibinafsishwe, serikali imeendelea kupata hasara na mali nyingi za kampuni kama mitambo, majengo, magari na rasilimali nyingine zimechakaa na hakuna ukarabati wowote uliofanyika.

Pia nchi yetu imepoteza ajira, fedha za kigeni, biashara na masoko ya mazao ya mifugo baada ya kiwanda kufungiwa kuuza mazao ya mifugo katika nchi za Jumuiya ya Kiarabu (UAE).

Alisema kampuni 10 pia zilisimama kusafirisha na kufanya biashara ya nyama baada ya kiwanda kufungiwa ambapo kwa mwezi mauzo ya nyama nje ya nchi katika machinjio yalikuwa yamefikia tani 192 sawa na mbuzi 24,000. Pia kiwango cha uchinjaji wa ng'ombe kushuka kutoka wastani wa ng'ombe 120 hadi 50 kwa siku.

Alibainisha kuwa hasara na madeni ya Kiwanda cha TMCL yanaendelea kukua kila uchao huku mbia (Nicol) akishindwa kurekebisha kasoro zilizobainika katika vipindi tofauti hata baada ya kupewa notisi ya muda wa siku 30 na hata mbia mwenzake (Narco) kumpa notisi ya siku 180.

## Polisi wamtia mbaroni Lipumba kikao cha ndani

INATOKA UK. 2

yake kutokuwa hewani.

Akizungumza na Nipashe, Mkurugenzi wa Ulinzi na Usalama wa chama hicho ambaye ni Diwani wa Kata ya Misima Wilaya ya Handeni, Masoud Mhina, alisema Lipumba bado yuko mikononi mwa polisi akiendelea kuhojiwa.

"Kumekuwa na ukiukwaji mkubwa wa sheria, kwa kuwa shughuli za kisiasa zipo kwa mujibu wa sheria na vikao vya ndani huwa havihitaji kibali cha Polisi," alieleza Mhina.

Alisema kwa sasa chama hicho kipo katika mchakato wa kumwekea dhamana Prof. Lipumba, na kwamba baada ya dhamana hiyo Mwanasheria wa Lipumba atatoa mwongozo wa hatua zinazotakiwa zichukuliwe.

Aliongeza kuwa Jeshi la Polisi limekuwa likitumika vibaya na viongozi wa upinzani. "Amekuja hapa Dk. Bashiru (Katibu Mkuu CCM), amefanya mikutano ya hadhara, tena kwa ulinzi mkali na akachukua madiwani wetu wanane mbona polisi hawakuzuia, lakini sisi tunafanya vikao vya ndani na kufungua matawi wanatukamata," alilalamika Mhina.

Alisema demokrasia ya Tanzania inapitia katika wakati mgumu. "Januari 27, mwaka 2001 kulitokea ukandamizaji mkubwa wa wafuasi wetu huko Zanzibar na leo inajirudia tena, na nchi yetu kwa sasa inapitia katika wakati mgumu sana ila hatuna mengi ya kusema kwa sasa," aliongeza Mhina.

Prof. Lipumba yupo mkoani hapa kwa ziara ya siku saba katika wilaya saba. Katika wilaya zote alizofanya ziara alikumbana na misukosuko ya kukamatwa na Jeshi la Polisi.

Katika Wilaya ya Korogwe amri ya kumkamata ilitolewa na Mkuu wa Wilaya hiyo, Gwakisa Kasongwa.

TCCIA Investment Public Limited Company

TCCIA INVESTMENT PLC

P. O. Box 72678 Dar es Salaam, Tanzania Tel: 255 – 22 – 760173/2761725 Fax: 255 – 22 – 2119437

Email:info@tcciainvest.co.tz, Web site: http://www.tcciainvest.co.tz

WE ARE MOVING!

We are pleased to inform you that our offices currently at the Copycat Building Plot No. 39a, Victoria Area,Bagamoyo Road will be relocated tothe 24th Floor of the Millennium Tower phase II Building (wing B) at Kijitonyama Area, Bagamoyo Road effectively from 1st February, 2020.We are extending our sincere apologies for any inconveniences caused.

By,
The Chief Executive Officer,
TCCIA Investment plc.

# Waziri Kairuki awataka wawekezaji kujisajili TIC

**Na Mwandishi Wetu,** PWANI

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angellah Kairuki, amewataka wawekezaji nchini kujisali katika Kituo cha Uwekezaji nchini (TIC) ili kupata fursa mbalimbali za kiuwekezaji pamoja na msaada wa huduma za kikodi.

Akizungumza mwishoni mwa wiki katika majumuisho ya ziara yake katika Mkoa wa Pwani ambapo pamoja na mambo mengine, alifurahishwa na uwekezaji mkoani humo na kutoa rai kwa wawekezaji kujisajili TIC.

"Ilikuwa ziara yangu ya siku saba huku nikiangazia kero na changamoto mbalimbali za kiuwekezaji lakini zipo ambazo zinajitokeza kwa sababu wawekezaji wengi wameiweka kando TIC. Rai yangu kwa wawekezaji wandani na nje ya nchi kujisaliji katika kituo chetu cha uwekezaji ili waendelee kupata ufafanuzi wa kikodi na maeneo ya kiuwekezaji," alisema.

Waziri Kairuki alisema licha ya sheria za uwekezaji kutowalazimisha wawekezaji kujisajili TIC, lakini wanakosa mambo mengi mazuri ambayo yamekuwa yakiathiri utendaji wao katika maeneo ya uwekezaji.

"Wapo wawekezaji ambao wanatambua umuhimu wa kujisajili TIC na wameshafanya hivyo, changamoto ni kwa wale ambao hawajajisajili kwani licha ya kukosa huduma za kimsaada na zile za kikodi, wawekezaji wanakosa ufahamu mpana juu ya fursa za kiuwekezaji zilizopo hapa nchini," alisisitiza.

Aidha, katika hatua nyingine, Waziri Kairuki alisema kuwa serikali itaendelea kushughulikia changamoto za miundombinu ya barabara ambayo ni kiunganishi muhimu kati ya maeneo ya uwekezaji na masoko hali itakayosaidia kukuza biashara na kuchagiza kufanikisha azma ya serikali ya uchumi wa kati na viwanda ifikapo 2025.

"Kama serikali tutaendelea kurahisisha mazingira ya kiuwekezaji na zaidi kwa sasa tunajikita katika kuyaunganisha maeneo ya uwekezaji na soko ili kufikia azma ya uchumi wa kati na viwanda kwa haraka zaidi," alieleza.

Waziri Kairuki alisema ili kupunguza changamoto za uwekezaji katika mikoa na wilaya ni vyema yakatengwa maeneo maalum ambayo yatatumika na wawekezaji kwa ajili ya viwanda, kilimo na sekta zingine za kiuchumi. "Kuna changamoto ya upatikanji wa maeneo ya kuwekeza, hali inayorudisha nyuma maendeleo katika sekta ya uwekezaji, hivyo natoa wito kwa wahusika kutenga maeneo maalum ya uwekezaji katika ngazi ya mkoa, wilaya na hata vijiji ili kuchohcea uwekezaji," alieleza.

Alisema serikali imejielekeza zaidi kuboresha mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji hapa nchini ili kufikia azma ya serikali ya awamu ya tano ya kujenga uchumi wa kati na viwanda kama ilivyokusudiwa.

"Kwa mwekezaji wa kigeni ambaye hisa zake ni zaidi ya asilimia 51, TIC ina haki ya kutoa hati isiyo ya asili kwa mwekezaji ili aweze kumiliki eneo hilo kwa miaka 98 ili kufanya shughuli za uwekezaji," alifafanua.

Akiwa katika ziara hiyo, Kairuki mbali ya kutembelea viwanda na maeneo mbalimbali ya uwekezaji, aliwakumbusha na kusisitiza umuhimu wa kulipa kodi staki za serikali kama sheria inavyoelekeza.




Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, akizungumza mbele ya wanafunzi wa Shule ya Sekondari Msalato jijini Dodoma, baada ya kupokea na kukabidhi taulo za kike kupitia kampeni ya 'Namthamini' inayoendeshwa na East Africa Television na East Africa Radio kwa mwaka wa nne mfululizo. **PICHA: EATV**

# Kilimo kutumika kukabili changamoto ajira kwa vijana

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

SERIKALI imeamua kutumia Sekta ya kilimo kutatua changamoto ya ukosefu wa ajira kwa vijana kwani kwa muda mrefu kilimo kimekuwa kikichukuliwa kama kazi ya ziada baada ya kukosa ajira maeneo mengine.

Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi,Vijana na Ajira, Anthony Mavunde, alisema hayo wakati akikabidhi hati za kusafiria vijana 12 wanachama wa ushirika wa wahitimu wajasiriamali wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo(SUA) SUGECO, waliopata ufadhili wa kwenda nchini Marekani kwa mafunzo zaidi ya kilimo kivitendo. Waziri Mavunde alisema wizara yake imeendelea kuwa karibu na SUA ili kushirikiana kutatua changamoto ya ukosefu wa ajira kwa vijana kupitia sekta ya kilimo ambapo mpango wa serikali kwa sasa ni kuhakikisha asilimia 40 ya watu milioni 24.3 wanaajiriwa kwenye sekta ya kilimo.

Aidha, alisema malengo ya serikali ni kuhakikisha ifikapo mwaka 2025 asilimia 40 ya nguvu kazi ya nchi inaajiriwa kwenye sekta ya viwanda ambayo ni mnyororo wa thamani na ambayo imekuwa ikianzia kwenye mazao ya kilimo, ufugaji, na misitu na huko mahitaji ya malighafi zitokanazo na mazao ya kilimo zitakuwa ni kubwa.

Mavunde alibainisha Mkoa wa Morogoro ni kati ya mikoa inayofanya vyema katika shughuli za kilimo kwa kutenga maeneo ya shughuli hizo ambapo baadhi ya vijana waliohitimu SUA (Agri Ajira) na kupatiwa shamba na kulima zao la mpunga tayari wamevuna na kupata fedha zaidi ya milioni 100, hivyo wizara hiyo iko kwenye mazungumzo na uongozi wa mkoa ili waongezewe maeneo.

Aliwaasa vijana wanaokwenda Marekani kwa mafunzo kuwawakilisha vyema vijana wenzao na kuhakikisha wanaileta sifa njema Tanzania na tija katika kilimo cha kisasa badala ya kwenda kufanya vinginevyo.

Alizishauri taasisi za kifedha kuacha kuweka masharti magumu kwa vijana katika kuwapatia mikopo, huku akipongeza benki ya Equity kuwawezesha vijana hao 12 mkopo wa nauli ya kufika Marekani na kuwataka kuweka utaratibu wa kuwawezesha pindi watakaporejea ili wafanyie kazi elimu waliyopata kivitendo kwa kulima au kufuga kisasa.

## Idara lawamani mapato kiduchu

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MADIWANI wa Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wamezilalamikia baadhi ya idara kwa kushindwa kukusanya mapato ya ndani ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20 kuanzia Julai hadi Desemba.

Madiwani waliyasema hayo kwenye kikao cha baraza cha kujadili mapitio ya bajeti ya utekelezaji wa mwaka wa fedha 2019/2020 kwa kipindi hicho.

Diwani wa Nyankende, Doa Limbu, alisema kila mwaka wa fedha Idara ya Kilimo, Maliasili na Mifugo ndio zimekuwa zikifanya vizuri kwenye ukusanyaji wa mapato kwa zaidi ya asilimia 52 kila mwaka wa fedha.

Alisema Halmashauri ya Ushetu kwa mwaka wa fedha 2019/20 ilipanga kukusanya kiasi cha Sh. bilioni 2.3 kupitia vyanzo vyake vya mapato ya ndani, lakini mpaka sasa imekusanya asilimia 40 ya mapato yake.

Aidha, alisema kila idara inatakiwa kukusanya mapato kwa asilimia 100 ukiachilia Idara ya Kilimo, Maliasili na Mifugo, idara nyingine bado ziko chini katika ukusanyaji wa mapato, huku ikiwa imebaki miezi michache kumaliza mwaka wa fedha.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Halmashauri, Juma Kimisha, alisema kama baadhi ya idara zinakusanya mapato chini ya asilimia 7.6 haipatii uhai halmashauari na inaweza ikasababisha baadhi ya miradi kutokamilika kwa wakati.

"Mkurugenzi, kama idara zako zisipofanya vema kwenye ukusanyaji wa mapato tulipofikia sasa tunaelekea kwenye wakati mgumu...tumeshatoa miongozo kupitia vikao vyetu kwamba hatutakiwa kukusanya mapato chini ya asilimia 50," alisema Kimisha.

Hata hivyo Kimisha, alimtaka mkurugenzi kuhakikisha kila idara iliyopangiwa asilimia ya makusanyo ahakikishe inafikia lengo la makusanyo nakuongeza asilimia 40 ya miradi ya maendeleo inategemea fedha za mapato ya ndani.

Akijibu hoja hiyo Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Wandere Lwakatare alisema kuwa, atahakikisha kila idara inakusanya mapato ipasavyo na atahakikisha wanaongeza kasi ya makusanyo na kufikia asilimia 52 ya makusanyo kabla ya mwaka wa fedha kuisha.

## Wanafunzi Suza wataka elimu afya

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

WANAFUNZI wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (Suza) kisiwani Pemba wameiomba Wizara ya Afya kutoa elimu ya afya kwa makundi yaliyojikusanya, ili kuepukana na maambukizi ya maradhi mbalimbali.

Wakizungumza baada ya kufanya usafi katika Hospitali ya Wete, walisema elimu ya afya ni muhimu katika makundi yaliyojikusanya ikiwamo vyuoni.

Walieleza kuwa sehemu zenye mikusanyiko ya watu kunaweza kujitokeza magonjwa mbalimbali, hivyo ipo haja kwa Wizara ya Afya kuchukua jitihada za makusudi kuhakikisha wanatoa elimu, ili kuzuia majanga yanayoweza kujitokeza.

"Ili tuimarishe masuala ya afya na kuelimisha wenzetu, ni vyema Wizara ya Afya kupita kwenye mikusanyiko ya watu ikiwamo vyuoni kwani usafi wa mazingira ndio afya na ndio utakaopunguza maambukizi," alisema Mkuu wa Serikali ya wanafunzi wa Chuo hicho, Mohamed Abdi.

Naibu Waziri wa Elimu wa Serikali ya Wanafunzi SUZA, Mohamed Ali Mohamed, aliwataka wanafunzi wenzake kuwa na moyo wa kujitolea, jambo ambalo litawajengea heshima kubwa maishani mwao.

"Tumejitolea kuja kufanya usafi katika Hospitali ya Wete... hii tunajijengea mazingira mazuri ya hapo baadaye ili tuwe na moyo wa kujitolea zaidi na kujenga Taifa lililo bora," alisema.

Naye Mlezi wa Klabu ya Mazingira ya SUZA, Idrisa Khamis Sabur, alisema lengo la kufanya usafi hospitalini hapo ni kuwaandaa vijana hao kuwa viongozi bora wa baadaye watakaokuwa wabunifu na wenye moyo wa kujitolea.

Alibainisha kuwa watakuwa vijana imara wenye kutumikia nchi yao na kuwa wabunifu katika shughuli mbalimbali ambazo zitaleta maendeleo endelevu.

"Tunauomba uongozi wa Hospitali ya Wete uendelee kutupa ushirikiano wakati tunapotaka kufanya usafi ili waendelee kujitokeza na watu wengine wenye nia kama yao," alisema.

Pamoja na kufanya usafi, pia klabu hiyo ilikabidhi vifaa vya kufanyia usafi hospitalini hapo pamoja na kutoa msaada wa sabuni za kuogea kwa wagonjwa.

# Maduka ya nyama yalalamikia tozo kubwa ushuru halmashauri

**Na Stevie chindiye,** TUNDURU

WAFANYABIASHARA wa maduka ya kuuza nyama ya ng'ombe wilayani Tunduru mkoani Ruvuma, wamelalamikia kuwapo tozo kubwa za ushuru wa halmashauri.

Hayo yalibainishwa na wafanyabiashara hao, ambao hata hivyo, hawakutaka ku tajwa majina yao gazetini kwamba baadhi ya maofisa wamekuwa wakiwalazimisha kulipia hadi wastani wa ng'ombe watano hewa, lakini inapotokea mfanyabiashara kanunua ng'ombe nje ya neo la mnada pia hutozwa fedha nyingine ambazo haziandikiwi stakabadhi.

Kwa mujibu wa taarifa hizo, kila ng'ombe analipiwa ushuru wa shilingi 20,000 kila anapokwenda kuchinjwa katika machinjio hayo.

Walisema katika ushuru huo ambao maofisa ambao husimamia zoezi hilo wame uweka katika mafungu mawili ambapo ng'ombe anapokwenda kuchinjwa analipiwa kiasi cha shilingi 12,500. Walisema kinachowashangaza kupitia tozo hiyo mbali na wao kulipa kiasi hicho lakini fedha halali wanayoandikiwa katika stakabadhi za kielektroniki ni shilingi 2,500 tu, hali inayoonyesha kuwa kiasi cha shilingi 10,000 kwa kila ng'ombe huingia mifukoni mwa wasimamizi hao.

Wafanyabiashara hao walibainisha kuwa fedha nyingine wanazotozwa na maofisa hao ni shilingi 7,500 ambazo hutozwa kama ghalama za mnada hata kama ng'ombe huyo hakununuliwa mnadani.

Walisema gharama hizo ni kubwa mno ikilinganishwa na maeneo mengine ambapo ng'ombe mmoja hulipiwa shilingi 5,000 kama ushuru wa mnada na kiasi cha shilingi 4,000 hutozwa kama ushuru wa machinjio na kufanya kila ng'ombe kulipiwa shilingi 9,000. Kero nyingine iliyobainishwa na wafanya biashara hao ni kuwapo kwa tabia ya wataalamu wa kupima nyama kukata zaidi ya kilo tatu kutoka kila ng'ombe aliyechinjwa kwa madai kuwa wanaenda kuonja.

Uchunguzi unaonyesha kuwa maofisa hao hupeleka nyama hizo ambazo ni maini, nundu na baadhi ya steki huenda kuuza kwa wafanyabiashara wanaopika chakula na kujipatia fedha kwa lengo la kujinufaisha kwa kujipaatia kipato cha ziada.

Takwimu zinaonyesha kuwa takribani ng'ombe 20 hadi 30 huchinjwa kwa siku.

Akizungumzia malalamiko hayo, Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru, Morton Msowoya, alisema hajapata taarifa za matukio hayo, lakini baadaa ya kuwauliza vijana wake ili kumjibu mwandishi wa habari hizi walidai kuwa madai hayo ni uongo.

Alisema katika majibu yao nyama wanazodaiwa kukata na kwenda kuuza wao wamekuwa wakilazilishwa kuchukua ili wakale na familia zao na wasipochukua wachinjaji hao huwa wanajisikia vibaya kuwa labda maofisa hao wamekasilika. Kuhusu malipo ya ushuru unaotozwa, alisema siyo shilingi 20,000 bali ni shilingi 9,000 tu, na akuwataka wafanyabiashara wanaolalamikia vitendo hivyo kukataa kutotozwa zaidi ya kiasi hicho cha fedha.

Aidha, Msowoya alisema anaendelea kufuatilia kutoka kwa wachinjaji ili na ikibainika atamjulisha mkurugenzi kwa ajili ya hatua za kinidhamu dhidi ya watendaji hao.




Ofisa Mkuu wa wateja binafsi, wafanyabiashara wadogo na wa kati wa Benki ya NMB, Filbert Mponzi, akizungumza na makandarasi kuhusu fursa za kifedha zinazotolewa na benki hiyo kuwawezesha makandarasi nchini kwenye mkutano wa Bodi ya Makandarasi (CRB) jijini Arusha juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Petrobena yahakikishia wakulima mbolea

**Na Mwandishi Wetu,**

KAMPUNI ya Petrobena East Africa Ltd imesema itaendelea kusambaza mbolea za YARA nchini kwa kuzingatia bei elekezi ya serikali kwa wakulima ili kuchagiza mageuzi kwenye sekta ya kilimo na kufanikisha azma ya serikali ya awamu ya tano ua kujenga uchumi wa kati na viwanda ifikapo 2025.

Akizungumza na ujumbe kutoka kampuni ya Yara Africa uliotembelea ofisini kwake mwishoni mwa wiki, Mkurugenzi Mtendaji wa Petrobena East Africa, Peter Kumalilwa, aliuambia ujumbe huo kuwa kampuni yake itaendelea kuwasambazia wakulima pembejeo kwa bei elekezi ili kuinua uzalishaji mazao hapa nchini.

"Katika ziara yao tumejadiliana mambo mbalimbali na jinsi tulivyojipanga kuhakikisha mbolea inamfikia mkulima kwa wakati na kwa bei elekezi ya serikali hali itakayo chochea uzalishaji wa mazao na kukuza kipato chake," alisema Kumalilwa.

Kumalilwa alisema kampuni yake itaendelea kuunga mkono jitihada za serikali ya awamu ya tano kufanikisha azma yake ya ujenzi wa uchumi wa kati na viwanda kwa kufanya mageuzi ya kilimo hapa nchini.

"Tutaendelea kuunga mkono juhudi za serikali ya Rais John Magufuli kwa kufanya mabadiliko katika sekta ya kilimo ambayo inawagusa Watanzania zaidi ya asilimia 70 na furaha yetu ni kuona tunakuwa sehemu ya mabadiliko yanayofanywa na serikali," alisema.

Kumalilwa alisema kuwa katika mazungumzo na ujumbe wa Yara Africa waliangazia pia uwezekano wa kampuni hiyo ya Yara kujenga kiwanda kitakachozalisha mbolea hapa nchini ili kuleta nafuu zaidi kwa wakulima.

Kumalilwa hakutoa ufafanuzi zaidi wa mpango huo wa ujenzi wa kiwanda cha mbolea nchini. Aliuthibitishia ujumbe huo kuwa kampuni yake itaendelea kuwafikia wakulima wengi zaidi ili waweze kutumia mbolea za Yara.

Kumalilwa alisema kuwa kwa sasa wanajivunia ongezeko la wakulima ambao wamekuwa wakitumia mbolea zao huku wengi wakisifu ufanisi wa mbolea hizo kwa kuongeza uzalishaji na ubora wa mazao shambani. "Tunajivunia ongezeko la wakulima wanaotumia mbolea za Yara kwani mpaka sasa zaidi ya wakulima laki moja wanatumia mbolea za Yara.

Ongezeko la watu hao kwa muda mfupi ni ishara ya ubora wa mbolea hizi ambazo zimegawanyika katika makundi kuanzia kupandia mpaka kukuzia," alieleza Kumalilwa.

# Askofu afichua siri ndoa kuvunjika

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

ASKOFU Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki la Arusha, Isack Amani, amesema ndoa nyingi zinavunjika kwa sababu ya kufanya uchumba wa muda mfupi tofauti na ule wa utawa, uchumba wake wa miaka sita.

Kadhalika, amewataka wanandoa kujenga misingi imara kwenye familia zao ili taifa lipate watoto wenye maadili na watawa.

Aliyasema hayo juzi katika Kanisa la Mtakatifu Yakobo Mtume lililopo Moshono wakati wa misa takatifu ya kuweka nadhiri ya kwanza kwa masista watatu wa Jimbo Kuu la Moshi, Iringa na Tanga.

Alisema ndoa nyingi zinavunjika kwa sababu ya kujengwa kwenye misingi isiyo imara na lawama zinapelekwa kwa walimu wa dini juu ya malezi ya watoto wao.

"Mimi leo nawapongeza wazazi hawa waliosimama imara na kutoa matunda ya masista hawa Maria Marcus wa Jimbo Kuu la Iringa, Monica Mdoe wa Jimbo Kuu la Tanga na Dafrosa Shayo kutoka Jimbo Kuu la Moshi, bila familia hizi kujenga msingi imara, leo tusingepata watawa hawa walioweka nadhiri zao za kwanza za kuwa masista," alisema Askofu Amani.

Askofu Amani alisema watoto wakipata malezi mazuri ni sawa na msingi imara ambao hata ikija mvua ya upepo hauwezi kubomoka.

"Hawa wameweka nadhiri zao kwa kufanya uchumba na Yesu kwa miaka sita, sasa hapa wamepita kila aina ya vikwazo, lakini wamepambana hadi kufikia siku hii ya leo, lakini sisi wengine tunakimbilia kufunga ndoa hata hatujafahamiana tabia, uchumba wa muda mfupi ni chanzo cha kuvunjika ndoa," alisema Askofu Amani.

Askofu Amani aliwaasa masista hao kusimama imara katika kipindi hicho cha utawa na kujiepusha kuingia katika mazingira yatakayo wakatisha safari yao ya utawa.

Aidha, aliwaonya baadhi ya wazazi wanaowabebesha mizigo watawa kwa kutaka wahudumie familia au kusomesha ndugu zao hali inayosababisha watawa kuchanganyikiwa kutokana na mzigo wa majukumu.

Askofu Amani alilipongeza Shirika la Missionari wa Ekaristi na Uinjilishaji Mpya, ambalo wamezalisha masista hao watatu kwa kuanzisha miradi ya maji na Shule ya Ufundi katika Kata ya Moshono.

Mwanzilishi wa Shirika la Missionari wa Ekaristi na Uinjilishaji Mpya, Gisela Upendo Msuya, aliwapongeza masista hao kwa kuweka nadhiri zao za kwanza na kuwaombea waishi katika ahadi hiyo.

Alisema mbali na kuzalisha watawa katika shirika lao, pia wanajihusha na shughuli za kijamii ikiwamo kuwasaidia wananchi kupata maji kwa kuwapatia mradi uliogharimu Sh. milioni 250 uliopo katika Kata ya Moshono.

Pia wamejenga shule ya ufundi ambayo ipo katika hatua za mwisho kukamilika ambayo itachukua vijana 200 katika fani za uselemala, upishi na kompyuta.

Masista hao walishukuru wazazi, watawa mbalimbali kwa kuwasaidia kufikia siku hiyo muhimu maishani mwao.



Msajili wa Bodi ya Makandarasi (CRB), Rhoben Nkori, akimkabidhi cheti mmoja wa wahitimu wa mafunzo ya siku tatu yaliyoandaliwa na bodi hiyo, jijini Arusha. Kulia ni Msajili Msaidizi Utafiti na Maendeleo, David Jere na kushoto ni Mratibu wa Mafunzo wa bodi hiyo, Neema Fuime. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Makandarasi sasa watakiwa kuleta mabadiliko chanya

**Na Allan Isack**, ARUSHA

MSAJILI wa Bodi ya Makandarasi nchini, Rhoben Nkori, amewataka makandarasi kutumia mafunzo yanayotolewa na bodi hiyo kuleta mabadiliko chanya katika kampuni zao za ujenzi.

Aliyasema hayo jana jijini Arusha, wakati akifunga mafunzo ya siku tatu ya kuwajengea uwezo makandarasi na wamiliki wa kampuni za ujenzi nchini.

Alisema endapo makandarasi watatumia vizuri mafunzo hayo, kampuni zao zitakuwa za kishindani katika kutafuta kandarasi za ujenzi wa miradi mikubwa na ile midogo.

"Mafunzo haya mkayazingatie na kuyafanya kazi kwa vitendo katika utekelezaji wa miradi kwenye makazi yenu ya ujenzi," alisema Nkori.

Aidha, aliwataka makandarasi hao kuwasimamia vizuri wafanyakazi wao na kila mmojawapo awajibike kulingana na nafasi yake.

Pia, aliwataka makandarasi hao kutokukata tamaa kutokana na vikwazo na matatizo wanayokumbana nayo kwa kuwa vikwazo na matatizo ndio njia ya kufikia malengo na mafanikio.

"Makandarasi msiogope vikwazo na matatizo mnayokutana nayo kwa kuwa njia hiyo ndiyo ya kufikia mafanikio na malengo," alisema Nkori na kuongeza: "Tusikate tamaa kwa sababu njia ya kufikia malengo na mafanikio ni nyeupe na inaonekana tusiogope vikwazo chamsingi tuwe wavumilivi na kufanya kazi bila ya kukata tamaa."

Alisema endapo makandarasi hao, watatekeleza miradi kwa ubora, serikali itawapa tenda za miradi na kuwataka kuwa na uaminifu, washirikiane wakati wanapopewa kandarasi za ujenzi kama njia mojawapo ya kufikia maendeleo waliyojiwekea.

Akizungumza kwa niaba ya makandarasi wengine, Marry Makenda alisema tatizo kubwa linalowakabili makandarasi nchini ni kuwapo kwa utitiri wa kodi kwenye sekta ya ujenzi.

Waliiomba serikali kupunguza malimbikizo ya kodi na tozo mbalimbali pamoja na kuwalipa kwa wakati fedha zao, kabla na baada ya kukamilisha ujenzi wa miradi.

# Mkurugenzi Jiji kujenga barabara kisasa shuleni

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Jiji la Arusha, Dk. Maulid Madeni, ameahidi kujenga barabara za kisasa katika Shule ya Sekondari Suye jijini hapa, ili wanafunzi na watumishi waondokane na kadhia ya matope wakati wa mavua.

Alitoa ahadi hiyo mwishoni mwa wiki wakati akiwa katika ziara ya Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Gabriel Daqarro, akikagua miundombinu ya shule hiyo, Sekondari ya Maoivaro, Kituo cha Afya.

Dk. Madeni alisema kutokana na hali mbaya ya miundombinu katika shule hiyo ikiwamo madarasa, ofisi za walimu na vyoo kujaa matope, atawajengea miundombinu ya kisasa ikiwamo barabara zinazopitika wakati wote.

"Sasa shule hii tumeijenga kwa gharama kubwa, kwa hiyo sitaki kuona wajukuu wa Rais Magufuli mkipata shida na matope, niombeeni mwaka huu wa mwisho kuhangaika, mwakani nitajenga njia za juu kwa juu nzuri za kuunganisha miundombinu yote ya eneo hili, ili mpite sehemu nzuri zisizo na matope," alisema Dk. Madeni.

Aidha, aliwataka wanafunzi hao wakati serikali inapambana na kurekebisha miundombinu ya shule zao zikae vizuri, wajitahidi kusoma kwa bidii ili wafikie ndoto zao.

Naye DC Daqarro, aliwataka wanafunzi hao kusoma kwa bidii zaidi ili wafikie malengo waliyojiwekea.

"Sisi serikali tunahakikisha tunaboresha mazingira ya shule zenu ili msipate kero ya aina yoyote, madarasa mnayo ya kutosha, madawati na vyoo vizuri vya kisasa, sasa nyie kazi yenu kutupa raha sisi viongozi wenu na wazazi kwa kufaulu vizuri," alisema Daqarro.

Baada ya kutoa ahadi hizo mmoja wa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Suye, Daniel Steven, aliwaongoza wanafunzi wenzake kuwaombea viongozi hao, ili watimize mipango waliyojiwekea juu yao.

"Lakini sisi kama wanafunzi tunaona jitihada mnazofanya chini ya Rais John Magufuli za kutupa elimu bure, tunaahidi tutasoma kwa bidii na hatutawaangusha, lakini na nyie tunawaombea shetani asiinuke juu yenu muwe na afya njema, ili mtimize ndoto mlizojiwekea juu yetu," alisema Steven.

# DC aonya wenyeviti kuvuruga taaluma

**Na Godfrey Mushi,** HAI

MKUU wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, amezinyooshea kidole serikali za vijiji na kamati za shule, akizionya kuacha mara moja kuingilia majukumu ya kitaaluma katika shule za msingi wilayani humo.

Badala yake, amewataka wawape walimu wa shule hizo nafasi ya kuwaandaa wanafunzi kufikia ndoto zao za kitaaluma na kuvuka malengo ya ofisi yake aliyoagiza kila shule kuongeza kiwango cha ufaulu katika mitihani ya kitaifa.

Ole Sabaya alikuwa akizungumza na wakuu wa shule zote za msingi wilayani humo ambapo kilihudhuriwa pia na wenyeviti wa kamati za shule na wenyeviti wa serikali za vijiji.

"Nyie wenyeviti wa serikali za vijiji kuna baadhi yenu kwa kushirikiana na kamati za shule mnawakwaza walimu kwa kuingilia masuala ya kitaaluma. Nyie wakati mwingine ndio kikwazo na mnasababisha hata maendeleo ya shule kitaaluma kushuka, acheni hayo mambo kuanzia sasa. Mimi nawaangalia lakini kuna siku nitaamka na mtu jumla jumla," alisema.

Pamoja na mambo mengine, Ole Sabaya alitoa maelekezo kwa viongozi hao kuhakikisha kwamba kila shule wanafunzi wanapata chakula shuleni.

Alisema uboreshaji wa elimu unaofanyika hivi sasa ni pamoja na utoaji wa chakula usio suasua katika shule zote zilizopo kwenye kata 17 za wilaya hiyo.

"Utoaji wa chakula ni msingi thabiti wa kumkuza mtoto kiakili, kimwili, kimaadili na hatimaye kupata wahitimu wenye elimu bora kwa Tanzania ya viwanda. Nimeambiwa kwamba kuna shule bado hazitoi huduma ya chakula shuleni, naagiza chakula kila shule kiwepo na ninakuja huko kukagua," alisisitiza Mkuu huyo wa Wilaya.

Alisema ni sharti wanafunzi wote wapatiwe chakula shuleni, huku akiwasisitiza wazazi kuhakikisha wanawajibika kuchangia michango ya chakula na kwamba mzazi atakayeshindwa kulipa hivyo atachukuliwa hatua za kisheria.

"Nyie watu, Rais Magufuli anatoa shilingi bilioni 23.86 kila mwaka kwa ajili ya kuhudumia elimu bure ambayo inatumika kulipa ada za wanafunzi, kuhudumia miundombinu, kuhudumia shughuli za utawala wa shule kwa kila mwanafunzi aliyeandikishwa kwenye shule husika.

# Uchumi unaojali kuwainua 500 Siha, Moshi Vijijini

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

SHIRIKA lisilo la kiserikali la Tusonge linalofanya kazi na makundi ya pembezoni katika mkoa wa Kilimanjaro, limezindua rasmi awamu ya nne ya mradi wa 'uchumi unaojali' ambao utachochea wanufaika zaidi ya watu 500 katika Wilaya za Siha na Moshi.

Watu hao watapata faida kwenye sekta mbili za kilimo na ufugaji na sekta ya uzalishaji wa sabuni.

Mkurugenzi Mtendaji wa Tusonge, Agnatha Rutazaa, akizungumza mwishoni mwa wiki na wadau ambao ni wataalamu wa afya, mazingira, maofisa maendeleo ya jamii, kilimo, Benki ya Uchumi (UCB), wanufaika wa mradi huo na mtaalamu wa Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (Sido), alisema wanalenga kuisaidia jamii kupata faida, kuangalia mazingira na wafanye uchumi ambao utakuwa hauathiri mazingira ambayo tunayaishi kama matumizi ya kemikali na kadhalika.

"Kwa maana hiyo basi katika uchumi unaojali tutakuwa tunaangalia mtu afanye biashara au mradi wa kumwongezea kipato, lakini kwanza utakuwa unajali afya yake. Katika tafsiri ya Tusonge ni kwamba mzalishaji ambaye ni mjasiriamali wetu ahakikishe kwamba bidhaa anazozizalisha na anavyozitunza na anavyoziua, zitakuwa ni bidhaa ambazo ziko salama katika afya ya mlaji na hata katika afya yake yeye mwenyewe kama mzalishaji.

Aliongeza: "Wengi wamekuwa wanafanya biashara kwa mfano hizi za kilimo, lakini ukiangalia kwa asilimia kubwa, mbinu zinazotumika katika kilimo kwa asilimia kubwa utakuta kwamba wanalima kwa kutumia mbolea za chumvi chumvi, na hii inakuwa sana sana kuongeza athari za afya za muda mrefu."

Alitolea mfano kwamba, mtu anaweza akala mboga zenye mbolea ya chumvi chumvi au amepiga dawa kwa mfano nyanya, karoti, vitunguu na hoho, ambapo mimea hiyo hubakia na sumu kali ambazo ni hatari kwa maisha na hasa mwili wa binadamu.

Kabla ya uzinduzi huo, msimamizi wa mradi wa uchumi unaojali, Aikael Manase alieleza kuwa: "Tunatarajia kufikia watu 500 katika Wilaya ya Siha na Moshi na katika hao watu tunalenga katika sekta kuu mbili ambazo ni sekta ya kilimo na ufugaji na sekta ya uzalishaji wa sabuni. Huko tutakuwa na jumla ya wanawake 300, wanaume 109, vijana 76 pamoja na watu wenye ulemavu wapatao 15."

Aidha, alieleza: "Leo tuko hapa na tumeweza kukutanisha wadau mbalimbali kuanzia ngazi ya mkoa, wilaya, kata, vijiji pamoja na wanufaika wa moja kwa moja wa mradi pamoja na wadau mbalimbali kama watu wa benki ya uchumi na Sido, kwa ajili ya kuwashirikisha shughuli tunazotarajia kufanya katika kipindi cha miezi mitatu nikimaanisha 2020/2022."

Msimamizi huyo wa mradi wa uchumi unaojali amesisitiza kuwa lengo la kuwaita wadau hao na kuwaweka pamoja ni kwa sababu wako katika hatua za awali za kupanga nini wanakwenda kukifanya.

"Tunataka watambue masuala ya afya zao, wafanye uchumi ule ambao unaweza kuwasaidia wao kutunza afya zao kama kupumzika, kupata faida, kuangalia mazingira na wafanye uchumi ambao utakuwa hauathiri mazingira ambayo tunayaishi kama matumizi ya kemikali na kadhalika. Tunatarajia kuona watu hao wa mkoa wa Kilimanjaro angalau waweze kuboresha maisha yao lakini waweze kufurahia maisha yao," alisisitiza Aikael.



Kikosi kazi cha wadhibiti ubora, maofisa elimu, walimu wakuu na waratibu wa elimu katika Halmashauri ya Wilaya ya Siha wakijadili falsafa kuhusu ujenzi wa uwelewa wa pamoja juu ya utekelezaji wa elimu jumuishi juzi. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Udhalilishaji kingono kwa wanawake waitishia Same

**Na Godfrey Mushi,** SAME

WANAWAKE mashuhuri 20 waanounda jukwaa la vuguvugu la ukombozi wa mwanamke kimapinduzi (Tapo) katika Wilaya ya Same, wamewasilisha rasmi malalamiko yao kwa serikali, wakitaka ichukue hatua za haraka kudhibiti matukio ya udhalilishaji wa kingono kwa wanawake.

Matukui hayo yanaendelea karibu na kilabu kimoja cha pombe za kienyeji kilichoko Kitongoji cha Ujamaa A, Kata ya Same.

Taarifa kuhusu udhalilishaji huo ziliwasilishwa mwishoni mwa wiki kwa Ofisa Maendeleo ya Jamii ya Wilaya hiyo Charles Anatoly na wanawake hao.

Jukwaa hilo liliwasilisha malalamiko yao kwa Anatoly, kabla ya kufungwa mafunzo ya siku nne ya mradi wa ujenzi wa nguvu ya pamoja ya kutetea wanawake na watoto kupambana na ukatili wa kijinsia.

Mradi unaotekelezwa na Shirika la Kwieco, kwa ufadhili wa Women Fund Tanzania (WFT).

Udhalilishaji huo wa kingono, unadaiwa kufanywa bila kificho na baadhi ya wanaume na wanawake wanaokwenda kunywa pombe za kienyeji, huku eneo hilo likiwa na idadi kubwa ya watoto wanaopita wakati wa kwenda na kutoka shuleni.

"Kunapofanyika udhalilishaji huo wa kingono hadharani ni karibu na kilabu kimoja cha pombe za kienyeji na kwa namna hali ilivyo, tunaomba nyie wenye dhamana na hata Mkuu wa Wilaya yetu kutafuta njia ya kudhibiti uchafu huo, kwa sababu pale kuna watoto wanapita wakitoka na kwenda shule. Je, wanajifunza nini?" Alihoji mmoja wa wanaharakati aliyeomba asitajwe jina lake.

Mratibu wa mradi wa ujenzi wa nguvu ya pamoja ya kutetea wanawake na watoto kupambana na ukatili wa kijinsia, Veronika Ullomi, akizungumza kabla ya mafunzo hayo alisema malengo mahususi ya Tapo ni kukuza uelewa na utambuzi wa kada hiyo.

"Nia yetu ni kujenga uelewa wa pamoja wa dhana muhimu za kijinsia zikihusishwa na maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa lakini pia kuhamasisha jamii na kukuza uelewa wao juu ya dhana na itikadi ya ufeministi kama dhana ya kufikia usawa wa kijinsia," alieleza Ullomi.

Akijibu madai hayo ya wanaharakati, Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya hiyo, Anatoly, alisema: "Kuna suala la hicho kilabu mmesema kuna ulawiti pale na ubakaji.

Alipotafutwa Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule kutoa ufafanuzi iwapo jambo hilo limefikishwa rasmi ofisini kwake alisema mpaka sasa bado hajapelekewa tuhuma hizo na kwamba ndani ya saa 48 kuanzia sasa atakuwa amejua ukweli wa tuhuma hizo.

"Bado hawajaniletea lakini kwa sababu Ofisa Maendeleo ya Jamii alikuwapo na ndiye aliyepokea taarifa ya tuhuma hizo ataniletea, na nitazifanyia kazi haraka baada ya kujiridhisha mimi na kamati yangu ya ulinzi na usalama," alieleza Mkuu huyo wa Wilaya.

NIPASHE JUMATATU JANUARI 27, 2020

Nipashe

# Spotika




**SABABU 3 KWANINI LACAZETTE AJIUNGE NA ATLETICO MADRID** UK. 20



## ISIKUPITE

LIVERPOOL imekuwa timu ya kwanza tangu Arsenal msimu wa 2001-02, kuweza kufumania nyavu katika mechi zake 23 za kwanza za msimu katika Ligi Kuu England. Hata hivyo, 'Gunners' yenyewe iliendelea kufunga hadi ilipotwaa ubingwa msimu huo.

# HUPITI HAPA

Beki wa Barcelona, Gerard Pique (kushoto), akimkwatua mshambuliaji wa Valencia, Jose Gaya ndani ya eneo la 18 katika mechi ya Ligi Kuu Hispania maarufu La Liga iliyochezwa juzi usiku na kusababisha mwamuzi wa mchezo huo kuamuru pigo la penalti. Barcelona ilichapwa mabao 2-0. **PICHA: MTANDAO**



# MESSI

## KWA AGUERO, MILAN KWA MODRIC

**BARCELONA, Hispania**

WAKATI dirisha la usajili la Januari ambapo ni kipindi cha majira ya baridi barani Ulaya, likiwa linaendelea, kumekuwa na taarifa tofauti tofauti kwa timu ambazo zinataka kuimarisha vikosi vyao.

Lionel Messi ameiomba Barcelona kumsajili Sergio Aguero, huku Inter Milan ikipanga kutoa ofa kwa Luka Modric wakati huu wa dirisha dogo la usajili la Januari.

**MESSI AMTAKA AGUERO**

Kocha mpya wa Barcelona, Quique Setien ameripotiwa kuyadharau maombi ya Messi anayetaka klabu yake hiyo imsajili mshambuliaji wa Manchester City, Sergio Aguero, kwa mujibu wa Express.

Setien alichukua nafasi ya Ernesto Valverde pale kwenye dimba la Nou Camp na tayari anaonekana kutaka kukijenga upya kikosi hicho.

Gazeti la Mirror limedai kuwa Messi amemshauri Setien kumsajili nyota huyo wa City, ambaye amekuwa ana upatina mzuri wakiwa kwenye kikosi cha Argentina.

**MILAN WAVUTIWA NA MODRIC**

Imeelezwa kuwa Inter Milan wanapanga kufufua mpango wao wa kutaka kumsajili kiungo wa Real Madrid, Luka Modric kwa mujibu wa Daily Mail Sport, ambalo limedai kwamba, Inter wameendeleza mpango wao huo wa kumwania kiungo huyo wa Timu ya Taifa ya Croatia baada ya ofa yao ya mwaka jana kukataliwa.

Modric, ambaye anafikisha umri wa miaka 35 Septemba mwaka huu, ameingia kwenye miezi yake 18 ya mwisho kwenye mkataba wake pale Bernabeu na atakuwa mchezaji huru kwa kipindi cha mwaka mmoja.

Imedaiwa kwamba Madrid watasikiliza ofa kutoka kwa Modric kipindi cha majira ya joto wakiepuka kumkosa akiwa mchezaji huru na miamba hao wa Italia wanaongoza kwenye mbio za kuwania saini yake.

**PSG 'WAIBANIA' ATLETICO**

Atletico Madrid imetoa ofa ya euro milioni 10 kwa ajili ya kumsajili Edinson Cavani mwezi huu, lakini Paris Saint-Germain wana mpango wa kumbakisha mshambuliaji huyo na wamekataa ofa hiyo kwa mujibu wa RMC.

Mshambuliaji huyo atakuwa huru Juni mwaka huu wakati mkataba wake na mabingwa hao wa Ufaransa utakapomalizika.

Lakini kocha wa Atletico, Diego Simeone anaamini nyota huyo ataongeza nguvu kwenye kikosi chake na anataka kumsajili mwezi huu kwa ajili ya timu yake kupata mabao mengi, ambapo msimu huu wameweza kufunga magoli 22 tu katika mechi 20.

Huku PSG wakiwa na nia na kulitwaa taji lao la kwanza la Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu, klabu hiyo inataka kuwa na mshambuliaji aliyekamilika kama Cavani na kama msaidizi wa Mauro Icardi, ambaye amekuja klabuni hapo kwa mkopo.

**LIVERPOOL, CHELSEA ZAMWANIA WERNER**

Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp anavutiwa kwa muda mrefu sana na Timo Werner kwa mujibu wa Daily Mirror.

Klabu hiyo sasa ipo kwenye mikakati ya kutaka kumsajili, lakini wapo kwenye mbio moja na wapinzani wao kwenye Ligi Kuu England, Chelsea.

Klabu zote mbili zinawania saini ya mchezaji huyo wakati wa kipindi cha majira ya joto msimu huu.

Chelsea tayari imefungua majadiliano na mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani mwezi huu baada ya kupunguziwa kwa adhabu yao ya kutosajili na Shirikisho la Soka la kimataifa, (Fifa).

Na sasa Blues hao wanataka kumsajili mshambuliaji huyo ambaye amefunga mabao 18 katika mechi 17 za Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, alizocheza msimu huu.

Werner mwenyewe tayari alishaonyesha nia ya kutaka kucheza kwenye Ligi Kuu England, ingawa inaonekana wazi kuwa klabu yake ya sasa ya RB Leipzig haitakuwa tayari kumwachia, Werner hadi kipindi kijacho cha majira ya joto ambapo inaamini kwamba watakuwa na nafasi ya kupata fedha ndefu.

**JE, WAJUA?**



KIPA wa Liverpool, Alisson amekuwa mlinda mlango wa kwanza kutoa pasi ya mwisho 'assist' kwenye Ligi Kuu England tangu Machi, 2010 wakati Pepe Reina alipofanya hivyo wakati 'Wekundu' hao wakicheza dhidi ya Sunderland.

MICHEZO

# SAMATTA ALIVYOWAHAMISHIA WATANZANIA ASTON VILLA

**Na Adam Fungamwango**

HABARI ya nchi kwa wiki nzima hii ilikuwa ni nahodha wa timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), Mbwana Samatta ambaye amejiunga na klabu ya Aston Villa inayoshiriki Ligi Kuu England.

Samatta amelamba mkataba mnono wa miaka minne na nusu akitokea Genk ya Ubelgiji, iliyomsajili kutoka TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), ambayo nayo ilimsajili kutoka kwa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba ya jijini Dar es Salaam.

Kwa sasa Samatta ameshaanza mazoezi na mambo yakienda kama yalivyopangwa anaweza kucheza kwenye mechi ya kwanza ya Ligi Kuu England hapo Februari Mosi, mwaka huu dhidi ya AFC Bournermouth, saa 12:00 jioni kwa saa za Afrika Mashariki.

Pilikapilika za Wabongo zilianza pale zilipoanza kama tetesi hivi, lakini baadaye taarifa zikaja kuwa kweli, lakini tatizo likaja pale kwenye kumtangaza ambapo kulikuwa na ucheleweshwaji kutokana na kupitia taratibu mbalimbali za kisheria.

Wabongo wakavamia kwenye akaunti ya instagram ya Aston Villa, wengine wakipongeza na wengine wakionyeshwa kushangazwa na ucheleshwaji huo.

Mara tu baada ya kutangazwa, mtandao huo ulivamiwa na mashabiki wengi kutoka Tanzania na lugha ya Kiswahili ndiyo ikawa inatawala, unaweza ukadhani ni instagram ya klabu moja pale Manzese.

Hata baadhi ya wazungu walionyeshwa kushangazwa na wingi wa Wabongo kuingia kwenye mtandao wa kijamii wa Aston Villa, wengine wakishangazwa na lugha iliyokuwa ikitumika, kwani baadhi hawaifahamu.

Taarifa zinasema kuwa wakati wa tetesi za Samatta kuhamia timu hiyo zilipoanza, mtandao wa instagram wa klabu hiyo ulianza kuongeza idadi ya watu walioingia, ambao inadaiwa wengi wao walikuwa ni Watanzania.

Wabongo wengi kwenye mitandao ya kijamii, vijiweni na mitaani, wameonekana kuanza kuifuatilia na kuishabikia Aston Villa, ukiacha klabu zao pendwa za England ambazo wengi wao ni mashabiki wa Manchester United, Arsenal, Liverpool na Chelsea.

Viongozi wa serikali, vyama vya siasa, watu maarufu, wanamuziki na wasanii mbalimbali wamekuwa wakituma salamu za pongezi wa Samatta kwa kuwa Mtanzania wa kwanza kucheza Ligi Kuu England.

"Hongera sana Mbwana Samatta kwa hatua kubwa ambayo umepiga kwenye maisha yako. Wanasimba tunakutakia kila la kheri kwenye timu yako mpya ya Asyon Villa." Uliandika mtandao wa klabu ya Simba ambayo aliichezea mwaka 2011, kabla ya kujiunga kwa mabingwa wa zamani wa Afrika, TP Mazembe.

Klabu ya Yanga, iliandika kwenye mtandao wake wa kijamii maneno yafuatayo.

"Hongera sana Samatta kwa kuendelea kuwa balozi mzuri wa soka la Tanzania."

Klabu ya Mbeya City pia iliandika waraka wa kumpongeza.

"Klabu inampongeza Mbwana Samatta, mshambuliaji na kapteni wa Taifa Stars, ambaye ni kaka mdogo wa aliyewahi kuwa mchezaji wetu Mohamed Samatta kwa kujiunga na Aston Villa inayocheza Ligi Kuu England.

Mkoa wa Mbeya una historia ndefu na Samatta tangu alipokuwa mdogo na familia yake huko Uzunguni, akishuhudia kaka zake wakisakata kabumbu kwenye uwanja wetu mashuhuri wa Ngoma, ulioibua vipaji vingi."

Baba mzazi wa Samatta, Ally Samatta amesema kuwa mtoto wake hadi kufika hapo, pamoja na kuwa ni mipango wa Mwenyezi Mungu, lakini nidhamu na kujituma ndiyo siri ya mafanikio.

"Mbagala ni sehemu ambayo kuna kila aina ya mambo ambayo yanaweza kusababisha mtoto akapotea, kuna magenge ya wezi, wakaa vijiweni, walevi, lakini mimi nilikuwa nikisimamia nidhamu kwa watoto wangu," anasema na kuongeza.

"Hata wanawake wakati mwingine wanakuja nyumbani kugonga na kumuulizia, lakini mimi natoka na kuwatimua. Halafu nikikaa naye na kumwambia kuwa ili ufanikiwe kwenye maisha yako ya soka, vitu kama hivi jiepushe navyo na hasa alipoanza kuichezea Simba. Nashukuru alinisikia na kufuata nilivyomwambia hadi leo yuko hapo." Anasema baba wa nahodha huyo wa Stars.




Mshambuliaji mpya wa Aston Villa, Mbwana Samatta, akiwa katika mazoezi ya timu hiyo baada ya kujiunga na klabu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu England, wiki iliyopita.

## NJE YA UWANJA

KAMA klabu ya Real Madrid ya Hispania itafanikiwa kufuzu kucheza nusu fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu, ikiwa ni mara ya kwanza tangu inyakue taji hilo msimu wa 2017/18, itakuwa timu ya kwanza kucheza mechi 100 kwenye hatua ya mtoano ya michuano hiyo. Kikosi cha Madrid kinafundishwa na nyota wa zamani wa timu hiyo Mfaransa Zinedine Zidane.

Extra Time



# SABABU 3 LIVERPOOL ITAPOTEZA KABLA YA MWISHO WA MSIMU EPL

**LIVERPOOL, England**

BAADA ya ushindi wao dhidi ya Manchester United, inaonekana wazi Liverpool watashinda taji la Ligi Kuu England msimu huu, lakini je, watamaliza msimu huu bila kupoteza mchezo wowote?

Baada ya ushindi huo mkubwa kwenye dimba la Anfield wikendi iliyopita, Liverpool sasa wanaonekana kuelekea kumaliza ukame wa miaka 30 wa kusubiri taji la Ligi Kuu England.

Wekundu hao wapo kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu England wakifikisha pointi 67 baada ya mechi 23, wakiongoza kwa kwa pointi 16 dhidi ya wapinzani wao wa karibu Manchester City, huku wakiwa na mchezo mmoja mkononi.

Sasa kikosi hicho cha Jurge Klopp kinaweza kufikia rekodi iliyowekwa na Arsenal msimu wa 2003-04 ambapo walimaliza msimu bila kupoteza mchezo wowote.

Lakini je, Wekundu hao wataweza? Hapa tunaangalia sababu tatu kwanini Liverpool haitamaliza msimu wa 2019-20 bila kupoteza mchezo.

1. WAMEBAKIA NA MECHI NGUMU

Liverpool imepata mechi ngumu zilizoongozana kwa wikendi mbili zilizopita kwa kuifunga Tottenham Hotspur na Manchester United, lakini bado wana ratiba za mechi nyingine ngumu hadi kumalizika kwa msimu huu.

Wekundu hao wanaonekana kuwa na mechi ngumu zinazofuata kwa Januari na Februari, huku pia wakiwa wamevuka kihunzi cha mechi ngumu dhidi ya Wolves ambapo walipata ushindi wa 2-1.

Liverpool sasa watakabiliwa na mchezo dhidi ya wapizani wao wa jiji moja, Everton pale kwenye dimba la Goodison Park - Machi 14, mwaka huu na halafu watafuatiwa na mchezo dhidi ya vijana wa Roy Hodgson, Crystal Palace wiki moja baadaye.

Lakini hilo sio kubwa, kwani bado wanakabiliwa na mechi na timu kubwa sita za ligi hiyo kabla ya msimu kumalizika.

Vijana hao wa Klopp watakuwa na kibarua kigumu dhidi ya bingwa mtetezi, Manchester City kwenye Uwanja wa Etihad Aprili 4 mwaka huu, na mbili kati ya tatu za mwisho wanaonekana watakabiliana na miamba wa Jiji la London, Arsenal na Chelsea.

Ni kweli kwamba, wekundu hao wameweza kuvuka vihunzi vingi, lakini mechi dhidi ya timu kama Brighton, Aston Villa na Burnley, kwa hakika zitakuwa ngumu kwa upande wao.

Hivyo, Liverpool watakuwa na wakati mgumu mno kuifikia rekodi ya Arsene Wenger na Arsenal aliyoiweka msimu wa 2003-04.

2. LIGI YA MABINGWA ULAYA

Taji la Ligi Kuu England ni muhimu zaidi kwao, lakini Liverpool hawatakuwa na uhakika wa kubeba taji lingine msimu huu, ikiwamo kutetea kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Wekundu hao bila shaka, walishinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita kwa kuifunga Tottenham kwenye fainali na yatakuwa mafanikio makubwa zaidi kwa kikosi hicho cha Klopp kutetea taji hilo Mei mwaka huu, hasa ikizingatiwa kuwa hakuna klabu yoyote ya Ligi Kuu England imeweza kutwaa taji hilo mara mbili mfululizo.

Kutetea taji hilo, Liverpool watatakiwa kupambana hasa; hasa kwa kuwa wamepangwa na kikosi cha Diego Simeone, Atletico Madrid kwenye raundi ya mtoano wa timu 16. Ingawa kiwango cha sasa cha Liverpool kina wapa nafasi kubwa ya kufuzu hatua ta robo fainali.

Bila shaka timu yoyote inayokwenda kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya itakuwa inatarajia kukutana na kikosi kigumu kutoka Ulaya na Liverpool watatakiwa kujithibitishia ubora wao huku wakiendelea kucheza bila kupoteza mchezo kwenye Ligi Kuu England.

Arsenal waliondolewa kwenye hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati wa msimu wao wa kutopoteza mechi kwenye Ligi Kuu 2003-04, huku wengi wakiwa na matarajio kwamba, Arsene Wenger angeweza kuhamishia nguvu ya EPL kwenye michuano hiyo ya Ulaya.

Je, Klopp ataweza kufikia hatua hiyo? Ni ngumu kufikiria, kutetea taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya pengine kutakifanya kikosi cha Liverpool kuwa timu bora ya wakati wote kwenye Ligi Kuu England.

Kushinda taji la Ligi Kuu na wakati huo huo kutetea kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya, kunaweza kuwa kugumu zaidi kuliko kumaliza msimu wote bila kupoteza mchezo na hilo lina maana kwamba, Klopp anaweza kuwa na hatari ya kuwapumzisha baadhi ya nyota wake muda mfupi kwa ajili ya michuano hiyo ya Ulaya, na hilo litamfanya kuwa kwenye hatari ya kupoteza rekodi yake ya kutopoteza mchezo kwenye ligi ya nyumbani.

3. KUJIACHIA WAKISHATWAA TAJI

Ni wazi bila shaka yoyote kwamba sasa Liverpool wanakwenda kushinda taji la Ligi Kuu England; mashabiki wake walionekana kuimba kwa furaha wikendi iliyopita wakati walipopata ushindi dhidi ya Manchester United kwa kuimba "Tunakwenda kushinda taji la Ligi Kuu!" Lakini likija suala la kwenda msimu wote bila kupoteza, kiwango chao kinaweza kuthibitisha kwamba ni laana kuliko baraka.

Dalili za mapema kabisa zitakazoonyesha wekundu hao wanaweza kulitwaa taji hilo ni pale watakaposhinda mchezo wao wa Februari 29, mwaka huu dhidi ya Watford, kwenye mchezo wao wa 28 wa msimu. Lakini hilo litawataka kuendelea kushinda mechi zao kabla ambapo watacheza na Manchester City na timu nyingine kama Leicester.

Hata hivyo, siyo jambo rahisi sana kwa vijana hao wa kocha, Klopp kuweza kupata ushindi kwenye mchezo wao pale katika dimba la Goodison Park watakapocheza dhidi ya Everton, Machi 14, mwaka huu. Kama hilo litatokea, Liverpool bado wanaweza kuwa na mechi nane zilizobakia huku wakiwa tayari wameshinda taji.

Hata kama wataweza kushinda taji kwenye Uwanja wa Etihad Aprili, mwaka huu, kitu kitakachowataka wote kushinda mechi zao zilizobakia, ambapo watatakiwa kuepuka kipigo kutoka kwa Aston Villa, Burnley na Brighton, pamoja na Chelsea na Arsenal.


Na kumbuka wakati huo watakuwa wameshashinda taji la Ligi Kuu, hivyo kwa namna yoyote wachezaji watacheza kwa kujiachia kwa kuridhika kwamba wameshatwaa kombe walilokuwa wakiliwania kwa msimu wote. Na hapo ndio watakapojikuta wakipoteza mechi zilizobakia kwa urahisi zaidi, kwani watacheza kwa kutokuwa na wasiwasi wowote, maana kama ubingwa tayari wanao mkononi na hakuna wa kuwapokonya kwa wakati huo.

## Nukuu

"Siku ambayo Didier [Deschamps] ataamua kuondoka au mkataba wake kutoongezwa, na kama Zidane [Zinedine] atakuwapo, yeye ndiye atachukua nafasi hiyo. Kuna Qatar [Kombe la Dunia 2022] Didier atakuwa pale na halafu baada ya hapo sijui kitakachotokea," **Rais wa Shirikisho la Soka la Ufaransa (FFF), Noel Le Graet akizungumzia uwezekano wa Zidane kuinoa timu ya Taifa ya Ufaransa.**



"Wakati Chelsea inataka ushindi, inamwingiza Michy Batshuayi na wakati Manchester City wakitaka kumbadilisha Gabriel Jesus, wanamwingiza Sergio Aguero, sisi [Tottenham] hatuna bahati, tuna majeruhi wengi. Hugo Lloris amerudi na tumempoteza Harry Winks, uhaba wa mshambuliaji unanilazimisha kufikiri, kufikiri na kufikiri zaidi," **Kocha wa Spurs, Jose Mourinho.**



"Yeye ni mchezaji mzuri [Edinson Cavani wa PSG], nilicheza dhidi yake na kila wakati, nilikuwa napenda mawazo na mtazamo wake na ni wazi rekodi yake ya ufungaji mabao inajielezea yenyewe. Ni mchezaji mzoefu lakini kuna wachezaji wengine wengi pale. Tu wachanga kama kikosi, kuleta mchezaji mzoefu ni kitu ambacho siwezi kukiweka mbali," **Kocha wa Chelsea, Frank Lampard.**



Michezo



Mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Wasichana ya Umri chini ya miaka 17, Aisha Masaka (kulia), akipambana kuwania mpira dhidi ya beki wa Uganda, Rose Mpoma, uliochezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA : JUMANNE JUMA**

# SERENGETI GIRLS YAPIGA HATUA KOMBE LA DUNIA

**Na Adam Fungamwango**

GOLI pekee lililofungwa na Protasia Mbunda limeifanya timu ya Taifa ya wasichana ya umri chini ya miaka 17 (Serengeti Girls), kusonga mbele katika safari ya kuwania tiketi ya kucheza Fainali za Kombe la Dunia za vijana zitakazochezwa baadaye mwaka huu nchini India.

Mechi hiyo iliyochezwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Intwari mjini Bujumbura nchini Burundi ilikuwa ni ya marudiano baada ya ile ya kwanza iliyochezwa Januari 12, mwaka huu jijini Dar es Salaam, wasichana hao wa Kibongo waliposhinda kwa mabao 5-1.

Kwa ushindi huo, Tanzania inasonga mbele kwa jumla ya mabao 6-1. Katika mechi ya kwanza, magoli yalifungwa na Aisha Masaka aliyefunga magoli matatu peke yake, 'hat-trick', Joyce Meshack na Mbunda pia alifunga goli kwenye mechi ya kwanza, huku la kufutia machozi la Burundi likifungwa na Lydia Karenzo.

Wasichana hao wa Tanzania ambao wanaonekana kwa sasa ni moto wa kuotea mbali, wanatarajia kumenyama na mshindi kati ya Uganda na Ethiopia ambazo zilitarajia kurudiana jana jioni nchini Ethiopia, baada ya mechi ya kwanza nchini Kampala, Uganda kuibuka na ushindi wa mabao 2-0.

Tanzania au Serengeti Girls ina mechi nne mbele ili kufuzu fainali hizo.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Bakari Shime amewapongeza wachezaji wake kwa kupambana katika mechi zote mbili na kuongeza kuwa amefurahishwa na matokeo hayo.

Shime alisema dhamira ilikuwa ni kwenda kushinda kwa idadi kubwa ya magoli kama ilivyokuwa mwanzo, lakini walikuta wenzao nao wamejizatiti kupindua matokeo, lakini kulikuwa na upungufu kadhaa ambao umeuona na kuahidi kuufanyia kazi.

"Lengo ilikuwa ni kushinda magoli mengi, lakini haikuwezekana, wenzetu walijizatiti kupindua matokeo, lakini nasi tukawa na upungufu, lakini tumeshinda tunashukuru Mungu," alisema kocha huyo.

Kabla ya mechi hiyo ya marudiano, wachezaji wa timu hiyo walitembelea kwenye ubalozi wa Tanzania nchini Burundi na kukutana na Balozi Dk. Jilly Maleko ambaye mbali na kuwapa nasaha, lakini alieleza kufurahishwa na ushindi mkubwa walioupata nyumbani na kuwataka 'kupigana' kufa au kupona kuhakikisha wanapata tena ushindi kwa mara ya pili.

"Nafurahi sana kuwaona na niliposikia kuwa mnakuja hapa kwa ajili ya mechi ya marudiano, najua mlicheza mechi ya kwanza na mkafanya vizuri sana, nikaongea na maafisa wenzangu na kuwaagiza kwamba mnapokelewa vizuri, nafurahi kuniambia kwamba mmelala salama na hali ya hewa haitofautiani na ya Tanzania, tena huku joto si kubwa sana, na hata Burundi na Tanzania hatutofautiani sawa na hata vyakula nadhani mmekula vyakula viko sawa tu. Natumai mtatoka na ushindi na jina la Tanzania litazidi kupaa juu, alisema balozi huyo kabla ya mechi ya marudiano.

**MAANDALIZI SAFI YAMEWABEBA**

Kikosi hicho cha Tanzania kimekuwa katika maandalizi ya muda mrefu kwa ajili ya mashindano hayo ya dunia.

Kikiwa chini ya Shime, wachezaji wa Serengeti Boys waliingia kambini Oktoba mwaka jana sambamba na kikosi cha Kilimanjaro Queens kilichokuwa kinajiwinda na michuano ya Kombe la Chalenji kwa nchi za Afrika Mashariki na Kati.


Kwa maana hiyo, mbali na kupata mechi za kirafiki, pia wachezaji wake walionyesha ushindani na baadhi yao kuwa kwenye kikosi cha Kilimanjaro Queens, akiwamo mshambuliaji tegemeo, Aisha Masaka.

Pia kilipata uzoefu wa mechi za kimataifa baada ya kushiriki michuano ya Kombe la Chalenji iliyochezwa Desemba mwaka jana mjini Jinja, Uganda na kumaliza katika nafasi ya pili, nyuma ya wenyeji Uganda ambao walitwaa ubingwa wa kwanza wa mashindano hayo yaliyoandaliwa na Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (Cecafa).

Katika mashindano hayo, Serengeti Girls walishinda mechi tatu dhidi ya Kenya, Djibouti na Eritrea huku wakitoka sare na Burundi na Uganda.

Kila la kheri katika safari ya kupeperusha bendera ya Tanzania katika michuano hiyo.


**NAJUA WAJUA**



TANGU kuanza kwa msimu uliopita, beki wa pembeni wa Liverpool, Trent Alexander-Arnold ndiye mwenye pasi nyingi za mwisho 'assists' (22) kwenye Ligi Kuu England kuliko mchezaji mwingine yeyote katika ligi hiyo.

SOKA

# MECHI 5 ZA MABAO MENGI LIGI 5 ULAYA




**LONDON, England**

BADO msimu wa Ligi Kuu mbalimbali za Ulaya unaendelea na sasa ni nusu ya msimu huu wa 2019/2020.

Hapa tunaangalia mechi tano zilizofungwa mabao mengi zaidi kwa ligi kuu tano za Ulaya kwa msimu huu.

**5. Atalanta 7-1 Udinese (Italia, Serie A)**

Atalanta imekuwa moja ya timu inayovutia zaidi barani Ulaya kwa misimu michache iliyopita, hasa kwa staili yao ya uchezaji chini ya kocha, Gian Piero Gasperini ambaye anafananishwa na Pep Guardiola.

Msimu uliopita Bergamo hao walimaliza kama ndio timu iliyofunga mabao mengi zaidi kwenye Ligi Kuu Italia, Serie A, na wakapata nafasi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara ya kwanza, huku wakitinga fainali ya Kombe la Coppa Italia na wachezaji kama Papu Gomez, Josip Ilisic, Duvan Zapata na Luis Muriel wakiliongoza jahazi hilo.

Msimu huu, wameendelea kuwa kwenye kiwango kile kile walichokuwa nacho msimu uliopita.

Mchezo wao dhidi ya Udinese kwenye dimba la Atleti Azzurri d'Italia kwenye mchezo wa tisa wa Serie A kwa hakika waliwanyanyasa wapinzani wao.

Wageni walianza kwa bao la kuongoza lililofungwa na Stefano Okaka dakika ya 11, lakini haraka Atalanta ikabadili matokeo na hadi kipindi cha kwanza kinamalizika walikuwa wanaongoza kwa magoli 3-1.

Mabao manne ya kipindi cha pili ndio yalibadilisha kila kitu, huku Luis Muriel ambaye alikuwa nyota wa mchezo aliibuka na 'hat-trick'.

**4. Manchester City 8-0 Watford (England, EPL)**

Katika historia yake ya miaka 120, soka la Uingereza halijawahi kushuhudia timu moja ikitawala kwa kipindi kirefu cha miaka mitatu kama Manchester City, huku wakishinda mara mbili mfululizo taji la Ligi Kuu England.

Wakiwa wamepoteza kwa mshtuko kwa kufungwa 3-1 dhidi ya Norwich City kwenye mechi ya nane, City ilionekana kutokuwa kwenye wakati mzuri.

Hasira zao wakazishusha kwa Watford, kwani katika mchezo wao ndani ya dakika 20 walijikuta wakiongoza kwa mabao matano na mabao mengine matatu yakifungwa kuanzia dakika ya 70.

Kulikuwa na wafungaji watatu tofauti kwenye mchezo huo na Bernardo Silva alipata hat-trick yake ya kwanza hapo City, ambapo pia ukawa mwanzo wa mwisho wa Quique Sachez Flores kuwa kwenye benchi la Watford.

**3. Leipzig 8-0 Mainz (Ujerumani, Bundesliga)**

RB Leipzig waliwashtua wengi wakati walipomaliza nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, kwa mara ya kwanza katika historia yao.

Julian Nagelsmann amekijenga kikosi imara baada ya kazi nzuri ya Ralph Hasenhuttl na Leipzig kwa sasa wapo kileleni mwa Bundesliga kwa tofauti ya pointi nne baada ya mechi 18.

Pia ndio timu inayofunga mabao mengi zaidi Ujerumani, ambapo walifikisha magoli 51 hadi kwenye mechi yao ya 10 dhidi ya Mainz 05.

Kiungo Marcel Sabitzer alianza kwa kufunga bao la kwanza dakika ya tano na kuanzia hapo mambo yakawa mazuri zaidi kwa Leipzig ambapo walifunga mabao mengine saba na kupeleka ujumbe mzito kwa timu nyingine za Ligi hiyo.

Mshambuliaji nyota, Timo Werner alikuwa kwenye kiwango cha kuvutia, akifunga bao la pili, la sita na la nane kuweza kujipatia hat-trick.

**1. Southampton 0-9 Leicester (England, EPL)**

Leicester City haikuwa na mafanikio mazuri zaidi hadi waliposhinda taji la Ligi Kuu England mwaka 2016, lakini msiu huu wanaonekana wapo vizuri.

'Mbwea' hao tangu wamwajiri Brendan Rodgers kuwa kocha mkuu Februari mwaka jana, walicheza mechi nane mfululizo kwa kupata ushindi mapema msimu huu na kujipambanua wao wenyewe kama washindani wa Liverpool kwenye mbio za Ligi Kuu.

Mechi yao ya pili kati ya nane za ushindi ilikuwa ni ile ya 10 iliyopigwa kwenye dimba la St Mary dhidi ya Southampton ikiwa ni siku ya Ijumaa jioni.

Beki wa kushoto, Ben Chilwell alianza kuwafungia dakika ya 10 na kadi nyekundu ya Ryan Bertrand kwa Southampton dakika moja baadaye ikaja kushuhudia mabao mengine nane yakifungwa na kuwa ushindi mkubwa zaidi kwenye historia ya Ligi Kuu England.

Mshambuliaji, Jamie Vardy ambaye kwa sasa anaongoza kwenye orodha ya wafungaji bora kwenye Ligi Kuu England akiwa na mabao 17, alikuwa mmoja wa wachezaji wawili waliofunga hat-trick kwenye mchezo huo pamoja na Ayoze Perez, huku James Maddison na Youri Tielemans pia nao walifunga bao moja kila mmoja.

NDANI YA 18

UEFA CHAMPIONS LEAGUE

NI timu tatu tu, Real Madrid yenye magoli 166, Bayern Munich (164) na Barcelona (159) ambazo zimefunga mabao zaidi ya 100 kwenye hatua ya mtoano ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.



BAADA ya ushindi wao dhidi ya Manchester United, inaonekana wazi Liverpool watashinda taji la Ligi Kuu England msimu huu, lakini je, watamaliza msimu huu bila kupoteza mchezo wowote?

**Uk. 16-17**



# SABABU 3 KWANINI LACAZETTE AJIUNGE NA ATLETICO MADRID

**LONDON, England**

HADI sasa Atletico Madrid wapo sokoni wakitafuta straika kwa ajili ya kuimarisha safu yao ya ushambuliaji.

Msimu huu kikosi hicho cha kocha Diego Simeone kimefunga mabao 22 katika mechi 20 za Ligi Kuu England, yakiwa 16 machache zaidi kuliko wapinzani wao Real Madrid na yakiwa 28 machache kuliko kwa Barcelona.

Edinson Cavani na Alexandre Lacazette wanaongoza kwenye mbio za kuwaniwa na Los Rojiblancos, huku dili hilo linaonekana kukamilika kabla ya mwisho wa kipindi cha dirisha dogo la usajili, kipindi hiki cha majira ya baridi.

Kuondoka kwa Lacazette pale Arsenal kunaonekana kuna uwezekano mkubwa zaidi tofauti na ilivyokuwa miezi michache iliyopita. Bahati mbaya kwa Mfaransa huyo, mambo hayajakuwa mazuri sana kwake pale kwenye dimba la Emirates.

Katika umri wake wa miaka 28 hadi sasa amefunga mabao matano kwenye Ligi Kuu England na amecheza mechi nane bila kufunga bao.

Hapa tunaangalia sababu 3 kwanini Lacazette anatakiwa kwenda Atletico Madrid kipindi hiki.

**3. ARSENAL INAHITAJI KUUZA ILI KUJIIMARISHA**

Ukweli lazima usemwe, Arsenal wapo kwenye awamu ya kipindi cha mpito kwa sasa. Washikabundi hao wanahitaji kuuza 'mbao zilizooza' huku wakileta wachezaji wengine wa kiwango cha juu. Ili kupata fedha za kukijenga kikosi hicho, mmiliki wake Stan Kroenke ameweka wazi kwamba klabu yake inatakiwa kutumia fedha.

Hadi sasa sio Pierre Emerick-Aubameyang wala Lacazette ambao wamesaini mkataba mpya, wakati mikataba yao ya sasa inatarajia kumalizika kipindi cha majira ya joto kijacho.

Ujumbe wa zama mpya uko wazi, sainisha mkataba mpya au uza. Siku za kumwachia mchezaji aondoke akiwa huru zishapita na wakati, kwa sasa wanatakiwa angalau kufanya uwekezaji kwa kuuza na kununua wapya.

Kuondoka kwa Lacazette kwenda Atletico Madrid kutaipa Arsenal nafasi nzuri zaidi ya kupata fedha za kujijenga. Na kama ikiwa ni kuchagua kati ya nyota huyo mwenye asili ya Gabon na yeye, ni wazi kabisa mashabiki wa Arsenal watamchagua yeye kuondoka. Rekodi yao ya ufungaji mabao haiwezi kulingana kwa namna yoyote ile.

**2. HAJAISHI KWENYE MATARAJIO YAKE**

Labda ni bahati mbaya kwa raia huyo wa Ufaransa kwamba, Aubameyang alitua hapo miezi sita baada ya yeye kufika. Kwa sababu kwa ulinganisho wao, mshambuliaji huyo ameshafikia matarajio yake.

Katika mechi 97 alizoichezea Arsenal, Aubameyang amefunga mabao ya kuvutia 57, akiwa na wastani wa 1.7 kwa mchezo. Lacazette amefunga mabao 42 katika mechi 118, sawa na kufunga goli katika kila mechi 2.8. hilo sio jambo zuri kwa mchezaji aliyeigharimu timu pauni milioni 46.5 kupata saini yake.

Kama tukiangalia ukweli, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 ubora wake wa kufunga kwenye Ligi Kuu kwa msimu ni mabao 14. Alisajiliwa kwa malengo ya kufunga mabao 30 kwa msimu wakati akichukua mikoba ya Robin Van Persie, badala yake hajafikisha hata mabao 20 kwa msimu.

Kwa kipindi cha misimu miwili iliyopita, ameifanya safu ya ushambuliaji ya Arsenal kuwa na nguvu, lakini kiuhalisia, Mfaransa huyo hana uwezo wa kuonyesha ubora wake zaidi. Unai Emery alitaka kutengeneza safu ya washambuliaji watatu kama Liverpool, huku Lacazette akiwa kama namba 9, hata hivyo, haraka akaona kwamba hawezi kufikia malengo yake.

**1. KUFUFUA MATUMAINI YA EURO 2020**

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 hajacheza mchezo wowote kwa timu ya taifa ya Ufaransa tangu Novemba 14 mwaka 2017, ambapo alifunga mabao mawili kwenye mchezo wa kirafiki dhidi ya Ujerumani.

Tangu hapo kocha Didier Deschamps hajaona kama mshambuliaji huyo ana thamani ya kuwa kwenye kikosi chake cha wachezaji 23.

Aliwekwa 'standibai' kwa kuweka kwenye kikosi kilichoshiriki fainali za Kombe la Dunia mwaka 2018, lakini hakuweza kuitwa. Kabla ya hapo Lacazette alicheza mechi 16 kwa nchi yake, akifunga mabao matatu.

Kumbuka kwamba mchezaji huyo pia amewahi kuiwakilisha nchi yake katika timu za vijana za umri chini ya miaka 16 na 21.

Kama fowadi huyo wa Arsenal anataka kufufua matumaini yake ya kuichezea timu yake ya taifa, anatakiwa kuondoka sasa. Ni wazi kwamba, maisha na staili ya pale Arsenal inamfanya, Lacazette kutofiti kwenye soka la Uingereza.

Mabingwa wa Dunia Ufaransa, macho yao yatakuwa kwenye mashindano ya Euro 2020 kipindi cha majira ya joto msimu huu. Kama Lacazette anaweza kwenda Atletico Madrid, atakuwa na nafasi ya kurudisha nafasi yake msimu huu kwa kufunga mabao zaidi na kupata nafasi ya kucheza Euro 2020.

**USILOLIJUA**



ARSENAL imeonyeshwa kadi nyekundu nyingi kwenye Ligi Kuu England ikicheza dhidi ya Chelsea (kadi 8) kuliko ikicheza na timu nyingine yoyote kwenye ligi hiyo.





Baadhi ya wananchi wakiwa wamekaa eneo lisiloruhusiwa, huku wakiwa wamekanyaga sehemu inayotakiwa kukaliwa katika vibanda vya kupumzikia abiria kwenye stendi ya mabasi ya Nanenane jijini Mbeya juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Takukuru yaokoa mil. 168/- kutoka viongozi mitaa, ushirika

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Mbeya imeokoa zaidi ya Sh. milioni 168 za umma ambazo zilikuwa zimefujwa na baadhi ya viongozi katika kipindi cha miezi mitatu kuanzia mwezi Oktoba mpaka Desemba mwaka jana.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake mwishoni mwa wiki, Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Mbeya, Julieth Matechi, alisema fedha hizo zote zilikuwa zimetumiwa vibaya na watendaji wa vijiji na mitaa pamoja na viongozi wa vyama vya ushirika vya wakulima (Amcos).

Alisema awali walibaini kuwa kulikuwa na ubadhirifu wa zaidi ya Sh. milioni 100 uliokuwa umefanywa na watendaji wa vijiji na mitaa katika Halmashauri za Jiji la Mbeya, Kyela na Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya waliokuwa wamepewa jukumu la kukusanya mapato ya serikali kwa kutumia mashine za 'Point of sale' (Pos).

Matechi alisema Takukuru ilishirikiana na viongozi wa halmashauri husika na kufanikiwa kuokoa Sh. milioni 87.7 ambazo zilirejeshwa na watendaji hao.

Alisema katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya fedha zilizokuwa zimepigwa zilikuwa Sh. milioni 44.3 na ndiyo halmashauri iliyokuwa inaongoza kwa upotevu wa fedha ikifuatiwa na Halmashauri ya Kyela ambayo zilikuwa zimepigwa Sh. milioni 29.2 na Halmashauri ya Jiji la Mbeya Sh. milioni 14.1.

"Watendaji hao walikuwa wanakusanya fedha hizo kwenye maeneo yao, lakini walikuwa hawaziwasilishi halmashauri kama utaratibu unavyoelekeza, sasa baadhi walirejesha na wengine tunaendelea na taratibu za ufuatiliaji," alisema Matechi.

Alisema pamoja na kwamba baadhi ya watendaji hao walirejesha fedha hizo lakini bado taratibu za kiuchunguzi zinaendelea na kwamba kuna uwezekano wakafikishwa mahakamani kwa hatua zaidi za kisheria.

Aidha, Matechi, alisema katika Wilaya ya Chunya, Takukuru ilifuatilia na kuokoa Sh. milioni 10 za Amcos mbili za Lualaje na Muungano na kwamba fedha hizo zilikuwa zimetafunwa na viongozi wa Amcos hizo.

Alisema katika Wilaya ya Kyela taasisi hiyo ilifuatilia na kuokoa Sh. milioni 31.6 za Amcos nne za Ipinda, Makwale Fubu na Bateko na kwamba fedha hizo zilizokuwa zimetafunwa na viongozi zilirejeshwa kwenye akaunti za amcos. Vilevile alisema katika Wilaya ya Mbarali walifuatilia na kufanikiwa kuokoa Sh. milioni 9.02 za Amcos nne za Chimala, Mkungwa, Muungano na Uwarasu, na kwamba pia fedha hizo zilirejeshwa kwenye akaunti.

Pia alisema Sh. milioni 29.4 ziliokolewa na taasisi hiyo kutoka kwenye taasisi mbalimbali za umma na binafsi kupitia operesheni za uchunguzi.

Katika hatua nyingine, Matechi, alisema katika kipindi hicho cha miezi mitatu, Takukuru ilipokea taarifa 140 za tuhuma za rushwa kutoka katika taasisi mbalimbali za umma na binafsi.

Alisema kati ya taarifa hizo, 48 zilikuwa zinazihusu halmashauri, taarifa 21 zilikuwa zinawahusu wafanyabiashara (sekta binafsi), mashirika ya umma taarifa 12, vyama vya ushirika taarifa 12, Idara ya Elimu taarifa 11, mahakama taarifa 10, Idara ya Ardhi taarifa sita na Idara ya Afya taarifa mbili.

Taasisi zingine alizozitaja ni vyama vya siasa, Idara ya Maliasili, Idara ya Fedha na Madini ambazo kila moja ilikuwa na taarifa moja.

Pia alisema katika kipindi hicho kesi tano ambazo zilikuwa zimefunguliwa na Takukuru mahakamani zilitolewa maamuzi ambapo taasisi hiyo ilishinda kesi nne na kushindwa moja pekee.

# Msako wanasa mifuko ya plastiki maduka 16

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BARAZA la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (Nemc) kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, limefanya ukaguzi wa kushtukiza kwenye maduka ya nyama mkoani Mbeya na kuwanasa wamiliki 16 wakiendelea kuuza na kutumia mifuko ya plastiki iliyopigwa marufuku na serikali.

Operesheni hiyo ilifanyika mwishoni mwa wiki katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Mbeya ambapo maofisa wa Nemc Kanda ya Nyanda za Juu Kusini waliamua kupita mitaani kwa ajili ya kujiridhisha juu ya utekelezaji wa katazo hilo la serikali.

Meneja wa Nemc Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Arnord Mapinduzi, alisema operesheni hiyo pia ilifanyika katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

"Tutaendelea kufanya operesheni hizi za kushtukiza, wakati tunaendelea na zoezi wengine walipata taarifa na wakaificha lakini tuna taarifa zao na tutaendelea kushtukiza mpaka tujiridhishe kuwa matumizi ya mifuko hii yamekoma," alisema Mapinduzi.

Alisema wataendelea kufuatilia ili wajuwe mifuko hiyo inakozalishwa nchini ili udhibiti huo uanzie huko na kwamba mmiliki wa kiwanda yeyote atakayebainika anaendelea kuzalisha mifuko hiyo atachukuliwa pia hatua za kisheria.

Baadhi ya wauzaji wa maduka hayo waliziomba mamlaka za serikali zinazodhibiti mifuko na vifungashio kutoa elimu ya kuwasaidia kutambua mifuko isiyohitajika sambamba na kuwaletea vifungashio vinavyofaa.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Japhet Samson, alisema mifuko hiyo ambayo walikutwa nayo inauzwa hadharani kwa sababu hawajui kama haihitajiki na hivyo akaiomba serikali kuwaelimisha.

"Mlipotukataza kuuza mifuko ya rambo tuliacha, lakini hii mingine hatujui kama ni kosa na wanatuletea sio kwamba wanatuuzia kwa kificho, tunaomba muwe mnatuelimisha kwanza badala ya kutukamata na kutupa kesi.

Alisema baadhi ya bidhaa wanazouza zinahitaji kufungwa kwenye mifuko ambayo haiwezi kuvuja na kwamba ndio maana wamekuwa wakishawishika kuinunua mifuko hiyo laini.

la Sokomatola, Peter Mwalingo, aliwataka wafanyabiashara wenzake kuachana na uuzaji wa mifuko ambayo imepigwa marufuku ili kuepuka misuguano. Kwa mujibu wa sheria ya Nemc, wafanyabiashara hao baada ya kukamatwa na mifuko hiyo iliyopigwa marufuku, wametozwa faini za kati ya shilingi elfu hamsini na laki mbili kila mmoja.

# Uharibifu vyanzo wapunguza maji

**Na Innocent Ng'oko,** MBEYA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya-WSSA), imesema kuwa uharibifu wa vyanzo vya maji umesababisha kiwango cha uzalisha wa maji kwa siku kufikia lita 45,000,000 hadi 48,000,000 kwa siku ikilinganishwa na uwezo wa vyanzo hivyo kuzalisha lita 51,446,000 kwa siku.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Mkurugenzi wa Mamlaka hiyo ya Mbeya-WSSA, Mhandisi Ndele Mengo, na kubainisha kuwa uharibifu mkubwa wa vyanzo vya maji unaotokana na shughuli za kilimo katika maeneo ya vyanzo vya maji na ufugaji umechangia kwa kiasi kikubwa upungufu wa uzalishaji maji.

Alisema mahitaji halisi ya matumizi ya maji kwa wananchi kutoka ndani ya mamlaka hiyo ni lita 62,000,000 kwa siku na kuwa kuna jitihada endelevu za serikali kuendelea kuongeza vyanzo vingine vya maji kwa lengo la kukidhi mahitaji ya maji kwa wananchi.

Alisema licha ya kuwamo kwa jitihada binafsi za mamlaka hiyo na kwa kushirikiana na taasisi zingine ikiwapo ofisi ya bonde katika vyanzo 15 vya mamlaka hiyo kikiwapo chanzo kingine kipya cha 16 cha maji, lakini bado tatizo la uharibifu wa vyanzo ni kubwa ingawa kumekuwa na hatua mbalimbali zinazochukuliwa.

Ofisa wa Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Rukwa, Mkanjilwa Watson, ambaye alikuwa mratibu wa zoezi la upandaji miti katika chanzo cha maji cha Iyela alisema kuwa ofisi ya bonde ndiyo ina jukumu la kulinda na kuhifadhi vyanzo vya maji na kuwa moja ya majukumu ya kimukakati ni kupanda miti katika maeneo mbalimbali ya vyanzo vya maji.

Alisema katika chanzo cha Iyela wamefanikiwa kupanda miche ya miti 200 na kuwa ofisi hiyo ya Bonde la Ziwa Rukwa inakusudia kupanda miche 6000 hadi kufikia Aprili mwaka huu katika vyanzo mbalimbali vilivyopo ndani ya bonde hilo pamoja na kutoa elimu kwa wananchi juu ya umhimu wa kuhifadhi vyanzo vya maji.

Alisema ofisi ya bonde inasimamia shughuli zake katika mikoa ya Mbeya, Rukwa, Katavi na sehemu ndogo ya mikoa ya Tabora na Singida na kuwa katika maeneo mbalimbali kuna jumuiya za watumiaji maji ambao wanaendelea na majukumu ya upandaji miti kwa kushirikiana na wananchi na kulinda vyanzo vya maji.



HABARI DODOMA

# Serikali yaombwa kutoa kanuni, miongozo upimaji VVU vijana

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imeombwa kuweka kanuni na miongozo ya upimaji wa Virusi vya Ukimwi (VVU) kwa vijana kuanzia miaka 15 ili kwenda sambamba na marekebisho Sheria ya Ukimwi ya mwaka 2019.

Awali, katika Sheria ya Ukimwi ya Mwaka 2008 kabla ya kufanyiwa marekebisho iliweka umri wa miaka 18 wa kupima VVU bila ridhaa ya wazazi.

Ombi hilo lilitolewa jana jijini hapa na Mwakilishi wa vijana wanaoishi na VVU, Doreen Odemba alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya kuhitimisha kikao cha vijana kilichoandaliwa na Mtandao wa Watoto na Vijana Mwanza (MYCN).

Alisema katika kikao chao wamejadili kwa mapana kuhusu namna ya kupambana na na VVU na Ukimwi hapa nchini kwa kuanza kupima afya zao kutokana na sheria hiyo kufanyiwa marekebisho, hivyo kuruhusu vijana wenye umri wa kuanzia miaka 15 kupima bila ridhaa ya wazazi.

"Tumejadili namna ya kuhamasisha vijana wenzetu kushiriki kupima ili kujua afya zao lakini pamoja na sheria kufanyiwa marekebisho ili wapime afya zao, utekelezaji bado haujaanza kutokana na kutokuwapo na kanuni na miongozo mipya itakayosimamia watu wenye umri wa kuanzia miaka 15," alisema.

Alibainisha kuwa asilimia 43 ya watu 222 ambao ni sawa na vijana 96 kila siku wanaambukizwa VVU nchini hali inayoashiria vijana kuanzia miaka 15-24 wapo kwenye hatari kubwa ya kupata VVU.

"Kutokana na hali hii sisi watoto na vijana kutoka mikoa mbalimbali nchini tulishiriki kikamilifu katika mchakato wa kufanya marekebisho ya Sheria ya Ukimwi ya Mwaka 2008, tunashukuru serikali kwa kusikiliza kilio chetu hii ni hatua kubwa katika mapambano ya Ukimwi," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Baraza la Watoto nchini, Aidath Ismail, alisema serikali ikitoa kanuni na miongozo mipya vijana na na watoto wengi watajitokeza kupima afya zao na kuanza matibabu.

"Tunaomba pia serikali kutushirikisha kikamilifu sisi vijana na watoto katika mchakato wa kanuni na miongozo ili tuwe na kanuni na miongozo ambayo ni rafiki kwetu," alisema.

Alisisitiza kuwa wapo tayari kushiriki kikamilifu ili serikali itimize malengo ya kidunia ya 90-90-90 na lengo la nchi isiyokuwa na maambukizi ya VVU.



Diwani wa Kilimani jijini Dodoma, Neema Mwaluko, akitoa taarifa yake ya utekelezaji wa kazi na shughuli za maendeleo za kata hiyo, kwenye mkutano mkuu wa kata uliofanyika mwisho wa wiki. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Bunge laipa siri serikali namna ya kuvilinda viwanda vyake

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, imeshauri serikali kuzipandishia kodi baadhi ya bidhaa zinazoingia nchini ili kuvijengea uwezo viwanda vyake kuzalisha kulingana na mahitaji ya soko.

Ushauri huo ulitolewa jana na Makamu Mwenyekiti wa kamati hiyo, Kanali mstaafu, Masoud Ali Khamis, katika semina kwa wabunge iliyoandaliwa na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade).

Alisema ili kuingia kwenye Tanzania ya Viwanda lazima kuhakikisha bidhaa za Tanzania zinazozalishwa zinapata masoko ya uhakika.

"Kwa zile bidhaa ambazo viwanda vyetu vya ndani vina uwezo wa kuzalisha, tungesema tuzuie lakini tutafute mbinu ambayo itasaidia wenzetu wa hapa ndani kuuza bidhaa zao, tatizo kubwa la viwanda vyetu kuuza bidhaa zake kwa bei ya juu inatokana na 'production cost' ipo juu," alisema.

Alitolea mfano kwenye viwanda vya nondo na plastiki wanazalisha chini ya uwezo wa kiwanda kutokana na bidhaa kujaa kwenye maghala na hawana sehemu ya kuuza.

"Kiwanda kingekuwa kinafanya kazi muda wote na bidhaa zingepata wateja basi gharama za uzalishaji zingeshuka, sasa hivi kiwanda kinaweza kuzalisha kikajaza godauni, wafanyakazi anao na wanafanya kazi anaingiza kwenye gharama za uzalishaji, hili nalo ni tatizo," alisema.

Makamu Mwenyekiti huyo alisema kamati inajua kuna biashara zipo kwenye mikataba ya pamoja ya kodi za kikanda ambazo haiwezekani kuziingilia lakini zile ambazo serikali ina uwezo wa kuziweka kodi hapa ndani ya nchi wachukue hatua ili kunusuru viwanda vya ndani.

"Tunaweza kuzipandishia kodi bidhaa zinazoingia nchini ili kushindana na bidhaa zetu za ndani zinazozalishwa na kuondoa tatizo la kuzalisha kwa msimu na viwanda vyetu vizalishe kwa uwezo mkubwa," alisema.

Aliongeza kuwa: "Kiwanda cha marumaru maghala yamejaa na hawana sehemu ya kuweka na masoko hamna, kiwanda cha nondo pia hali ni hiyo, kwa mfano nondo mahitaji yake yote Tanzania ni tani 400,000, lakini viwanda vyetu vina uwezo wa kuzalisha tani milioni moja."

Alibainisha kuwa kwa sasa vinazalisha kwa msimu kutokana na mali ipo ndani ya viwanda na hawana sehemu ya kuuza.

Naye, Mkurugenzi Mkuu wa TanTrade, Edwin Rutegaruka, alielezea namna mamlaka hiyo inavyotekeleza majukumu yake ikiwamo wazalishaji kuzalisha bidhaa kulingana na mahitaji ya soko.

Alibainisha kuwa kuna intelijensia ya masoko ambapo mwaka huu wameweka mifumo mizuri kwa kuwa na maofisa masoko 35 kwa ajili ya kujua mahitaji ya soko.

"Kwenye biashara ya mipakani tunatakiwa kujipanga kujua washindani wetu ni kina nani na itasaidia wafanyabiashara kuzalisha kwa mahitaji ambayo yanatakiwa," alisema.

# Waziri ataka udhibiti utoroshaji wa madini

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

VYOMBO vya ulinzi na usalama nchini, vimeagizwa kuunda mfumo wa pamoja wa utendaji kazi ili kudhibiti masoko ya madini yasiwe kichaka kipya cha utoroshaji wa rasilimali hiyo.

Agizo hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki jijini hapa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Bunge, Sera, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu), Jenista Mhagama, katika semina maalum kwa vyombo hivyo juu ya usimamizi wa sekta ya madini nchini.

Alieleza kuwa vyombo hivyo vikiungana kwenye utendaji kazi itasaidia kwa kiasi kikubwa kuzuia ukwepaji kulipa tozo, kodi na utoroshaji madini kwenda nje ya nchi.

Alisema vyombo hivyo vikitengeneza mfumo wa mtandao mzuri unaozungumza lugha moja kutoka sehemu moja kwenda nyingine wawekezaji watazidi kuongezeka.

"Tunapaswa kuangalia ukamataji, ufunguaji wa mashtaka kiholela naomba kikao cha leo kujadili hilo na mlifanye kwa kufuata sheria bila ya kumuonea mtu, maana kuna ukamataji holela unafanywa wakati mwingine," alisema.

Alivitaka vyombo vya ulinzi na usalama kuwa mstari wa mbele kudhibiti masoko hayo yasiwe kichaka cha utoroshaji wa madini kwenda nje ya nchi.

Hata hivyo, alisema asilimia kubwa ya ulinzi unafanywa na wageni jambo ambalo linapaswa kuangaliwa kwa kina.

"Mnatakiwa kuangalia sifa zinazotakiwa ili mgeni anapoondoka nchini ujuzi uwe umerahisishwa kwa wenyeji sasa ukichukua wa hali ya chini hapo hutaweza kupata ujuzi wowote," alisema Mhagama.

Naye Waziri wa Madini, Dotto Biteko, alisema kutokana na kuboreshwa kwa sera na sheria ya usimamizi madini mwaka 2017, serikali inatarajia kukusanya Sh. bilioni 470 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ikilinganishwa na mwaka uliopita ambapo zilikusanywa Sh. bilioni 370.

Alisema usimamizi mzuri ukiendelea kufanywa na vyombo vya ulinzi na usalama sekta hiyo itaendelea kuwa bora kila siku.

"Nalala usingizi kutokana na ushirikiano ninaopewa na watu hivi sasa tumejitahidi kupunguza na kuwadhibiti watu wanaoiba madini na kuuza nje kiholela," alisema Biteko.

"Semina hii tunataka wote kwa pamoja kama serikali tuwe na kauli moja kama tunamkamata mtu anatorosha madini wote tuwe kitu kimoja na wote tunapaswa tuambiane hapa ili tuondoke na kauli moja," alisema.





# Shein amwagiwa sifa uongozi uliotukuka

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

VIONGOZI wa vyama vya siasa nchini wamempongeza Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, kwa kuleta maendeleo kwa wananchi wa Zanzibar na kudumisha amani na utulivu.

Viongozi hao ni kutoka vyama vya Ada-Tadea, TLP, NLD, DP, SAU, UPDP, AFP, ADC pamoja na NCCR-Mageuzi.

Akizungumza na waandishi wa habari kwa niaba ya viongozi wa vyama 10 vya upinzani, Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia Makini, Ameir Hassan Ameir, alisema katika kipindi cha miaka tisa Rais Shein amefanikiwa kuwaunganisha wapinzani, kuwajumuisha katika serikali, kuwapata nafasi za juu za uongozi.

Alisema hatua hiyo ni kupevuka kwa demokrasia ya vyama vingi nchini ambayo msingi wake mkubwa ni kuwajumuisha wananchi kushiriki katika ujenzi wa taifa.

"Tumefurahishwa na uongozi wa Dk. Shein sisi viongozi wa vyama vya siasa katika kipindi chake tumeshirikishwa na kujumuishwa katika serikali na kutoa mchango mkubwa katika ujenzi wa taifa letu," alisema Ameir.

Viongozi hao pia walimpongeza Dk. Shein kwa kuendelea kutekeleza fikra za Rais wa kwanza wa Zanzibar, hayati Abeid Karume za kuyaendeleza mapinduzi ya mwaka 1964 kwa kuendelea kutoa huduma muhimu za elimu na matibabu bure.

Alisema kitendo cha kufutwa kwa michango waliyokuwa wakitoa wazazi kwa ajili ya watoto wao ni matokeo halisi ya kutekeleza kwa vitendo fikra za mapinduzi katika sekta ya elimu.

"Tunashuhudia mabadiliko makubwa katika sekta ya elimu ambayo kuanzia msingi hadi sekondari ada zote zimefutwa huku shule za kisasa za ghorofa zikijengwa Unguja na Pemba," alisema Ameir.

Kadhalika, viongozi hao wamewataka wananchi kujitokeza kwa wingi kujiandikisha katika daftari la kudumu la wapigakura na kufanya uhakiki kwa ajili ya maandalizi ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Alisema malalamiko na shutuma zinazotolewa na wapinzani kutoka chama cha ACT-Wazalendo hayana ukweli kwa sababu ili uweze kuandikishwa kwenye daftari unatakiwa kufuata sifa na vigezo.

"Sisi viongozi wa vyama vya siasa tumeshuhudia kazi ya uandikishaji wa daftari la kudumu la wapigakura huko Pemba... kazi inaendelea vizuri na kwamba cha msingi ni kufuata vigezo na sifa," alisema Ameir.



Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia Makini, Ameir Hassan Ameir, akitoa tamko la viongozi wa vyama 10 vya siasa Tanzania la kupongeza mafanikio ya miaka tisa ya Uongozi wa Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, wakati akizungumza na wanahabari mjini Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Taasisi binafsi zahimizwa kuwasaidia watoto wa kike

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MLEZI wa Mtandao wa kuwasaidia watoto wa kike kupata maendeleo ya Elimu Zanzibar (FAWE), Shadia Karume, amezitaka jumuiya zisizo za kiserikali kuwasaidia watoto wa kike wanaoishi katika mazingira magumu ili kufikia malengo waliojiwekea.

Aliyasema hayo alipokuwa akifungua mkutano mkuu wa tisa wa jumuiya hiyo, katika ukumbi wa Shule ya Sekondari ya Haileselassie Mjini Zanzibar. Alisema kumpatia elimu mtoto wa kike ni msingi mzuri katika kulinda familia hivyo ni muhimu taasisi za kiraia kushirikiana na serikali kuwapatia elimu hasa masomo ya sayansi na teknolojia ili waweza kujitegemea na kujikwamua katika hali ngumu ya kimaisha. Alisema kuwa programu ya Tuseme ni muhimu sana kwa wanawake kwani inawafanya watoto wa kike kujiamini na kuwasaidia katika kujieleza kuwa yeye ni nani na anataka nini.

Shadia ambaye ni mke wa Rais mstaafu wa Zanzibar, alisema masomo ya sayansi yanawasaidia vijana kiuchumi na kijamii hivyo ameipongeza Jumuiya ya Fawe kwa kuanzisha programu ya Stemp kwa wanaume na wanawake.

Aidha, alizishauri taasisi za kiraia kuisaidia jumuiya hiyo na kuwataka vijana kujiunga na Fawe ili waweze kunufaika na elimu inayotolewa.

Mratibu wa Jumuiya ya FAWE, Hinda Abdallah Juma, alisema wameamua kuwashirikisha watoto wa kike zaidi kuliko wanaume kutokana na uwoga walionao.

Alisema Fawe imekuwa ikitoa ushauri kwa Wizara ya Elimu ili kuhakikisha kuwa mtoto wa kike anasaidiwa kupata elimu hata wale ambao uwezo wao wa kusoma ni mdogo kutokana na mazingira yasiyorafiki ya maisha.

Alisema wameanzisha mradi wa kufadhili watoto yatima na kuwasaidia watoto zaidi ya 200 wanaoishi katika mazingira magumu wanaume na wanawake visiwani Zanzibar.

Mwanafunzi Amina Omar Kitwana kutoka Klabu ya Tuseme alisema kuwa mafunzo aliyopatiwa yamemsaidia kuwa na uwelewa na kujiamini.

# 986 wagundulika vimelea malaria

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Afya, Harusi Said Suleiman, amesema baadhi ya wananchi wamegundulika na ugonjwa wa malaria na kwamba wamesharipotiwa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja na vituo vya afya vya Unguja na Pemba.

Suleiman aliyasema hayo wakati akitoa ripoti ya robo ya pili ya utekelezaji kwa Kamati ya Ustawi wa huduma za Jamii ya Baraza la Wawakilishi na kueleza kuwa wagonjwa hao walipatiwa matibabu stahiki.

Alisema katika kipindi ambacho uchunguzi uliofanyika na kugundulika vimelea vya malaria kwa wagonjwa waliofika hospitali na vituo vya afya.

Alisema kazi ya ufuatiliaji kwenye makazi kwa wagonjwa walionekana na vimelea hivyo ilifanyika na kwamba wagonjwa 986 sawa na asilimia 88 waligundulika na malaria.

Alisema asilimia 10 ya utekelezaji na ufuatiliaji wa wagonjwa kwenye makazi umeongezeka ukilinganisha na kipindi cha miezi mitatu iliyopita cha Julai hadi Septemba 2019 na kwamba mafanikio hayo yametokana na kuwapo kwa ushirikiano kati ya jamii na wahudumu wa afya.

Alisema katika hatua nyingine za kudhibiti kuenea kwa ugonjwa wa malaria Zanzibar, wizara kupitia Kitengo cha Kumaliza Malaria Zanzibar inafuatilia sehemu zinazoripotiwa kutoa wagonjwa kwa kufanya uchunguzi yakinifu katika mazalio ya mbu ili kuzuwia maambukizi mapya.

"Mikutano saba ya kuhamasisha jamii ilifanyika katika ngazi tofauti kwa Unguja na Pemba. Mada kuu zililenga juu ya zoezi endelevu la ugawaji chandarua pamoja na upatikanaji na utoaji wa elimu ya afya juu ya ongezeko la ugonjwa wa malaria katika shehia za Kisiwandui, Kisima-majongoo, Kikwajuni Bondeni na Kikwajuni juu katika wilaya ya Mjini," alisema Suleiman.

Alisema huduma za ugonjwa wa Ukimwi, homa ya ini, kifua kikuu na ukoma, ushauri nasaha na upimaji wa VVU ziliendelea katika vituo vyote vinavyotoa huduma hizo.

Alisema katika kipindi cha robo mwaka ya pili, watu 56,770 walichunguzwa VVU katika vituo vya ushauri nasaha na upimaji na kupatiwa huduma za mikoba.

Alisema kati yao, watu 373 sawa na asilimia 0.7 waligunduliwa na maambukizi ya ugonjwa wa Ukimwi, na kwamba hadi kufikia Desemba mwaka jana watu 6,710 wanaoishi na VVU walipatiwa huduma na tiba kwenye vituo vya afya 13.

Mwenyekiti wa Baraza la Wawakilishi, Mwanasha Khamis Juma akitoa majumuisho ya Kamati ya Ustawi ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar kwa Wizara ya Afya alisema kamati ilitekeleza majukumu yake kwa kutembelea katika vituo vya afya kwa Unguja na Pemba.

Alisema kwa upande wa Pemba alitembelea baadhi ya vitengo vya Wizara ya Afya pamoja na kupata maelezo ya miradi hiyo inavyoendelea na kubaini kwamba sehemu ya kuhifadhia dawa ni ndogo huku zingine zikikosa sehemu nzuri ya hifadhi.

# Wakurugenzi waagizwa bajeti ya mabaraza ardhi

**Na Mwandishi Wetu**, ILEJE

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angeline Mabula, amewataka wakurugenzi wa halmashauri nchini kutenga bajeti kwa ajili ya mabaraza ya ardhi ya kata na vijiji sambamba na kufuatilia tozo zinazotozwa na mabaraza hayo ili yafanye kazi kwa ufanisi.

Mabula alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki wilayani Ileje na Mbozi wakati akizungumza na viongozi pamoja na watendaji wa sekta ya ardhi akiwa katika ziara yake ya kukagua utendaji kazi wa sekta ya ardhi na ujenzi wa miradi inayofanywa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) mkoani Songwe.

Alisema, wakurugenzi wa halmashauri nchini hawatengi bajeti kwa ajili ya nabaraza ya ardhi ya kata na vijiji jambo linalosababisha wajumbe wake kujifanyia mambo wanavyotaka ikiwamo kuweka viwango tofauti vya tozo za kwenda viwandani.

Kwa mujibu wa Mabula, mabaraza ya ardhi ya kata na vijiji yanapaswa kusimamiwa na wakurugenzi wa halmashauri kwa kuyapatia kwa kuyatengea bajeti za kuendesha ofisi kama vile shajala sambamba na kujua yanayofanyika ikiwemo tozo zake ili kuepuka uonevu unaoweza kujitokeza kwa wananchi wanaoshtakiana.

"Katika mabaraza ya ardhi ya kata na vijiji watu wanalipa tozo kulingana na sura kama mtu kavaa tai basi anapigwa shilingi 50,000 jambo linalowaumiza wananchi," alisema Mabula.

Alizitaka ofisi za wakurugenzi wa halmashauri nchini kuyasimamia mabaraza hayo na kutoa semina kwa wajumbe wake na kuyapangia viwango vya tozo na kusisitiza kuwa hayo yasipofanyika kuna hatari wajumbe wake kufanya maamuzi kwa matakwa ya wenye uwezo.

Aliwataka wakurugenzi wa halmashauri kubadilika katika kuyasimamia mabaraza ya ardhi ya kata na vijiji na kubainisha kuwa mabaraza hayo yakifanya vizuri yatapunguza mrundikano wa kesi za ardhi zinazokwenda mabaraza ya ardhi ya nyumba ya wilaya. Awali Ofisa Mipango Miji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ileje, Mkoa wa Songwe, Dismas Ndinda, alimweleza Mabula kuwa halmashauri hiyo pamoja na kuwa mabaraza ya ardhi ya kata na vijiji 71, lakini haina baraza la ardhi la wilaya, jambo linalowafanya wananchi washindwa kupata suluhu kusafiri hadi Mbeya kupata huduma za baraza la ardhi la wilaya.

# Kesi za udhalilishaji kijinsia 111 zaripotiwa

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

JUMLA ya kesi 111 za udhalilishaji zimeripotiwa katika Ofisi ya Ustawi wa Jamii Wilaya ya Wete Mkoa wa Kaskazini Pemba, kuanzia Januari hadi Novemba mwaka 2019.

Kesi hizo ni za kubaka 41, kulawiti 13, kutorosha 35, shambulio la aibu 14, mimba nne na shambulio la kuumiza mwili nne.

Ofisa Ustawi wa Jamii Wilaya ya Wete, Haroub Suleiman Hemed, alisema, kati ya kesi hizo, 72 ziko kwenye upelelezi, 21 zipo mahakamani, kumi zimefungwa, nne zinasubiri kipimo cha vinasaba cha DNA na moja mtuhumiwa amekimbia.

"Kesi za kubaka 30 ziko kwenye upelelezi kati ya 41 zilizoripotiwa, kesi za kulawiti 10 ziko kwenye upelelezi, kutorosha 20 ziko kwenye upelelezi na shambulio la aibu 10 pia ziko kwenye upelelezi, sijui ni kipi kinachokwamisha hapa," alisema.

Ofisa huyo alisema changamoto zinazowakabili katika kukabiliana na kesi hizo ni rushwa ya muhali iliyotawala katika jamii pamoja na ukosefu wa kipimo cha vinasaba cha DNA.

"Kwa kweli rushwa muhali bado ni donda ndugu linalokwamisha kesi hizi zisimalize kwani jamii haiko tayari kutoa ushahidi na hii nahisi ndio inayosababisha pia upelelezi kukwama," alisema.

Alitaja mafanikio yaliyopatikana ni baadhi ya shehia kuunda kamati za maadili kwa ajili ya kusimamia tatizo la mporomoko wa maadili, ili kupunguza ama kuondosha kabisa udhalilishaji katika jamii iliyowazunguka pamoja na jamii kuwa na mwamko wa kuripoti kesi hizo kwenye vyombo vya sheria.

"Kuwapo kwa ushirikiano ya pamoja kwa taasisi za serikali na binafsi katika kusimamia na kufuatilia kesi za udhalilishaji, hii inasaidia sana kupambana," alieleza.

Ofisa Ustawi Hifadhi ya Mtoto, Nafhat Salim Yahya, alisema ili kukomesha udhalilishaji kwa wanawake na watoto, ni vyema jamii irejeshe malezi ya pamoja, kuchukuliwa hatua za haraka kwa mashauri yanayofikishwa mahakamani sambamba na kinababa kuache kuzitelekeza familia ili kuwakinga watoto kujiingiza katika vitendo viovu.

"Pia wazazi na jamii kwa ujumla ishirikiane na Jeshi la Polisi, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na mahakama kwa kuripoti kesi na kutoa ushahidi ili sheria ichukue mkondo wake, kwani bila ya ushahidi hakuna hatia.

Naye Mratibu wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (Tamwa) tawi la Pemba, Fat-hiya Mussa Said, aliwataka wanajamii kushirikiana katika kuhakikisha wanaondosha udhalilishaji.

"Tusiogope kusema ukweli hata kama utasusiwa ndani ya jamii usirudi nyuma... toa ushahidi ili haki itendeke, tusiwalinde wahalifu eti kwa sababu jamii itakutenga," alisema.



Mafundi kutoka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) wakilaza bomba eneo la Magari Saba kwa ajili ya kuongeza msukumo wa maji katika maeneo hayo. Zoezi hili litanufaisha mitaa ya Magari Saba, Takukuru Road, Madafu, Mnarani na Njiapanda ya Makonde wilayani Ubungo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Sababu za Katibu Mkuu NaCoNGO kuondolewa

**Na Gwamaka Alipipi**

BARAZA la Taifa la Mashirika yasiyo ya kiserikali (NaCoNGO), limemwondoa kwenye nafasi ya uongozi Katibu Mkuu wake, Ismail Suleiman, kutokana na tuhuma za matumizi mabaya ya madaraka, ubadhirifu wa fedha za baraza hilo.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, Mwenyekiti wa baraza hilo, Nicholaus Zacharia, alisema uamuzi huo umetokana na matokeo ya kamati ya uchunguzi ya baraza iliyoundwa Desemba 19, mwaka jana katika kikao cha dharura kilichokutana jijini Dodoma.

"Baraza la Taifa na mashirika yasiyo ya kiserikali katika kikao chake cha dharura kilichofanyika kimefanya maamuzi ya kumvua nafasi zote za uongozi katibu mkuu wa baraza kutokana na tuhuma mbalimbali zinazomkabiri," alisema Zacharia.

Alieleza kuwa pamoja na kutoa ushirikiano wakutosha kwa baraza, kamati ya uchunguzi pia imemkuta na hatia katibu huyo na makosa ya kuingizi kwenye baraza wajumbe watano ambao hawakuchaguliwa.

Zacharia alisema tuhuma zingine zinazomkabiri ni kufungua na kuendesha akaunti mbili za benki pasipo uelewa wala idhini ya kamati tendaji au baraza, pamoja na kumuweka mtia sahihi ambae sio kiongozi ndani ya baraza.

"Amekuwa akitoa vitisho kwa wawakilishi wa baraza waliokuwa wanadai uwazi na uwajibikiaji wa fedha, hivyo kutokana na uamuzi huo baraza limeteua Focus Magwesela kuwa kaimu katibu mkuu wa baraza kuanzia leo mpaka hapo itakapoamriwa," alisema Zacharia.

Aliongeza kuwa baraza limempatia siku tatu Suleiman kufika ofisini na kujieleza dhidi ya tuhuma hizo vinginevyo atafikishwa katika vyombo vya sheria.

Nipashe lilimtafuta Suleiman kufafanua tuhuma hizo ambaye alisema: "Sina taarifa zozote, ndiyo kwanza nasikia kutoka kwako, hizo tuhuma siyo za kweli, miaka mitatu yangu ya uongozi imeshaisha, na miaka mitatu ya uongozi wa baraza imeshaisha, hivyo uongozi mpya utakaoingia madarakani ndiyo unapaswa kuhoji hayo."

Suleimani aliongeza kuwa: "Kimsingi nimeongea na mwenyekiti wala hakuniambia chochote kuhusu hayo mambo, zaidi aliniambia kuna kikao kitafanyika mchana".

HABARI KIMATAIFA

# Polisi Iraq wavamia kambi za waandamanaji

**BAGHDAD, Iraq**

MAANDAMANO nchini Iraq yamekuwa yakiendelea kwa miezi kadhaa na kwamba vikosi vya usalama vimeendelea kutumia nguvu dhidi ya waandamanaji.

Watu wanne wameuawa katika maandamano nchini humo yanayoendelea kwa miezi kadhaa katika taifa hilo lililotumbukia katika mzozo wa kisiasa na vurugu.

Vikosi vya kulinda usalama vimechoma moto mahema ya waandamanaji kusini mwa Iraq.

Vikosi hivyo viliwatawanya waandamanaji kwa kutumia mabomu ya kutoa machozi pamoja na risasi za moto katika viwanja viwili vya mji mkuu wa Baghdad ikiwamo cha Tahrir na kusababisha kifo cha mtu mmoja, na wengine 44 kujeruhiwa.

Wakati huo huo, watu watatu waliuawa kwa kupigwa risasi katika mji wa kusini wa Nasiriyah baada makabiliano kati ya waandamanaji na vikosi vya usalama.

Maandamano hayo ya kuipinga serikali yamepata pigo baada ya kiongozi wa kidini Muqtada al-Sadr na wafuasi wake pamoja na wanamgambo wanaomuunga mkono kujitenga na maandamano hayo.

Al-Sadr ameamua kutounga mkono maandamano hayo baada ya maelfu ya wafuasi wake kufanya maandamano tofauti Ijumaa mjini Baghdad ya kutaka wanajeshi wa Marekani kuondoka nchini humo, ambayo waandamanaji wengi wanaoipinga serikali hawakushiriki.

Kufuatia uamuzi huo wa al-Sadr mwishoni mwa wiki, Jeshi la Polisi kikosi cha kutuliza ghasia kilichoma moto kambi za waandamanji katika uwanja wa mji wa Basra kusini mwa nchi hiyo.

Katika uwanja wa Tahrir, ambako ndiko kitovu cha vuguvugu hilo la maandamano ya kuipinga serikali mjini Baghdad, waandamanaji wanasema wanahofia kitakachofuatia baadaye.

Waandamanaji hao wamekuwa wakiikosoa serikali kutokana na vitendo vya ufisadi, kiwango kikubwa cha ukosefu wa ajira pamoja na ushawaishi wa Iran ndani ya siasa za Iraq.

Wanaharakati wa haki za binadamu wanasema kitendo cha Jeshi la Polisi kutumia nguvu kubwa imesababisha vifo vya waandamanaji wapatao 500 tangu Oktoba mosi mwaka jana.

"(Kauli ya al-Sadr) imesafisha njia kwa serikali kuukandamiza zaidi upinzani wa waandamanaji," amesema Hussein Ali, mwandamanaji mwenye umri wa miaka 35. Wengine wanasema wataendelea kupambana na wanayajenga tena mahema yao yaliyochomwa moto.

**DW**

# Wanaougua virusi vya corona wafikia 2,000

**BEIJING, China**

MAOFISA wa China wamesema kuwa virusi vipya vya corona vimeshasambaa kwa watu takribani 2,000 na kwamba dalili zake zinakuwa bado hazijaanza kujitokeza kwa mtu aliyeathirika na kufanya iwe vigumu kuudhibiti.

Hadi sasa watu 56 wamefariki kutokana na kuugua kwa ugonjwa huo. Waziri wa Afya wa China, Ma Xiaowei aliwaambia wanahabari kwamba uwezo wa virusi hivyo kusambaa ni mkubwa na unaonekana kuongezeka.

Baadhi ya miji ya China imepiga marufuku kwa wananchi wake kusafiri kutoka sehemu moja kwenda nyingine.

Mji wa Wuhan uliopo Hubei, ambao ndiyo chanzo cha mlipuko wa virusi hivyo kwa sasa umefungiwa kabisa na kwamba hakuna raia anayetoka wala kuingia.

Ma Xiaowei alisema maambukizi ya virusi hivyo katika mji huo yako katika kiwango ambacho ni vigumu kudhibitika," amesema Ma Xiaowei.

Maofisa nchini China wameahidi kuongeza juhudi mara dufu za kudhibiti virusi hivyo na kutangaza kwamba biashara ya kuuza wanyama wa porini itapigwa marufuku.

Virusi hivyo vinaaminika kwamba vimetokana na wanyama na vimesambaa kwa haraka kati ya wanadamu.

Maofisa hao walieleza kuwa wakati wa kuatamia mayai mtu anapokuwa ameambukizwa virusi lakini hakuna dalili zozote zinazojitokeza na kwamba kati ya siku 1 hadi 14, ndipo dalili zinaanza kuonekana.

Wameeleza kuwa bila ya kujitokeza kwa dalili mtu hawezi kufahamu ikiwa ameambukizwa virusi vya corona lakini pia vinaweza kusambaa kwa wakati huo huo.

Kiongozi wa Hong Kong, Carrie Lam, alitangaza hali ya dharura kuhusu virusi vya corona katika Jiji hilo na serikali yake imetangaza kufungwa shughuli za usafiri, shule na vyuo vikuu.

Matukio matano ya maambukizi ya virusi vya corona vimeripotiwa katika Jiji la Hong Kong na watu zaidi ya 122 wanadhaniwa kuwa na virusi hivyo.

Shughuli mbalimbali zimefungwa wakati ambapo raia wengi wa Hong Kong wanasherehekea mwaka mpya huku kukiwa na mivutano inayoendelea baada ya miezi saba ya maandamano dhidi ya serikali.

Ndege na safari za reli ya mwendokasi kati ya Hong Kong na Wuhan zimesimamishwa, wakati ambao shule na vyuo vikuu vitaendelea kufungwa hadi Februari 17.

Serikali ya China ilitangaza kwamba mji wa Wuhan utajengewa hospitali yenye vitanda 1,000 ili kukabiliana na janga hilo, ambayo ujenzi wake utakamilika Februari 3, mwaka huu.

Ujenzi huo ni sawa na ujenzi wa hospitali iliyojengwa kwa ajili ya kupambana na ugonjwa wa SARS iliyojengwa ndani ya siku sita mjini Beijing mnamo mwaka 2003 wakati mlipuko wa ugonjwa huo ulipozuka.

***BBC***



Wananchi nchini China wakiwa mitaani wamejifunika uso kujikinga na kirusi cha corona katikati ya mji wa Wuhan. **PICHA: AP**

# Mali yawaita viongozi wa makundi ya kigaidi

**BAMAKO, Mali**

MWAKILISHI Mkuu wa Rais Ibrahim Boubacar Keïta katika eneo la Kati, Dioncounda Traoré, amesema kwamba amewaagiza wajumbe wa serikali kuwasiliana na makundi mawili ya kigaidi.

Traoré aliwaagiza maofisa kadhaa ambao walipendekezwa kuwa wasimamizi wa mazungumzo na makundi ya kigaidi.

Wiki chache zilizopita mwakilishi mkuu wa Rais Keita aliamua, kuwafuta kazi wajumbe wapya. Alisema yuko tayari kuwaagiza wengine ikiwa itahitajika.

Mchakato wa kuwaita viongozi wa makundi ya kigaidi nchini humo uliwekwa hadharani mwishoni mwa wiki na ofisi ya rais wa Mali.

Lengo ni kuanzisha mawasiliano ya moja kwa moja ni kuona kama mazungumzo yanawezekana, hasa na viongozi wawili; Iyad Ag Ghali na Amadou Koufa.

Traoré anamjua Iyad Ag Ghali, kutoka GSIM, kundi linalounga mkono dini ya Kiislamu. Alikuwa katika serikali mwanzoni mwa miaka ya 1990, wakati Tuareg walipoanzisha uasi chini ya uongozi wa Iyad Ag Ghali. Hata hivyo, wawili hao hawajaonana kwa karibu muongo mmoja.

Kiongozi wa pili wa kundi la waasi ambaye Bamako inataka kufanya naye mazungumzo ni Amadou Koufa, kiongozi wa katiba ya Macina, kundi ambalo linaendelea kuhatarisha usalama nchini Mali tangu mwaka 2015.

Kwa sasa, hakuna mawasiliano yoyote ambayo yamefanywa ili kukutana kwa mazungumzo na Abu Walid al-Sahraoui, mkuu wa kundi la Islamic State katika Grand Sahara. Awali Traoré alikuwa mstari wa mbele kupinga mazungumzo yoyote na makundi ya kigaidi nchini Mali.

***RFI***

# Maambukizi mapya ya ugonjwa ukoma yashuka

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

SERIKALI imesema viwango vya maambukizi mapya ya ugonjwa wa ukoma vimepungua kutoka wagonjwa 43 kati ya watu 1,000,000 mwaka 2014 hadi kufikia wagonjwa 26 mwaka 2019.

Aidha, idadi ya watoto wanaougua ukoma imepungua kwa asilimia 41, kati ya watoto 90 mwaka 2014, hadi 53 mwaka 2019.

Hayo yalibainishwa juzi na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, wakati akitoa tamko la Siku ya Ukoma Duniani alipotembelea makazi ya waathirika wa ugonjwa huo yaliyopo katika eneo la Samalia Hombolo Bwawani jijini Dodoma.

Ummy alisema kupungua huko kwa maambukizo kumetokana na jitihada kubwa za serikali ya awamu ya tano.

"Kutokana na juhudi za serikali, viwango hivyo vya utokomezaji vimeendelea kuboreshwa na kushusha idadi ya waathirika wa ukoma kutoka wagonjwa 4.3 kati ya watu 100,000 mnamo mwaka 2014 na kufikia wagonjwa 3 kati ya watu 100,000 mwaka 2019," alisema Mwalimu.

Katika hatua nyingine, alisema Tanzania imefikia viwango vya kidunia vya utokomezaji wa ukoma vya kuwa na chini ya wagonjwa 10, kati ya watu 100,000 mnamo mwaka 2006.

"Siku ya Ukoma Duniani inatupa fursa ya kutathmini mwelekeo wa jitihada zetu nchini na zile za kimataifa katika kupambana na ugonjwa huu," alisema.

Pia alikiri kuwa waathirika wengi wa ukoma wananyanyapaliwa na kubaguliwa katika maeneo mengi nchini.

Alisema, kutokana na hali hiyo takriban asilimia 50 ya wagonjwa wa ukoma hupatwa na ugonjwa wa sonona kutokana na kuishi maisha ya huzuni na wasiwasi mkubwa katika jamii zao.

Alifafanua kuwa unyanyapaa na chuki dhidi ya waathirika wa ukoma, huwafanya wajifiche na kushindwa kujitokeza katika vituo vya huduma za afya kwa ajili ya matibabu na hivyo kusababisha kupata ulemavu wa kudumu.

Alisema serikali, wadau na wananchi wote wanatakiwa kuungana na kuongeza nguvu katika kupinga matukio yote ya unyanyapaa.

Kuhusu utokomezaji kwa Tanzania, Waziri huyo alisema hadi kufikia mwaka 2019, mikoa yote isipokuwa Lindi ilikuwa tayari imefikia kiwango cha utokomezaji.

Aliongeza kuwa zipo halmashauri 16, ambazo bado hazijafikia viwango hivyo ambazo ni Lindi, Liwale, Nachingwea, Ruangwa, Masasi, Nanyumbu, Morogoro, Mvomero, Mpanda, Nkasi.

Zingine ni Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, Manispaa ya Kigoma, Kibaha, Mkinga na Tunduru ambazo amezitaka kuongeza kasi ya kutokomeza ugonjwa huo.

Aliitaka mikoa na halmashauri zihakikishe zinatenga bajeti katika mipango yao ili kuendesha kampeni za uhamasishaji, uelimishaji, na uibuaji wa wagonjwa wapya.



Baadhi ya wanafunzi wa kidato cha kwanza wa sekondari mpya ya Busambara katika kijiji cha Kwikuba, Musoma Vijijini mkoani Mara wakiwa darasani. Shule hiyo ilianza kuchukua wanafunzi Januari 14 mwaka huu **.PICHA:**

# RC awapa neno waajiri magonjwa, ajali kazini

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, amewataka waajiri mkoani humo kuhakikisha wanatokomeza ajali na magonjwa sehemu za kazi na kuitekeleza kampeni ya 'Vision Zero'.

Akizungumza katika hafla ya kuzindua kampeni hiyo mkoani Mwanza ambayo ni mahususi kutokomeza ajali na magonjwa sehemu za kazi, Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Phillip Nyimbi, aliyemwakilisha mkuu wa mkoa, alisema endapo waajiri watapata mafunzo ya uhakika kuhusu kampeni hiyo, ni dhahiri uzalishaji utaongezeka na kuleta tija kwa serikali na wananchi.

"Kupitia kampeni na mafunzo haya, Wakala wa Afya na Usalama Mahali pa Kazi (Osha) mmenirahisishia sana kazi kwani hata nisipopita mara kwa mara katika maeneo ya kazi kukagua, naamini mafunzo haya yataenda kusafisha vitu vichache vilivyobakia.

"Pia yataenda kujazia pale palipokuwa pamepwaya na naamini kuwa mafunzo haya yataenda kuleta tija pia kwa watumishi na wafanyakazi katika maeneo mbalimbali ya kazi," alisifu.

Mkurugenzi wa Mafunzo, Utafiti na Takwimu wa Osha, Joshua Matiko, alisema kupitia kampeni hiyo, wataendelea kuwaelimisha waajiri ili kuona umuhimu wa kuwekeza katika afya na usalama wa wafanyakazi wao.

"Kupitia kampeni hii tuliyoianzisha, tunataka kuwadhihirishia waajiri kwamba wakiwekeza katika masuala ya usalama na afya kwa wafanyakazi, hawatapata hasara bali itawaletea tija zaidi," alisema.

Mwenyekiti wa Chemba ya Biashara, Viwanda na Kilimo (TCCIA) Mkoa wa Mwanza, Dk. Elibariki Mmari, alisema wanachama wa TCCIA wameipokea kampeni hiyo na wameshiriki katika mafunzo ili kutambua wajibu wao katika utekelezaji wa kampeni hiyo.

"Tumefurahi baada ya kuona Osha na WCF kufika mkoani kwetu kutoa semina kuhusu kampeni ya Vision Zero, mkakati huo ni wa kutaka kuhakikisha hali ya usalama na afya katika maeneo yetu ya kazi, iwe ni kwenye viwanda, hospitali na maeneo mengine ya kazi, vihatarishi vyake vinapungua hadi kufikia sifuri," alisema.

Kaimu Meneja wa Osha Kanda ya Ziwa, Mjawa Mohamed, alisema wataendelea kutoa elimu na kufanya uhamasishaji zaidi katika mikoa yote ya Kanda ya Ziwa ili kufikia lengo la kampeni hiyo ambalo ni kutokomeza ajali na magonjwa katika maeneo yote ya kazi.

Alisema dhana ya Vision Zero ilibuniwa na Shirikisho la Mashirika ya Hifadhi za Jamii Duniani (ISSA) na inatekelezwa na nchi mbalimbali duniani kwa namna fofauti kutegemeana na mazingira ya nchi husika.

# Ujenzi chuo Veta bado kiza Igunga

INATOKA UK. 3

awamu kulingana na upatikanaji wa fedha," alisema.

Udadisi wa Nipashe ulihamia kwa Mkuu wa Wilaya ya Igunga, John Mwaipopo, ambaye alisema mradi huo utatekelezwa baada ya fedha kupatikana.

"Bado hatujapata fedha, fedha ikipatikana tutajenga chuo," Mwaipopo alisema.

Hata hivyo, alipoulizwa kuhusu kuibuka kwa mvutano wa viongozi ndani ya wilaya hiyo kuhusu eneo ambako chuo cha Veta kitajengwa, Mwaipopo hakuwa tayari kuweka wazi eneo hilo, akieleza kuwa Igunga ina maeneo mengi kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

"Igunga ina maeneo mengi ndiyo maana ninakaribisha wawekezaji. Msalimie Gulamali," Mwaipopo alisema, akimaanisha salamu zake zifike kwa Mbunge wa Manonga, Seif Gulamali, ambaye amekuwa mstari wa mbele kufuatilia suala hilo.

Nipashe pia ilimtafuta mbunge huyo jana, ambaye alisema anasikitika kuona uongozi wa halmashauri unashindwa kutekeleza maagizo ya Wizara ya Elimu iliyotaka wapeleke wataalamu ili eneo hilo lipimwe na hati yake kukabidhiwa kwa Veta makao makuu.

"Hii ni ahadi ya Makamu wa Rais. Kinachotakiwa kwa sasa ni halmashauri kutuma wataalamu kwenda Choma kupima eneo lililokabidhiwa na World Vision ili Veta makao makuu wapatiwe hati na kuanza ujenzi, sisi viongozi tunapaswa kuweka kando maslahi yetu ili wananchi wapate huduma," alisema.

Katika mwaka huu wa fedha, serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, imetenga Sh. bilioni 40 kwa ajili ya ujenzi wa vyuo 25 vya ufundi stadi katika wilaya mbalimbali nchini.

Akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya Urambo Julai 9 mwaka jana, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, alisema ujenzi wa vyuo hivyo ni utekelezaji wa mkakati wa serikali kuhakikisha vijana wengi zaidi wanapata fursa za mafunzo ya ufundi stadi.

Prof. Ndalichako alisema vyuo hivyo vinatarajiwa kujengwa katika Wilaya za Chunya, Kilindi, Korogwe, Ukerewe, Igunga, Pangani, Kishapu, Rufiji, Uyui, Kwimba, Bahi, Mafia, Longido, Mkinga, Uvinza, Ikungi, Iringa vijijini, Lushoto, Mbarali, Monduli, Buhigwe, Ulanga, Masasi, Butiama na Chemba.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MKOPO WA HARAKA KUTOKA ENTERPRISE FINANCE LIMITD (EFL).** Kwa mahitaji kama kulipa ada ya shule, kodi, kuboresha biashara, kumalizia tenda etc. Kwa maelezo zaidi **piga 0758 112 332. Karibu EFL**.

**TANZANIA RESEARCH AND CAREER DEVELOPMENT INSITUTE:** Inatangaza mhula mpya wa masomo Certificate na Diploma za kilimo na maendeleo ya jamii.maelezo zaidi tembelea tovuti yetu www.tracdi.ac.tz Simu**:0714404491/0746995144**


*NIPASHE NI JIBU LAKO*

NJOO UTANGAZE NASI

BIDHAA YAKO


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;21/2020**

Ombi la RAJAB RAJAB KUSENGE Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu TABIA SAID KUSENGE.

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 21/02/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 23/01/2020.

Sahihi ya Hakimu
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

215599502

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI KISUTU**
**DAR ES SALAAM**
**SHAURI LA MADAI NO. 202 YA MWAKA 2019**
**FAST JET.............................MDAI**
**DHIDI YA**
**AIR FORCE ONE..................MDAIWA**

**KWA: MONICA DE MELLO, FLAVIANA, MARIAM SAROGA, SANDRA, ENNA LUTENGANO, HALIMA RAJABU**

**KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa mdai ameleta madai yake ambayo maelezo ya mdai yameelezwa katika nakala ya madai ambazo zinaweza kupatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo mnahitajiwa kuhudhuria katika Mahakama hii binafsi au kwa Wakili au mwakilishi ambaye anaruhusiwa, siku ya tarehe 30.1.2020 saa 7 mchana.

**ANGALIA:** Kama hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikithibitisha kama mmepokea kuitwa shaurini, itaweza kutoa hukumu kuwa mmeshindwa.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 12 Mwezi wa 12, 2019.

HAKIMU MKAZI MKUU
KISUTU -DAR ES SALAAM

115599002

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**ELIREHEMA OPHORO MACHA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya Suzuki yenye namba za usajili **T 427 DFY.** Chassis No. **DC51T553057,** Engine No. **F6AEAA3057.**Yeyote atakaye iona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi **DOD/DOD/RB/24235/2020.**

115600602


*Kwa Habari Motomoto*

*usikose Gazeti lako*

*la Nipashe kila siku*

*Tupigie 0782253676*

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi*

*Kwa Bei Poa*

*Tupigie 0782253676*

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku


Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# KOCHA BARCA AFUNGUKA BAADA YA KUPATA KIPIGO



**BARCELONA, Hispania**

BARCELONA haikutumia mbinu na mawasiliano yake yanayotakiwa kufanyiwa kazi, Kocha Quique Setien amebainisha hayo baada ya kufungwa na Valencia, juzi Jumamosi.

Setien alipoteza mchezo wake wa kwanza tangu achukue mikoba ya Ernesto Valverde kama kocha wa Barca Januari 13, mwaka huu baada ya kufungwa 2-0 pale kwenye dimba la Mestalla, shukrani kwa mabao mawili ya Maxi Gomez; la kwanza likimgonga Jordi Alba na kujaa wavuni.

Blaugrana hao licha ya kushambulia muda mwingi wa mchezo huo, Setien anaona kwamba timu yake haikucheza vizuri.

Kocha huyo wa zamani wa Real Betis aliachwa akiangalia namna ya kukimarisha kikosi hicho, akisema kwamba wachezaji hawakuelewa maelekezo yake.

"Bado hawafuati maelekezo yangu vizuri au pengine hatuwaelekezi vizuri," alisema Setien. "Hakuna anayependa kuona kile kilichotokea leo (juzi).

"Valencia walitubana, walicheza vizuri. Kwa upande wangu kuna vitu tunatakiwa kuvisahihisha. Tulicheza pasi nyingi zisizokuwa na maana. Hatuwezi kufanya hivi.

"Katika kipindi cha kwanza, hatukucheza vizuri. Kitu cha muhimu ni kwamba tulikwenda mapumziko tukiwa 0-0.

"Kipindi cha pili, timu iliimarika kwa kiasi fulani na tuliweza kuwa mchezoni, lakini hii haitoshi kwa upande wetu."

## DI MARIA: NITAMALIZIA SOKA LANGU PSG

**PARIS, Ufaransa**

ANGEL Di Maria anataka kumaliza kipindi chake cha uchezaji barani Ulaya akiwa pale Paris Saint-Germain, na amemsifia Thomas Tuchel kuwa chachu ya kile anachoamini kuwa ni msimu wake bora.

Di Maria amekuwa kwenye kiwango cha kuvutia msimu huu 2019-20, akifunga mabao 10 katika mashindano yote na kutoa pasi za mwisho nane katika Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1.

Inaweza kuwa rahisi na tofauti kwa Di Maria, ambaye amethibitisha kwamba alikuwa anataka kuondoka PSG mwaka 2018 kabla ya mazungumzo ya Tuchel ambaye alimshawishi kubakia hapo Parc des Princes.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 mkataba wake unamalizika mwaka 2021 na ingawa mazungumzo kuhusu mkataba wake mpya bado hajaanza, ana matumaini ya kumaliza kipindi chake cha uchezaji soka barani Ulaya akiwa na PSG kabla ya kuwa na uwezekano wa kurudi Argentina kumalizia kabisa siku chake za uchezaji soka.

"Sijazungumza na yoyote kwenye klabu, kuhusu mkataba mpya," amesema Di Maria.

"Sifikiri kuhusu hilo kwa sasa, bado nina mwaka mmoja. Ninajiamini. Naendelea kufanya kazi.

"Nilisema kwamba, nataka kumaliza kipindi changu cha kucheza Ulaya nikiwa hapa PSG na nina furaha kubwa kuwa hapa. Halafu pengine nitaangalia kama nitataka kucheza tena Argentina."

Di Maria aliongeza kwamba, Tuchel ni mmoja wa makocha ambao wana imani naye kubwa mno.

"Ameonyesha kuniamini na kunipa ujasiri. Alizungumza na mimi mjini Barcelona kabla ya Kombe la Dunia mwaka 2018," alisema.

"Alijaribu kunishawishi mimi kubakia PSG na nafikiri ndio sababu ya mimi kubakia hapa. Familia yangu na mimi tunajisikia vizuri hapa."



# ATLETICO MADRID NI MAISHA YANGU – SIMEONE



**MADRID, Hispania**

DIEGO Simeone amesema atairudisha Atletico Madrid kwenye nafasi yake nzuri, huku akielezea kwa namna gani klabu hiyo ilivyoyabeba maisha yake.

Simeone amekuwa na msimu mgumu pale kwenye dimba la Wanda Metropolitano, huku Atletico ikipoteza mechi zake tatu zilizopita kwenye mashindano yote na jana Jumapili ilikuwa ikicheza kwenye mchezo wa LaLiga dhidi ya Leganes.

Real Madrid waliwafunga wapinzani wao hao wa jiji moja kwa mikwaju ya penalti katika fainali ya Supercopa de Espana, lakini Atletico wakajikuta kwenye wakati mgumu dhidi ya Eibar kwenye LaLiga na dhidi ya Cultural Leonesa kwenye raundi ya tatu ya Copa del Rey.

Simeone amesisitiza kuhusu kuwa na kiwango kibovu kwa timu yake na kusema timu hiyo itarudi kwenye ubora wake.

"Mara zote nimekuwa nafikiria kuhusu timu yangu," alisema kabla ya mchezo huo akiwaambia waandishi wa habari.

"Sifikirii kuhusu nyakati ambazo napoteza mchezo au nashinda, lakini mara zote naiangalia timu yangu.

"Wakati mwingine siwezi kulala nikifikiria kuhusu kikosi cha kukipanga. Kwa uhakika Atletico ni maisha yangu, watu wanaonijua mimi wanalijua hilo."

# HABARI MICHEZO



## FLICK ASIFIA KIWANGO BAYERN IKIIKARIBIA LEIPZIG

**MUNICH, Ujerumani**

HANSI Flick amebainisha kuwa na "siku yenye mafanikio makubwa" baada ya Bayern Munich kuifumua Schalke na kuwakaribia vinara wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, RB Leipzig, juzi Jumamosi.

Bayern walishinda mabao 5-0 nyumbani na sasa wamepitwa pointi moja na Leipzig, ambao walifungwa 2-0 na Eintracht Frankfurt.

Kocha mkuu Flick alifurahishwa na ushindi huo wakati kikosi chake kikiifumua Schalke na sasa kina nafasi ya kuwakaribia vinara wa Ligi Kuu.

Robert Lewandowski, Thomas Muller, Leon Goretzka, Thiago Alcantara na Serge Gnabry kila mmoja alifunga bao kwenye mchezo huo.

"Ilikuwa nzuri sana," alisema Flick. "Schalke walionesha kiwango cha juu kwenye mchezo wa kwanza kwa mwaka 2020 dhidi ya Gladbach. Lakini tulicheza hapa nyumbani na tulitaka kucheza mchezo wetu, kwa kutumia falsafa yetu.

"Tulitaka kuwasumbua wapinzani wetu, tuliweka presha kubwa kwao na kwa nguvu kubwa. Tulifanya vizuri sana, hasa katika kipindi cha kwanza.

"Ilikuwa muhimu kwamba tulipata pointi tatu. Hii itatufanya tujiamini zaidi. Ubora wa kikosi ni mzuri zaidi, na kama timu itaweza kuwa kwenye kiwango kama cha leo (juzi) nitakuwa nimeridhishwa mno."

## LAMPARD ataka Chelsea ikamilishe usajili

**LONDON, England**

FRANK Lampard amesema Chelsea lazima "ipate mtu sahihi" kwenye soko la uhamisho baada ya kupata ushindi mwembamba wa Kombe la FA dhidi ya Hull City.

Ushindi huo wa mabao 2-1 kwenye Uwanja wa KCOM Jumamosi umeifanya Chelsea kufuzu raundi ya tano, lakini walikabiliwa na wakati mgumu dhidi ya timu hiyo ya daraja la chini.

Huku Tammy Abraham akiwa majeruhi na mshambuliaji, Olivier Giroud akiwa anaangalia uwezekano wa kuondoka kabla ya dirisha dogo la usajili kufungwa, ni wazi kwamba Chelsea lazima ijiimarishe.

Lampard anajua wapi Chelsea wanapokosea, ingawa aliezea kuridhishwa na kiwango cha Michy Batshuayi alichokionyesha dhidi ya Hull.

Chelsea walifungiwa kufanya usajili wakati Lampard akipewa timu hiyo, lakini sasa wapo huru kusajili wachezaji wapya, huku muda wa usajili wenyewe ukikaribia kufungwa mwishoni mwa Januari hii.

"Kazi yangu ni kupendekeza na kufanya kazi kila siku kwenye uwanja wa mazoezi," alisema Lampard akiiambia BT Sport.

"Sehemu nyingine ya klabu ni namna gani tunakwenda mbele kwa kununua wachezaji wapya, kwani tulikuwa hatuna uwezo huo kipindi cha majira ya joto kilichopita."

***



## MOURINHO HAFURAHII UHAMISHO WA ERIKSEN

**LONDON, England**

JOSE Mourinho hana furaha na kupatiwa ufumbuzi kwa majaliwa ya Christian Eriksen, lakini hailaumu Tottenham kwa hali ilivyo, huku Inter Milan ikiendelea kumshawishi mchezaji huyo kiungo.

Huku zikiwa zimebakia siku tano kufungwa kwa dirisha dogo la usajili la Januari hii, Eriksen alisafiri na Tottenham lakini hakuwa sehemu ya kikosi kilichocheza dhidi ya Southampton kwenye mchezo wa raundi ya nne wa Kombe la FA, juzi Jumamosi, ambao ulimalizika kwa sare ya kufungana 1-1.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Denmark anatarajiwa kufanyiwa vipimo vya afya leo Jumatatu pale Inter, huku Spurs ikiripotiwa kukubali ofa ya ada ya uhamisho ya euro milioni 15 na nyongeza ya euro milioni 5 akiwa anatarajia kusaini miaka minne.

"Unaweza kusoma kile unachotaka kusoma (kuhusu Eriksen kuondoka) - nataka kusema hali hii haikutakiwa kutokea Januari 25 (juzi) hii, ambapo mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu.

"Na hilo sio kosa la Tottenham kwamba hadi Januari 25 bado tupo kwenye hali hii.

"Kitu pekee ninachoweza kusema ni Eriksen, tangu nilipowasili hapa, ameonyesha uungwana mzuri kabisa kwangu mimi na kwa timu.

"Tottenham ndio ya mwisho kulaumiwa kwa hali hii, lakini hadi Januari 25 hali kama hii sio nzuri sana kwa timu."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# SOLSKJAER AFUNGUKA HAOGOPI KUFUKUZWA

Kocha huyo aeleza kila anachofanya ndani ya klabu hiyo kina baraka kutoka kwa mabosi...

**MANCHESTER, England**

OLE Gunnar Solskjaer amesisitiza hana hofu na kazi yake pale Manchester United, lakini amekubali kuwa anahitaji kuona matokeo mazuri yanapatikana ndani ya kikosi hicho.

Solskjaer amekalia kuti kavu pale kwenye dimba la Old Trafford, huku United ikiwa imeshinda mechi mbili tu kati ya saba zilizopita kabla ya jana Jumapili kuivaa Tranmere Rovers kwenye mchezo wa Kombe la FA.

Lakini raia huyo wa Norway amesema hana hofu kuhusu nafasi yake hiyo, ingawa anajua kwamba United, ambao wapo nafasi ya tano katika msimamo wa Ligi Kuu England, na wanatakiwa kuimarisha kiwango chao.

"Tulipokaa chini wote tulikubaliana, klabu na mimi, kwamba utamaduni unatakiwa kubadilika," alisema Solskjaer akiviambia vyombo vya habari vya Uingereza.

"Sio kwamba nimekuwa nafanya bila ruhusa, kwa sababu tumekubaliana kufanya vitu ambavyo tumesaini mkataba na tumekubaliana kwenye mipango. Sihofii nafasi yangu, kwa sababu naendelea kufanya kile tulichokubaliana.

"Bila shaka unajua tunahitaji matokeo na kuonyesha kwamba unafanya jambo sahihi na sitatumia fedha nyingi kwa mtu kuja hapa kama siyo mtu sahihi kwa klabu yetu."

United imekuwa kwenye presha kubwa kwa matokeo yao mabaya na kutokuwa na kiwango kizuri na hivyo wamekuwa na harakati za kuimarisha kikosi chao Januari, huku wakihaha kujaribu kumsajili nyota wa Sporting CP, Bruno Fernandes.

Lakini Solskjaer amesema kusajili mchezaji sahihi lilikuwa jambo muhimu, akishauri kwamba miamba hao wa Ligi Kuu wameshindwa kusajili wachezaji wengine wakati huu wa soko la usajili.

"Ni jambo zuri kujitazama mwenyewe kwenye kioo wakati mwingine na sio kuwalaumu wengine. Na hilo ndio tatizo kwa watu kuwalaumu wengine," amesema.

"Kwa upande wangu, ni suala la kuelewana. Tunatakiwa kutumia fedha kwa umakini na hilo ndio moja ya jambo letu muhimu. Tumetumia fedha nyingi kwa misimu mitano au sita iliyopita, tangu Sir Alex Ferguson alipoondoka.

"Ninatakiwa kuhakikisha kwamba wakati tunapotumia fedha, tunatumia kwa mchezaji sahihi wa klabu hiii.

"Sio kwa mchezaji yoyote ambaye hana ubora na hajui utamaduni wa Manchester United, na ndio maana tunapotaka kufanya usajili tunatakiwa kutulia kuangalia mchezaji yule anayetufaa."

## KWA UFUPI

**SPURS KUMREJESHA BALE**

TOTTENHAM inafanya mchakato wa kumrejesha mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Wales, Gareth Bale (30), kutoka Real Madrid kabla wiki hii ya mwisho ya dirisha la usajili wa Januari halijafungwa. ***(Express)***

**SOUTHGATE ATAJWA UNITED**

MANCHESTER United itafikia uamuzi wa kumfukuza kazi Ole Gunnar Solskjaer kama timu hiyo itaendelea kupata matokeo mabaya katika msimu huu, huku Kocha wa Timu ya Taifa ya England, Gareth Southgate akiwa anaongoza katika orodha ya makocha wanaotajwa kurithi mikoba ya kocha huyo. ***(Mail)***

**CHILWELL KUTUA UNITED**

MABOSI wa Manchester United watafanya mchakato wa kumsajili beki wa kushoto wa Leicester na Timu ya Taifa ya England, Ben Chilwell, ambaye ana umri wa miaka 23, katika majira ya joto. ***(Metro)***

**MORENO AKARIBIA BARCA**

BARCELONA imesitisha mpango wa kumsajili straika wa Gabon na Arsenal, Pierre-Emerick Aubameyang (30), katika dirisha dogo la usajili linaloelekea ukingoni na badala yake itaongeza nguvu kuwania saini ya mshambuliaji wa Hispania na Valencia, Rodrigo Moreno (28). ***(Sport)***

**AUBAMEYANG ANUKIA PSG**

STRAIKA wa Timu ya Taifa ya Gabon na Arsenal, Pierre-Emerick Aubameyang anawindwa na Paris St-Germain ili kuziba pengo litakaloachwa na straika wa Uruguay, Edinson Cavani, ambaye ana umri wa miaka 32. ***(Foot Mercato - in French)***

**CHELSEA, UNITED VITANI**

STRAIKA wa Timu ya Taifa ya Uruguay, Edinson Cavani, anahusishwa na mipango ya kujiunga na Chelsea na Manchester United, huku tayari ameshafikia makubaliano ya awali ya kuhamia Atletico Madrid kabla ya kufungwa kwa dirisha la usajili la Januari. ***(Goal)***

**MITROVIC MAMBO MAGUMU**

TOTTENHAM na Aston Villa haitaendelea na mchakato wa kumwania straika wa Timu ya Taifa ya Serbia, Aleksandar Mitrovic katika dirisha dogo linaloendelea baada ya Fulham kutaka kulipwa pauni milioni 40. Nyota huyo mwenye umri wa miaka 25 anaweza kuondoka katika klabu hiyo kwenye majira ya joto kama Fulham itashindwa kujiokoa na janga la kushuka daraja. ***(Star)***

**MARI AKARIBIA ARSENAL**

ARSENAL inakaribia kukamilisha mchakato wa kumsajili beki wa Flamengo, Pablo Mari ambaye ana umri wa miaka 26. ***(Mail)***

**SMALLING HAKIJAELEWEKA**

MANCHESTER United imekataa kupokea ofa ya pauni milioni 25 ili kumuuza beki wa kati wa Timu ya Taifa ya England, Chris Smalling, huku Roma ikijiandaa kukamilisha mchakato wa kumpa mkataba wa kudumu nyota huyo ambaye yuko kwa mkopo katika ligi hiyo ya Serie A. ***(Sun)***

**UNITED, SPORTING WATETA**

MANCHESTER United bado inaendelea na mchakato wa kuwania saini ya kiungo wa Sporting Lisbon na Timu ya Taifa ya Ureno, Bruno Fernandes (25), lakini bado klabu hizo mbili hazijaafikiana kuhusu dau la kukamilisha usajili huo. ***(A Bola - in Portuguese)***

**NEWCASTLE, VALENCIA VITANI**

NEWCASTLE inaamini itaizidi ujanja Valencia katika kuwania saini ya straika wa Borussia Dortmund na Timu ya Taifa ya Hispania, Paco Alcacer (26), ambaye anapatikana kwa mkataba wa mkopo. ***(Sun)***

HABARI MICHEZO

# MAXIMO ATOBOA SIRI ALIVYOMWIBUA SAMATTA

**Na Somoe Ng'itu**

ALIYEKUWA Kocha Mkuu wa timu ya Taifa (Taifa Stars), Marcio Maximo, amesema Tanzania ina wachezaji wengi wenye vipaji vya kucheza soka la kulipwa katika klabu mbalimbali za Ulaya, lakini wanakosa misingi bora ya kuwaibua.

Kauli hiyo ya Maximo imekuja siku chache baada ya nahodha wa Taifa Stars, Mbwana Samatta kusaini mkataba wa miaka minne na nusu wa kuitumikia Aston Villa inayoshiriki Ligi Kuu England.

Maximo ambaye kwa sasa anaifundisha Timu ya Taifa ya Guyana aliliambia gazeti hili anajivunia mafanikio ya Samatta kwa sababu yeye ndiyo kocha wa kwanza kumuita mshambuliaji huyo kulitumikia taifa.

"Nimefurahi na nimefarijika kwa mafanikio ambayo ameyapata Samatta, lakini bado wachezaji wenye kiwango kama chake wako wengi Tanzania, ila wanakosa watu wakuwaongoza," alisema Maximo ambaye aliifundisha Taifa Stars kuanzia mwaka 2006 mpaka 2010.

Kocha huyo alisema kuwa licha ya kupigiwa kelele na wadau wa soka kwa uamuzi wake wa kuwatumia zaidi wachezaji vijana, hakusika kuendelea na utaratibu wake huo ambao sasa matunda yake yameanza kuonekana.

"Mara ya kwanza namuita Samatta katika kikosi cha Stars alikuwa na umri chini ya miaka 20, nilifanikiwa kumjenga kwa kumpa misingi ya uchezaji na sasa amefikia hapo alipo, niliziba masikio, sikutaka kusikiliza maneno ya watu," Maximo aliongeza.

Alisema kuwa mbali ya Samatta ambaye alimuita akitokea African Lyon, katika kikosi chake pia kilikuwa na wachezaji wengine vijana wakiwamo Jerryson Tegete, Mrisho Ngasa, Yusuph Soka, John Bocco, Kigi Makasi na Himid Mao.

"Samatta alikuwa na kipaji cha hali ya juu pamoja na kutoa ushindani wa kuwania namba ndani ya Taifa Stars," alisema Maximo ambaye alirejea nchini na kuifundisha Yanga kwa muda mfupi.

"Mipango yangu ilikuwa ya baadaye na wala haikuwa ya wakati ule, baadaye walianza kuona matunda ambapo wachezaji wote walikuwa nyota na kutaikiwa kimataifa, Samatta alikuwa na kipaji kikubwa pamoja na baadhi ya watu kupinga, hata hapo alipojiunga na Simba, alikuwa na kipaji na kucheza nusu msimu na baadaye kujiunga na TP Mazembe," alisema Maximo.

Aliongeza kuwa kama mambo yatabalidilika, Tanzania itatoa wachezaji nyota wengi hapo baadaye kwa sababu ina wachezaji wenye vipaji.

"Naweza kusema kuwa Tanzania ina wachezaji wengi wenye vipaji kushinda nchi za Afrika Magharibi, lakini jinsi gani ya kuwavumbua na kupata nafasi ya kuonekana ni shida. Leo hii tunamzungumzia Samatta ambaye ametokea Mbagala Market. Kipaji chake cha hali ya juu ndicho kimemfanya afike hapa alipo," alisema Maximo.

Alimaliza kwa kuwataka wachezaji wengine kuendelea kujituma na muda sahihi utakapofika, wataonekana na klabu za Afrika au nchi za Ulaya.

"Naipenda sana Tanzania, najua ipo siku moja nitakuja na kitu ambacho wadau wa soka hawatasahau katika kumbukumbu zao, bado nina majukumu mengine, lakini naamini soka la Tanzania lina tija na kuna vijana wengi wenye vipaji kama Samatta," aliongeza.




Beki wa Simba, Shomary Kapombe (chini), akiokoa mpira uliokuwa unaelekea katika lango la timu yake katika mechi ya mashindano ya Kombe la FA dhidi ya Mwadui iliyochezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Chipukizi Zanzibar, Bara kujumuishwa

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Etienne Ndayiragije, amesema Zanzibar ina wachezaji chipukizi wenye vipaji vya kucheza soka katika kiwango cha juu hapo baadaye, kama watafanya mazoezi zaidi.

Ndayiragije alisema hayo baada ya kushuhudia mechi mbili za Timu ya Taifa ya vijana ya umri chini ya miaka 16, zilizochezwa kwenye Uwanja wa Amaan Visiwani hapa.

Akizungumza na gazeti hili, Ndayiragije alisema endapo nyota hao watasimamiwa vema na kufuata programu mbalimbali za mazoezi, wana nafasi ya kutoa mchango katika katika timu ya Taifa ya vijana.

Kocha huyo alisema wapo vijana ambao wamecheza vizuri na wakichanganywa wenzao wa Tanzania Bara na kufanya mazoezi ya pamoja, nchi itakuwa na kikosi imara ambacho kitaandaliwa kwa ajili ya kushiriki katika mashindano mbalimbali.

Hata hivyo, Ndayiragije hakuwa tayari kutaja majina ya wachezaji ambao amewateua kwa ajili ya kuungana na wenzao wa Bara ili kuunda kikosi cha Tanzania.

Mrundi huyo alishauri timu za vijana kuwa na makocha wa mazoezi ya viungo ili kuwajenga imara wachezaji kama ilivyo kwa klabu na timu nyingine za Taifa.

Katika mechi ya kwanza ya kirafiki, Timu ya Tanzania Bara ilipata ushindi wa mabao 5-1 dhidi ya wenzao wa Zanzibar na katika mchezo wa marudiano, timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1.

# Azam FC, Friends hapatoshi FA leo

**Na Mwandishi Wetu**

KIKOSI cha Azam FC kinatarajia kuwakaribisha Friends Rangers inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza katika mechi ya raundi ya nne ya mashindano ya Kombe la FA itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Azam FC ndio mabingwa watetezi wa michuano hiyo inayotoa mwakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Azam FC, Iddi Cheche, alisema wamejiandaa vizuri kuelekea mchezo huo na wanaamini utakuwa na ushindani.

Cheche alisema Friends Rangers ni moja ya timu zenye ushindani na wamekutana katika nyakati tofauti kwenye mechi za kirafiki.

**"Tutacheza kwa tahadhari zaidi kwa sababu mashindano haya ni ya mtoano, ni mchezo mgumu sana, tumejiandaa imara kuwakabili ili tusonge mbele," alisema Cheche.**

Aliongeza kuwa kikosi chake kimeimarika na sasa wanahitaji kuendelea kupata matokeo chanya katika kila mechi iliyoko mbele yao ili kutimiza malengo waliyojiwekea kwa msimu huu.

Naye Ofisa Habari wa Azam FC, Jaffer Iddi, alisema kikosi chao kilirejea salama kutoka Shinyanga na kila mchezaji yuko tayari kwa mechi ya leo.

Iddi alisema wamejipanga kuendeleza kutoa 'dozi' baada ya kupata ushindi wa mechi tano mfululizo katika Ligi Kuu Tanzania Bara.

Timu ambazo zimesonga mbele katika mashindano hayo ni pamoja na mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba, Gwambina, Alliance, JKT Tanzania, Ndanda FC, Ihefu na Sahare All Stars.

Azam FC ilitwaa ubingwa wa michuano hiyo baada ya kuwafunga Lipuli FC bao 1-0 katika fainali iliyochezwa kwenye Uwanja wa Ilulu mkoani Lindi.

Fainali za msimu huu zinatarajiwa kuchezwa Mei 30, mwaka huu kwenye Uwanja wa Nelson Mandela mkoani Rukwa.

Michezo
Jumatatu Januari 27, 2020
Nipashe



Solskjaer afunguka haogopi kufukuzwa HABARI UK 30



Mshambuliaji wa Yanga, Bernard Morrison, akipambana kumtoka beki wa Tanzania Prisons, Michael Ismail katika mechi ya Kombe la FA iliyochezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam jana. Yanga ilishinda 2-0. **PICHA : JUMANNE JUMA**

# YANGA YATAKATA FA

## Morrison, Yikpe waongoza 'mauaji' dhidi ya Tanzania Prisons, sasa kukutana na Gwambina FC ya Mwanza...

**Na Adam Fungamwango**

MABAO mawili ya wachezaji wa kigeni, Mghana Bernard Morrison na raia wa Ivory Coast, Yikpe Gislain, yaliipeleka Yanga kwenye hatua ya 16 Bora ya michuano ya Kombe la FA baada ya kuwafunga Tanzania Prisons magoli 2-0, katika mechi iliyopigwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Ushindi huo, ni wa pili mfululizo, ikiwa ni mwezi mmoja tu uliopita, Desemba 27, mwaka jana Yanga walipoifunga Tanzania Prisons bao 1-0 katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara, Uwanja wa Samora mjini Iringa, mchezo wa kwanza Maafande hao kupoteza.

Kwa matokeo hayo, Yanga sasa itakutana na Gwambina FC inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara, ambayo imeitoa kwenye mashindano hayo timu ya Ruvu Shooting ya Mlandizi, mkoani Pwani.

Yanga ilianza biashara asubuhi, dakika ya 10 tu ilipata bao lililofungwa na winga wake machachari, Morrison kwa mkwaju wa penalti baada ya beki wa Tanzania Prisons, Michael Ismail kuunawa mpira kwenye eneo la hatari.

Kabla ya goli hilo, Prisons ilikuwa imepata nafasi safi dakika ya nane, lakini Adili Buha alipiga mpira juu ya lango na kupoteza nafasi hiyo ya kufunga bao la mapema katika mchezo huo wa raundi ya nne.

Yanga ilikosa bao la wazi dakika ya 30, baada ya kutokea patashika kwenye lango la Prisons, lakini wachezaji wake wakiongozwa na David Molinga walikuwa wakipiga mashuti yaliyokuwa yakiwagonga mabeki wa wageni hao na kipa wao Jeremiah Kasubi, hatimaye ukaokolewa.

Prisons walikaribia kusawazisha dakika ya 35, baada ya shuti la Salum Kimenya ambaye alifanikiwa kuwatoka mabeki wa Yanga kugonga mwamba wa juu na kutoka nje.

Kipindi cha pili Yanga iliongeza kasi ya mashambulizi langoni mwa wapinzani wao, huku Prisons ikishambulia kwa kushtukiza, lakini kadri muda ulivyozidi kusonga mbele wachezaji wake walionekana kuchoka na kuruhusu Yanga kutawala mchezo huo.

Yikpe, aliyeingia kuchukua nafasi ya Mkongomani Molinga aliyeumia, aliihakikisha Yanga ushindi baada ya uzembe wa kipa Jeremiah kushindwa kutoka mapema kuufuata mpira mrefu uliopigwa na Morrison, badala yake alitoka muda mfupi kabla ya mfungaji kuufikia mpira na kuujaza wavuni kwa kichwa.

Samson Mbangula aliyeingia badala ya Kimenya naye alipoteza nafasi ya kufunga bao hata la kufutia machozi dakika za mwisho za mchezo, alipopiga shuti lililookolewa kwa ustadi na kipa wa Yanga, Metacha Mnata.

Mashindano hayo yanatarajiwa kuendelea tena leo kwa mabingwa watetezi, Azam FC kuikaribisha timu ya Ligi Daraja la Kwanza, Friends Rangers ya Magomeni jijini.

Bingwa wa michuano hiyo, atapata tiketi ya kuiwakilisha Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

# Kiwango Simba chamkera Sven

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya kusonga mbele katika mashindano ya Kombe la FA, Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck, hajafurahishwa na kiwango kilichoonyeshwa na timu yake katika mchezo wa raundi ya nne dhidi ya Mwadui FC, kutoka Shinyanga.

Ikitokea nyuma, Simba imesonga mbele katika mashindano hayo ambayo hutoa tiketi ya kushiriki michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika baada ya kupata ushindi wa mabao 2-1.

Sven aliliambia gazeti hili timu yake imeonekana kuwa kuna tatizo la kukosa mawasiliano na kufanya wapoteze nafasi nyingi za kufunga mabao na hivyo kujiweka katika nafasi isiyofurahisha.

"Tulikuwa na uwezo wa kufunga mabao mengi, ila wachezaji wangu walishindwa kuwa na mawasiliano mazuri ndani ya uwanja jambo ambalo limewafanya wavune ushindi mwembamba, tulistahili kufunga mabao mengi zaidi ya haya mawili tuliyopata," alisema Mbelgiji huyo.

Bao la kwanza la kusawazisha la Simba lilifungwa na Mzambia Clatous Chama na lile la ushindi likipachikwa kimiani na Mkenya Francis Kahata, wakati Gerald Mdamu aliifungia Mwadui bao pekee katika mchezo huo.

# Wapinzani Stars CHAN Februari

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), itajua wapinzani wake wa fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), katika droo maalumu iliyopangwa kufanyika Februari 17, mwaka huu jijini kwenye ukumbi wa michezo wa Palais Polyvalent des Sports ulioko mjini Yaoundé nchini Cameroon, imeelezwa.

Fainali za mashindano hayo yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (Caf), zinatarajiwa kuchezwa kuanzia Aprili 4 hadi 25 mwaka huu katika miji ya Yaounde, Douala na Limbe.

Taifa Stars inayonolewa na kocha raia wa Burundi, Etienne Ndayiragije, ilipata tiketi ya kushiriki fainali hizo kwa mara ya pili baada ya kuwaondoa majirani zao Kenya maarufu Harambee Stars na baadaye Sudan.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >